**28 APRILI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 28 Aprili, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU WA MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na maswali Ofisi ya Rais TAMISEMI ninamwita Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi aweze kuuliza swali lake.

Na. 185

**Kuongeza madarasa Shule ya Msingi Puma – Ikungi**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaongeza madarasa katika Shule ya Msingi Puma kutokana na kuzidiwa na idadi ya wanafunzi?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Deo Ndejembi Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Jimbo la Singida Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa kutokana na utekelezaji wa sera ya elimu bila ada, kumepelekea ongezeko kubwa la wanafunzi na uhitaji wa miundombinu ya shule ikiwemo madarasa. Hatua mbalimbali za kukabiliana na uhitaji wa miundombinu ya shule zinaendelea kufanywa na Serikali katika halmashauri, manispaa na majiji hapa nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na ongezeko kubwa la wanafunzi katika shule ya Msingi Puma, Katika bajeti ya mwaka 2023/2024 shule hii imetengewa madarasa mawili sambamba na ufunguzi wa shule shikizi Isalanda ambayo itasaidia pia kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule ya msingi Puma.

**MWENYEKITI:** Nimemuona Mheshimiwa Kingu, swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya kaka yangu Naibu Waziri Deo Ndejembi nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Shule ya Msingi ya Muhintiri inakabiliwa na changamoto hizo hizo ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa majibu kwa Shule ya Puma.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuambatana na mimi kwenda jimboni kujionea msongamano mkubwa wa wanafunzi katika shule hiyo na kuangalia namna ya kuweza kuwasaidia wanafunzi wa Shule Msingi ya Muhintiri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu, bila kurudia majina yake kwa sababu anafahamika.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Kingu kuelekea katika shule hii ya Muhintiri ili kujionea msongamano huo na kuweza kuona ni hatua gani Serikali inaweza ikachukua kuweza kutoa msongamano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; je, ni lini sasa Serikali itaimarisha Shule za Msingi Salakwa, Salama A na Salama B, Salama na Nyarubundu; ni lini majengo ya shule hizi yamezeeka sana, ya muda mrefu, lini Serikali itatekeleza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kama utakuwa nayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba baada ya *session* hii ya maswali nikae na Mheshimiwa Getere kuweza kuona ni hatua gani tunaweza tukazichukua za haraka kuweza kuzifanyia shule hizi matengenezo ambayo zinahitaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante, ninamwita Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate Mbunge wa Tunduru Kusini aweze kuuliza swali lake.

Na. 186

**Hitaji la Shule za Kidato cha Tano na Sita Tunduru Kusini**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga shule ya Kidato cha Tano na Sita katika Jimbo la Tunduru Kusini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Daimu Idi Mpakate, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uhitaji wa shule za kidato cha tano na sita kwa maeneo mengi hapa nchini, Shule ya sekondari ya Mchoteka katika jimbo la Tunduru, wazazi pamoja na halmashauri walijenga hosteli mbili ambazo zimekamilika; hostel moja ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshapeleka kiasi cha shilingi milioni 160 kwa ajili ya kuongeza miundombinu mingine ili kukidhi vigezo vya kupandisha hadhi shule. Hata hivyo, shule hii imeombewa usajili wa mkondo walau mmoja wa kidato cha tano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa wananchi wako tayari kukamilisha majengo ya madarasa ambayo Serikali imetoa shilingi milioni 260 na uwezekano upo ndani ya miezi miwili majengo haya yakakamilika.

Je, anihakikishie Naibu Waziri mwezi Julai ujasili na uanzwaji wa kidato cha tano utakuwa tayari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Shule ya Sekondari Mchoteka ina walimu watano tu wa sayansi.

Je, kukamilisha kidato cha tano na sita Serikali itapeleka walimu wa sayansi zaidi ili watoto wale wawe na ufaulu mzuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hii kama nilivyokwishakusema kwenye majibu yangu ya msingi imeombewa usajili kutoka Wizara ya Elimu. Na kuona kama itakuwa tayari mwezi wa saba kuweza kupokea wanafunzi tutalifanyia kazi hili kwa haraka sisi Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kuweza kupata usajili na kuona kama itaweza kupokea wanafunzi mwezi huu wa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la ukosefu wa walimu wa sayansi. Bunge lako tukufu ni mashahidi kwamba Serikali imetoa ajira zaidi ya 21,000 ambapo katika hizo zipo za walimu na zipo za Idara ya Afya. Hivyo basi katika ajira hizi tutaiwekeza kipaumbele Shule hii ya Sekondari ya Mchoteka.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Nimemwona Mheshimiwa Husna Sekikobo aulize swali lake la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali moja. Shule ya Sekondari *Kilindi Girls* na Shule ya Sekondari Mlongwema zilizopo Wilaya ya Lushoto zina upungufu mkubwa wa mabweni lakini zinachukua watoto *all over the country,* ni *form five* na *six.*

Je, ni lini Serikali itapeleka mkakati maalum wa kuongeza mabweni katika shule hizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali upo wa kuendelea kutafuta fedha kuhakikisha kwamba shule zote zenye uhitaji wa mabweni yanaweza kujengwa. Nitoe rai kwa

viongozi wa Halmashauri hii ya Lushoto na Kilindi kuanza kuhamasisha wananchi kuanza ujenzi wa mabweni na Serikali inaweza ikaja kuja kuyamalizia majengo hayo kama walivyofanya kule Mchoteka kwa Mheshimiwa Mpakate.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba niulize swali moja fupi. Kwa vile Kata ya Mamba Kaskazini na Mamba Kusini kuna shule nyingi za sekondari lakini hatuna shule hata moja ya kidato cha tano na sita.

Je, Serikali iko tayari kuipandisha hadhi Shule yaSekondari ya Mboni kwa kuijengea pia hosteli?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye shule hizi ambazo amezitaja Mbunge za Mamba Kaskazini na Mamba Kusini, utaratibu ni ule ule kuweza kujenga miundombinu ambayo inatakiwa ili kupandisha hadhi shule halafu kuiombea usajili kutoka Wizara ya Elimu. Tutakaa na Mheshimiwa Mbunge kuona shule hizi kama miundombinu inakidhi vigezo, na kama inakidhi vigezo basi tuone taratibu za kuombea usajili wa kuweza kupata mkondo wa kidato cha tano na sita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daktari Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Shule ya Sekondari ya Kumkubwa ni shule ya kidato cha tano na sita inayotumia majengo chakavu yaliyokuwa kambi ya wakimbizi.

Je, ni lini Serikali itajengea miundombinu ya madarasa katika Shule hii ya Sekondari ya Kumkubwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lengo la Serikali kuboresha miundombinu ya shule zote, si tu za sekondari, kuanzia za msingi, sekondari na hizi za *A-level.* Hivyo basi tutaona ni namna gani ambavyo tunaweza tukaanza ukarabati wa shule hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, swali langu, nataka kujua ni lini Serikali itaanza ujenzi wa shule ya mkoa ya mfano ya wasichana katika Mkoa wa Mtwara kama ilivyojenga kwenye mikoa mingine?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kujenga shule hizi katika kila mkoa na tayari bilioni 30 ilishatoka kwa ajili kujenga shule kumi kwenye mikoa kumi ambao kila mkoa ilipata bilioni tatu. Tunaenda sasa kwenye hatua ya pili ambapo mikoa mitano itapokea hizi bilioni tatu pia kujenga na awamu ya tatu pia tutamalizia hizo shule nyingine na tutahakikisha Mkoa wa Mtwara pia nao unapata shule hii kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Tabasamu Hamis Mwagao Mbunge wa Sengerema aweze kuuliza swali lake. Swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Furaha Matondo.

Na. 187

**Mpango wa Sekondari ya Sengerema kuwa Chuo cha Madini na Uvuvi**

**MHE. FURAHA N. MATONDO K.n.y. MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza: -

Je, mpango wa kutumia majengo ya Sekondari ya Sengerema kuwa Chuo cha Madini na Uvuvi umefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Jimbo la Sengerema, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari Sengerema ni miongoni mwa shule za Sekondari kongwe hapa nchini. Shule hii inachuka wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita kutoka nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapanga kuongeza nafasi kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha Tano na Sita, kutokana na wanafunzi wanao maliza kidato cha nne kuongezeka sana. Mpango wa kuifanya Shule ya Sekondari Sengerema kuwa Chuo cha Madini na Uvuvi hauwezekani kutokana na uhitaji wa shule hii kwani kubadili matumizi ya

shule hii kutaongeza uhaba wa nafasi za wanafunzi wa kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais TAMISEMI haijashirikishwa kwa namna yoyote kuhusu kubadili matumizi ya shule ya Sekondari Sengerema. Hivyo, tunawaomba wenzetu wa Wizara ya Madini kuja mezani na kujadiliana juu ya jambo hili, hasa ikizingatiwa kuwa kwa sasa tuna uhitaji mkubwa wa shule za kidato cha tano na sita. Aidha tunaomba kuwashauri Wizara ya Madini kutafuta eneo na fedha kwa ajili ya kujenga chuo kitakachojihusisha na kada ya madini kuliko kubadili matumizi ya Sekondari hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha Matondo swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nashukuru majibu mazuri ya Serikali lakini niombe tu kwa kuwa maeneo ya kanda ya ziwa yamezungukwa na madini ya kila aina.

Je, hamuoni haja ya kujenga chuo cha madini katika Wilaya ya Sengerema ili kuwapatia wananchi wetu wapate ujuzi lakini waweze kuchimba kitaalamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa, kuwa sasa uvuvi umekuwa ni wa kisasa;

Je, hamuoni haja ya kujenga chuo cha uvuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ili wavuvi wetu waweze kuvua kitaalam tuendane na kasi ya Uganda nan chi nyingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI una hiari ya kujibu maswali hayo kama itakuwa kwenye sekta yako.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo umesema hapa haya masuala ambayo ni yako chini ya Wizara ya Madini. Sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Madini. Swali lake la pili ni la Wizara ya Uvuvi, kuona mipango waliyonayo juu ya kuweka vyuo hivi katika kanda ya ziwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha Matondo unaweza kuleta kama swali la msingi halafu yakawekewa utaratibu mzuri haya maswali yako.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na maswali ya nyongeza namwita Mheshimiwa Issa Mchungahela swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametamka uhaba wa shule za A-*Level* na jambo hilo limejityokeza katika jimbo langu. Mpaka sasa hivi kuna A-*Level* mbili tu zinazofanya kazi wakati kuna kata 18 na tulishaomba kupandisha hadhi Shule ya Makong'onda kuwa A- *Level;* mchakato huu wa kupandisha hadhi utakamilika lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kupandisha hadhi shule kuwa na mkondo wa kidato cha tano na sita ni upo chini ya Wizara ya Elimu, maombi yale yanapelekwa Wizara ya Elimu. Nitakaa na Mheshimiwa Mchungahela kuona mchakato huu umefikia wapi na kuweza kumpa majibu hayo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa kuuliza swali lenye uhusiano wa moja kwa moja na swali la msingi ili Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kulijibu. Hamna aliyeomba swali la nyongeza tunaendelea namwita sasa Mheshimiwa Francis Leonard Mtega Mbunge wa Mbarali aweze kuuliza swali lake.

Na. 188

**Ujenzi wa barabara kati ya Wilaya ya Mbarali na Chunya**

**MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga barabara ya mkato kati ya Wilaya za Mbarali na Chunya ili kupunguza gharama za usafiri na kukuza biashara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa umbali kutoka Wilaya ya Chunya hadi Wilaya ya Mbarali kwa kupitia Wilaya ya Mbeya ni mrefu ukilinganisha na umbali wa kupitia barabara ya mkato kati ya Wilaya ya Chunya na Mbarali. Serikali inatambua changamoto ya kutokuwepo kwa barabara hiyo na kusababisha adha ya mzunguko mrefu kwa wananchi wa wilaya hizo mbili ndani ya mkoa wa Mbeya na kusababisha gharama kubwa kwa wananchi wanaosafiri kati ya wilaya hizo mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa uhitaji wa barabara hiyo ya mkato, Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mbeya kupitia kikao chake cha tarehe 09 Januari, 2023, kilitoa mapendekezo kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kuipandisha hadhi barabara ya Njiapanda – Sangambi – Shoga na kufungua barabara mpya kutoka Shoga Wilaya Chunya hadi Udindilwa katika Wilaya ya Mbarali inayokadiriwa kuwa kilomita 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mapendekezo hayo kuwasilishwa kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, aliiagiza Kamati ya Kitaifa ya kupanga barabara katika hadhi stahiki *(NRCC)* kufika mkoani Mbeya na Kamati hiyo ilifika mnamo tarehe 24 Februari, 2023 na kutembelea barabara zilizoombwa kupandishwa hadhi ikiwemo barabara ya Njiapanda – Sang'ambi – Shoga na kipande cha Shoga - Udindilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kamati yaliwasilishwa kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na yanachambuliwa na uchambuzi ukikamilika taarifa itatolewa. Kama barabara hiyo itakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi, itakuwa barabara ya mkoa na itahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali; lakini hata hivyo nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara ni moja ya barabara ambazo wananchi wa Mbarali wanazitumia sana kusafirishia mazao na sasa barabara nyingi zimeharibiwa mno na mvua hali inayopelekea ugumu wa kufanya shughuli hizi.

Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa wanambarali kuhusu adha hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge, barabara nyingi ambazo zimeharibika kutokana na msimu huu wa mvua zimewekewa kipaumbele cha matengenezo katika mwaka huu wa fedha tunaoenda kuuanza Julai, Mosi mwaka huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nataka nijue Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya mkato inayotoka Komaswa – Tarime Vijijini kuja mpaka Rorya kupitia Nyatorogo pamoja na Daraja lake la Nyatorogo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kama ina mpango wowote wa ujenzi wa daraja pamoja na barabara hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaweza ukataja vizuri hizo barabara zako kutoka wapi mpaka wapi?

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayotoka Komaswa – Tarime Vijijini kuja Rorya kwa kupitia Kata ya Nyatorogo ikiwa ni pamoja na daraja lake linalounganisha Tarime Vijijini pamoja na Rorya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakaa na Mheshimiwa Mbunge

kwanza kuona kwamba barabara hii ni ya *TARURA* au ya *TANROADS* halafu kuona ni hatua gani ambazo tunaweza tukazichukua kuweza kufungua Barabara hii ya mkato ya Komaswa hadi Rorya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nishukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kipindi hicho Ummy Mwalimu aliahidi shilingi bilioni 1.5 kuunganisha Wilaya ya Tanganyika na Wilaya ya Uvinza kupitia Kata ya Kalia na Kata ya Mwese.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo ili wananchi waweze kupata huduma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hii ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutakaa na wenzetu wa *TARURA* kuona mpango wao juu ya kutenga fedha hii ya bilioni 1.5 ya kuunganisha barabara kati ya Tanganyika hadi Uvinza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE J. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona. Barabara inayoanzia Chunya Mjini kupita Igundu mpaka Sangambia ambako itaunganisha na Mbarali kwa kipindi hiki imeharibika sana kutokana na changamoto za mvua. Je, ni Serikali itatenga fedha hili barabara hii ijengwe kwa kiwango cha changarawe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* ina bajeti ya bilioni 11 kwa ajili ya dharura na hivi sasa maombi tayari yamefanyika kwa ajili ya kuongeza bajeti hii kwenda bilioni 46 ili kuhakikisha wana fedha ya kutosha kuweza kutengeneza barabara hizi wakati wa dharura. Kwa sasa tutaangalia barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge kuona katika mwaka fedha unaoenda kuanza tarehe 1, Julai inapewa kipaumbele cha kutengenezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Tuna ahadi ya Waziri wa TAMISEMI katika Wilaya ya Kibiti kutoa fedha kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kibiti Mjini kwenda kule kwenye Halmashauri yetu ya Kibiti.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha hizo kukamilisha ujenzi huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri ya Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutakaa na wenzetu wa *TARURA* kuona ni namna gani wamejipanga katika kutekeleza ahadi ya hii ya Mheshimiwa Waziri ya kuweka barabara ya lami kutoka Kibiti Mjini mpaka ambapo wamejenga halmashauri yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahadi ya Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu ni kuiunganisha Kata ya Nyahua na Makao Makuu ya Wilaya ya Sikonge na zilitengwa bilioni 1.86 mwaka juzi na mwaka jana, lakini haijatoka hata senti moja. Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza hiyo ahadi kwa kutoa hizo fedha ambazo zilitengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeshawajibu Waheshimiwa Wabunge wengine hapa kwamba, kwa kuwa hii ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutakaa na wenzetu wa *TARURA* kuona ni namna gani wamejipanga katika utekelezaji wa ahadi hii.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Dejembi kwa majibu mazuri, hakuna Mbunge aliyesimama tena kwa ajili ya kuuliza swali la nyongeza, ahsante sana.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namwita Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, aweze kuuliza swali lake.

Na 189

**Kesi za wakulima kulishiwa mazao yao Mvomero**

**MHE. JONAS V. ZEELAND** aliuliza: -

Je, ni kesi ngapi za Wakulima kulishiwa mazao yao zimeripotiwa na ngapi zimepelekwa Mahakamani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jumanne Sagini, Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashauri ya kesi za wakulima kulishiwa mazao yao zilizoripotiwa Vituo vya Polisi katika Wilaya ya Mvomero kuanzia Januari, 2022 hadi Machi, 2023, ni jumla ya Mashauri 343. Kesi zilizofikishwa mahakamani ni 184. Kati ya hizo kesi 119 zimehukumiwa, kesi 65 zinaendelea kusikilizwa mahakamani na kesi 159 zipo kwenye hatua mbalimbali za uchunguzi na upelelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI.** Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa yapo malalamiko kwa baadhi ya askari wako kutotenda haki ikiwemo kuchukua rushwa na kuziharibu hizi kesi za migogoro ya wakulima na wafugaji, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongozana nami baada ya Bunge hili la Bajeti kwenda kuwasikiliza wananchi wa Mvomero? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kutokana na jiografia yetu ya Mvomero, tuna uhaba mkubwa wa vituo vya polisi. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutuongezea Vituo vya Polisi lakini pia kuvimalizia Vituo vya Polisi vilivyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi kikiwemo Kituo cha Polisi Turiani na Kituo cha Polisi Mvomero? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwepo wa madai ya rushwa na kwamba Mheshimiwa amependekeza niende Mvomero pamoja naye kuwasilikiliza wananchi, hilo halina shida Mheshimiwa tutaongozana. Hata hivyo pale zinapokuwepo tuhuma za rushwa ushauri wangu wananchi waelekezwe kwenda kwenye vyombo vinavyosimamia sekta hiyo. Tunayo TAKUKURU kila Wilaya, kila Mkoa na Taifa, lakini kama inashindikana kuna Kamati ya Usalama inayoongozwa na Mkuu wa Mkuu wa Wilaya wanaweza wakapeleka manung'uniko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wapo Wakuu wa Mapolisi hawa wadogo wanaokuwa kwenye *site* kama *OCD* wanaweza pia kuwasikiliza, lakini nipo tayari kuungana naye kwenda kuwasikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya swali la pili la kuongeza Vituo vya Polisi kwa sababu Wilaya ni pana, nitakapokwenda kwenye kikao hicho tutaweza kuviangalia vituo viwili vinavyoendelea kujengwa na kupata mapendekezo yako ni wapi kwingine wanapenda viongezwe ili viweze kuingizwa kwenye mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza katika Jimbo la Kilwa Kusini, Kata za Nanjilinji, Kikole na Kiranjeranje bado migogoro ya wakulima na wafugaji inaendelea. Je, ni nini jukumu la Jeshi la Polisi kuzuia na kukomesha kabisa migogoro hii badala ya kuendelea na kesi ambazo hatima yake inakuwa si nzuri sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwepo wa migogoro katika eneo la Kilwa alilotaja Mheshimiwa Mbunge ni kweli tunafahamu na kuna maelekezo yalitolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Wakuu wote wa Mikoa ambao ni Wenyeviti wa Kamati za Usalama na wadogo zao kwa maana ya Wakuu wa Wilaya, Wenyeviti wa Kamati za Usalama ngazi ya Wilaya kuwa na mipango ya usimamizi wa matumizi bora ya ardhi pamoja na kuwapanga wakulima na wafugaji kuepuka mwingiliano unaosababisha migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa Jimbo la Kilwa na hizo kata tatu alizozitaja Mheshimiwa Mbunge nishauri tutumie *infrastructure* kwa maana ya miundombinu iliyopo ya upatanisho, Jeshi la Polisi kupitia Kitengo cha Polisi Jamii wanaendelea kuelimisha wananchi juu ya kupunguza migogoro isiyokuwa ya lazima kama hii. Hata hivyo, tuwaombe wataalam wetu wa ngazi za Serikali za Mitaa ambao hufanya uthamini wa uharibifu wa mazao kabla Polisi hawajachukua hatua za kurejesta kesi Mahakamani ili watimize wajibu wao ipasavyo, kwa sababu wakati mwingine wanaona inachelewa kumbe ni kutokana na kuchelewa kwa zile tathmini za wenzetu. Vinginevyo tuendelee kuwaelimisha

wakulima na wafugaji, wote ni Watanzania, waishi kwa maelewano kila mmoja akitimiza wajibu wake, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ahsante sana.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, namwita Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 190

**Kupitia Muundo wa Utumishi wa Madaktari Bingwa wa Mwaka 2022**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuupitia tena Muundo wa Utumishi wa Madaktari Bingwa wa mwaka 2022?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Molel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na.1 wa mwaka 2009 kwa kada zilizo chini Wizara ya Afya ambao umeainisha miundo na sifa za wataalam mbalimbali wanaopaswa kuajiriwa na kufanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inakamilisha Mapitio ya Miundo ya kada za afya ambayo inatarajiwa kukamilika

Mwezi Mei, 2023 na kuwasilishwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kupata idhini. Miundombinu hii itakapokamilika itaweza kukidhi mahitaji ya kiutumishi kwa wataalam mbalimbali wa afya wakiwemo Madaktari Bingwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Namshukuru Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa sababu swali langu ni swali la kiutumishi, je, Serikali inafahamu tofauti ya kati ya Vyama vya Wafanyakazi ambavyo vinatetea maslahi ya Utumishi na Vyama vya Kitaaluma kwenye kada husika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; linakuja suala zima la uhuishwaji wa maslahi ya kiutumishi je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwa unashirikisha Vyama vya Wafanyakazi ambavyo vimesajiliwa kisheria kutimiza maslahi ya wafanyakazi ili kuepusha sintofahamu ambayo imetokea kwa uhuishwaji wa mwaka jana 2022 kutangazwa kwamba Daktari Bingwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Alice siyo tu kwa kufuatilia masuala ya Watumishi na Madaktari Bingwa, lakini kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kusaidia wenzetu wa Mkoa wa Pwani haswa kwenye maeneo ya afya na masuala ya akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema katika swali lake la kwanza, je, tunafahamu tofauti ya vyama na vile vya kitaaluma. Ndiyo tunafahamu kuna Vyama vya Wafanyakazi

lakini kuna vya Kitaluuma kama ambayo mimi na yeye tupo cha Madaktari cha Tanganyika tunafahamu tofauti ya hivyo viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile swali lake la pili kwamba je, wakati wa kuamua haya tunawashirikisha. Ndiyo maana imechelewa ni kwamba baada ya kutengeneza ile *draft* na kuona matatizo ambayo na wewe umeyaona hasa tunapofika kuna Madaktari *super specialist* ambao sasa kwenye muundo hawatambuliki, kuna watu walioongeza elimu kama manesi wengine wameongeza elimu lakini haifiki kwenye muundo, tulivyoyaona hayo tumemaliza sisi kama Wizara. Sasa tunataka tushirikishe hivyo vyama vyote, tukishashirikisha sasa, wakishakubali wote tunapeleka utumishi sasa kitu ambacho ni shirikishi na kimekubalika na pande zote.

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Afya, ahsante sana.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango namwita Mheshimiwa Grace Victor Tendega Mbunge wa Viti wa Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 191

**Kuondoa kodi kwenye vifaa vinavyotumika na watu wenye ulemavu**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuondoa kodi kwenye vifaa vinavyotumiwa na Watu wenye Ulemavu wakati wa kuingia nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* SURA 148 na ushuru wa forodha kwenye vifaa vilivyotengenezwa mahsusi kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu. Msamaha wa *VAT* umeainishwa katika kipengele cha 8 na 12(d) cha Jedwali lililopo kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vilivyopewa msamaha wa kodi ni pamoja na baiskeli na magari yaliyotengenezwa mahususi kwa matumizi ya watu wenye ulemavu. Vile vile, Serikali imetoa msamaha wa *VAT* kwenye huduma za elimu zinazotolewa katika vituo vya mafunzo ya mwili na akili kwa watu wenye ulemavu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana naomba nimwite Mheshimiwa Grace Victor Tendega, aulize swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwanza kabla ya swali langu nitoe utangulizi, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema msamaha wa kodi uliotolewa ni baiskeli pamoja na magari mahususi kwa matumizi ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlemavu wa macho au asiyoona hivi gari lake linafananaje? Naomba kuuliza swali la kwanza; Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inatoa msamaha wa kodi kwa watu wenye ulemavu wa macho na vifaa vingine vyote wanavyoleta iwe sawa kama

wale wenye ulemavu wengine waweze kupata msamaha wa kodi hiyo na kuleta unafuu wa maisha yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kumekuwa na baadhi ya Watendaji wa Wizara hiyo ambao wanahusika na utoaji wa msamaha wa kodi wakiwatoza kodi wenye ulemavu na katika majibu ya Mheshimiwa Waziri ameonyesha msamaha wa kodi unatolewa. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari nimletee watu wenye ulemavu ambao wametozwa kodi wakati wanahitaji msamaha huo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tendega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu maswali hayo, naomba nimpongeze sana kwa kiasi ambacho anawapigania ndugu zetu wenye ulemavu. Swali lake la kwanza kama nilivyojibu katika swali la msingi ni vifaa tu mahususi ambavyo wanatumia ndugu zetu wenye ulemavu ndivyo ambavyo vinapata msamaha, lakini maoni yake tunayachukua, tunaenda kuyaangalia kama yanaleta tija kwa pande zote mbili kwa walengwa na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, siwezi kukataa kukutana na ndugu zetu, wananchi wenzetu wenye ulemavu na watu wengine wote mimi niko tayari kukaa nao, lakini naomba baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu nikae na Mheshimiwa Mbunge tuone kwa kiasi gani tunaweza tukapata ufumbuzi wa suala hilo na kuwasaidia ndugu zetu hawa wenye ulemavu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Chande kwa majibu yako.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, namwita Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 192

**Ukarabati wa miundombinu chakavu ya vyuo**

**MHE. MWANTUM M. ZODO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati wa miundombinu chakavu katika Vyuo Vikuu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantum Mzamili Zodo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto ya uchakavu wa miundombinu katika Vyuo Vikuu vya Umma hapa nchini. Ili kutatua changamoto ya uchakavu wa miundombinu vyuoni Serikali imefanya ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na Chuo Kikuu cha Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa inaendelea na ukarabati wa miundombinu chakavu na ujenzi wa miundombinu mipya katika Vyuo Vikuu vyote vya Umma 14

na Taasisi tano (5) za Elimu ya Juu zilizopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji vyuoni. Aidha, Taasisi hizi zimekwishapokea fedha kwa ajili ya kuendelea na ukarabati na ujenzi wa miundombinu kupitia Mradi wa Mageuzi ya Uchumi katika Taasisi za Elimu ya Juu *(HEET)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuwa kwenye majibu ya Waziri katika ukarabati wa awali nimesikia baadhi ya Vyuo Vikuu ambavyo vimekarabatiwa, lakini sikusikia Chuo Kikuu cha *UDOM* na kwa kuwa Chuo Kikuu cha *UDOM* kina changamoto sugu ya uhaba wa maji kwa miaka kumi na sita sasa toka 2007, ambayo inapelekea uchakavu wa majengo yale. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali inakwenda kuondoa changamoto ya miundombinu ya maji katika Chuo Kikuu cha *UDOM? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa Chuo Kikuu cha *UDOM* kilikuwa kinajengwa kwa phase na kwa kuwa ujenzi wake bado haujakamilika, kuna uhaba wa madarasa na hakuna kabisa nyumba za watumishi. Je, Serikali imejipangaje sasa kwenda kumaliza *phase* za ujenzi wa Chuo Kikuu cha *UDOM*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilitaja baadhi ya Vyuo ambavyo tayari Serikali imeshapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati na ku–*improve* miundombinu chakavu lakini sikutaja vyuo vyote ambavyo vimenufaika na fedha za mradi

wa *HEET*. Chuo Kikuu cha *UDOM* ni kati ya vyuo ambavyo vimenufaika na fedha za mradi huu wa *HEET* na tayari fedha zimeshapelekwa kwa ajili ya ujenzi. Suala la maji *UDOM* kwa ujumla wake tunaendelea kulishughulikia kwa kushirikiana na Wizara husika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata utatuzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake tunaongeza jitihada kuhakikisha kwamba vyuo vyote ikiwa ni pamoja na *UDOM* tunamaliza ujenzi na ukarabati katika maeneo ambayo yalikuwa hayajakamilika ili wanafunzi wetu waweze kupata huduma nzuri ya elimu ya juu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza Swali dogo la nyongeza. Wakati ambapo wenzetu wanazungumzia kuboresha Vyuo Vikuu chakavu, Mkoa wa Njombe hauna Chuo Kikuu hata kimoja, mara kwa mara tumekuwa tukiomba na kwa kuwa Wilaya ya Makete tuko tayari kutoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu chochote kile ambacho unaweza kuona kinafaa;

Je, ni lini Serikali na ipi ahadi ya Serikali kwa wananchi wa Jimbo la Makete na Mkoa wa Njombe kwamba mtajenga Chuo Kikuu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hakuna Mkoa hapa nchini ambao hauna Tawi la Chuo Kikuu Huria, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Sanga kwamba Njombe siyo kati ya

Mikoa ambayo inayo au itanufaika sasa hivi kwa mradi wa *HEET* kwa kuwa na kampasi ya Chuo Kikuu kwa jitihada ambayo Serikali imefanya kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tumesambaza kampasi katika Mikoa kadhaa. Mipango iko mbioni ya mazungumzo na Mkoa wa Njombe kuhakikisha kwamba tunapeleka kampasi kule. Ningeomba *details* tuzitoe baada ya kukamilisha mikakati hii, lakini tunatambua umuhimu huo na tunajua kwamba kulikuwa na ahadi ilitolewa pale Njombe kwamba Njombe na yenyewe itapata kampasi ya Chuo Kikuu.

**MWENYEKITI:** Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Je, Serikali ina mpango gani kujenga au kuboresha vituo atamizi katika vyuo vyetu vikuu au taasisi za elimu ya juu, kwani hivi vituo ndio chachu ya kutengeneza viwanda hapa nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba vituo atamizi ni muhimu sana kwa ajili hasa ya kuunganisha juhudi za taaluma na maendeleo ya viwanda na maendeleo ya nyanja nyingine mbalimbali hapa nchini, nguvu kubwa tunazielekeza huko. Naamini hata baadhi ya Wabunge watakuwa wamepata fursa ya kuangalia wiki ya ubunifu ambayo inaendelea kwenye viwanja vya Jamhuri leo na juhudi ambazo tumezifanya na baadhi ya matokeo ambayo tayari tumeshazifanya. Kwa hiyo, tunalichukulia suala hili kwa umuhimu mkubwa na tutajitahidi sana kuongeza juhudi ya kuwa na vituo vyakutosha atamizi katika vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kesho tunazindua *Industrial Advisory Council* ya Sokoine ambayo vilevile ni kwa ajili ya kuunganisha juhudi za maendeleo ya viwanda na Chuo Kikuu cha Sokoine na vyuo vingine vyote hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, namuita Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, aweze kuuliza swali lake.

Na. 193

**Kupunguza msongamano wa malori mpaka wa Tunduma**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza: -

Je, lini mpaka wa Kasesya/Zombe utafanya kazi kwa ufanisi ili kupunguza msongamano wa malori katika mpaka wa Tunduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa mpaka wa Tunduma/Nakonde na mpaka wa Kasesya/Zombe ambayo inatumika kupitisha mizigo inayokwenda au kutoka Zambia. Aidha, wasafirishaji wana hiari ya kuchagua mpaka upi wautumie katika kusafirisha mizigo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wa Tunduma/Nakonde umekuwa ukitumiwa zaidi na wasafirishaji wanaosafirisha mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Zambia na DRC kwa kuwa ndiyo mpaka wenye umbali mfupi ukilinganishwa na mpaka wa Kasesya/Zombe. Kwa mfano, kutoka Dar es Salaam hadi Tunduma ni kilomita 922, kutoka Dar es Salaam kwenda Kasesya kupitia Tunduma na Laela ni kilometa 1,172; kutoka Dar es Salaam kwenda Kasesya kupitia Tunduma na Sumbawanga ni Kilometa 1,249; na kutoka Dar es Salaam kwenda Kasesya kupitia Dodoma,Tabora na Mpanda ni Kilometa 1,530. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo tunavyoongea mpaka ule unatumika lakini kwa kiasi kidogo sana na hili tatizo limetokana na upande wa pili wa Zambia ambapo wafanyakazi kama walivyo *TRA* Tanzania, ZRA wamekuwa hawaishi pale. Je, Serikali kwa kutumia ushirikiano uliopo na Zambia haioni kwamba ni wakati muafaka sasa wa kuongea na upande wa pili ili watumishi wa *ZRA* wawepo muda wote ili kusiwe na shida kwa wasafirishaji wa mizigo.

Swali la pili; ukitaka kwenda Congo ya Lubumbashi njia iliyokuwa rahisi kabisa ni kwa kupita Kasanga *Port* ambayo naomba niipongeze Serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana. Kazi ndogo ambayo imebaki ni upande wa pili kwa maana kupitia Mlilo kule na kwa wakati huu ambao ni rahisi kabisa kutumia *PPP*.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka kutangaza mradi huu ambao *economically* unaonekana kwamba *viable*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mpaka wetu wa Kasesya ambao una taasisi mbalimbali, kuna taasisi za Uhamiaji, Polisi, watu wa kilimo, *TRA,* kwa hiyo tunafanya kazi masaa 24, lakini upande wa wenzetu Zambia haufanyi kazi masaa 24, Serikali imechukua juhudi za kuwasiliana kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na hata mwaka jana tulifanya mikutano Tarehe 14 na 15 mwezi wa Kumi, kuhakikisha mpaka huu tunauhuisha na unafanya vizuri, waliahidi Serikali ya Zambia kwamba watafanya kama ambavyo tunafanya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekti, swali la pili kuhusu *PPP* hususan katika Bandari yetu ya Kasanga ambayo ni kweli imegharimu zaidi ya Bilioni 4.7 na Serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji pamoja na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tumekuwa tukifanya mikutano mbalimbali kuishirikisha sekta binafsi ili upande wa pili wa Congo waweze kutengeneza barabara ili bandari yetu ya Kasanga *Port* iwe na tija. Kwa hiyo, haya tunaendelea kuyafanya, tunataendelea pia kuwasiliana na wenzetu wa Serikali ya Congo ili kuhakikisha miundombinu upande wa kwao inafanya vizuri, ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mpaka wa Namanga ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu lakini kuna msongamano mkubwa wa malori. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha huduma katika mpaka huu wa Namanga ili basi kuleta tija? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na suala la mpaka wa Namanga kuwa na msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna mipaka kama Tunduma pamoja na Namanga ni mipaka ambayo ina msongamano mkubwa na ni kwa sababu ya bidhaa zinazoingia na kutoka kwenda nchi jirani. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba kwanza maeneo haya tumepanga utaratibu na *scanner* ambazo ziko katika maeneo hayo, kabla zilikuwa zinafanya masaa 12 na sasa tumeweka mpango wa zifanye kazi masaa 24 maana yake usiku na mchana ili magari ya kwenda Kenya na magari ya kuingia Tanzania kusiwe na msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tumeweka eneo maalum kwa ajili ya kuegesha magari hususan ya mizigo ili yasisongamane sana eneo lile la mpakani, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza kwa ufupi.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikumi idadi ya malori ni kubwa msongamano ule unasababisha hatari na usalama

wa maisha ya raia na mali zao. Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imetoa Milioni Mia Moja kwa ajili ya kutatua tatizo hilo la malori kwa kutenga eneo na kusaidia ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini *commitment* ya Serikali kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa katika kutatua tatizo la malori ambalo linasababishwa na mizani pale Mikumi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli eneo la Mikumi kuna msongamano wa malori mengi na Mheshimiwa Mbunge ninakupongeza kwa kufatilia jambo hili, alipolileta Serikalini tukawapa eneo ambalo ni la *TRC* kwamba waendelee kulitumia na tayari tulishatoa kibali hicho kama Serikali, kinachosubiriwa sasa ni wao kama Halmashauri kulifanyia hilo eneo ukarabati ili malori yaliyoko pale barabarani yahamie eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninakupongeza Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi zako hizo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Namuita Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 194

**Ujenzi wa Daraja Tanzania Bara - Zanzibar**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja litakalounganisha Tanzania Bara na Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi *Engineer* Kasekenya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo kuhusu ujenzi wa daraja litakalounganisha Tanzania Bara na Zanzibar yalishaanza kwa kuzihusisha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, sekta ya ujenzi kwa upande wa Tanzania Bara na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa upande wa Zanzibar, ambapo mnamo tarehe 11 Machi, 2023 kwa pamoja walikutana na Wawekezaji Kampuni ya *China Overseas Engineering Group Company* waliokuwa wameonesha nia ya kujenga daraja hilo. Yatokanayo na kikao hicho bado yanafanyiwa kazi kwa pande zote mbili Tanzania Bara na Zanzibar, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri sana ambayo ameyatoa sasa hivi. Nilikuwa na kitu kwanza kidogo kabla sijampa maswali yangu ya nyongeza mawili niliyonayo.

Nashukuru kwamba mwezi wa Ramadhani wenzetu wa jamii, wenzetu humu Bungeni walituheshimisha sana, wote walikuwa wanavaa mashungi na wanaume walikuwa wakivaa kanzu pamoja na koti, hilo kwanza niwashukuru sana na Mwenyezi Mungu awajaalie wazidi kutufuata sisi wenzetu Waislam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza, zipo nchi zimefanikiwa kujenga daraja za umbali mrefu, kwa nini tusipate uzoefu kutoka kwao?

Swali langu la pili, je, kwa nini usitumike mpango wa ubia na sekta binafsi *PPP* kwa ajili ya ujenzi huo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, upande wa Zanzibar na upande wa Tanzania Bara, wahusika tayari wameshakutana kwamba hili suala linazungumzika na lipo linachakatwa, bado yatokanayo na hilo hayajapatikana ikiwa ni pamoja na kulifanyia kazi lile alilosema Mheshimiwa Mbunge kupata uzoefu kutoka sehemu mbalimbali ambazo wenzetu wameshajenga madaraja mengine marefu kama haya, ndiyo maana tunasema yatokanayo na hayo bado lakini suala hilo lipo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili kuhusu *PPP*, ni kweli kabisa kwamba siyo mpango kwa maana ya Serikali ichukue fedha zake ijenge na hata hao walioonesha nia ni sekta binafsi. Kwa hiyo, tunaamini daraja hili kama litajengwa, litajengwa kwa mtindo wa *PPP* kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tuulize maswali kwa ufupi ili tutoe fursa kwa walio wengi. Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Denmark kuna daraja linalounganisha Odense na Sealand na lilichukua muda mfupi sana kujengwa.

Je, Serikali inatueleza nini katika kupeleka mtu kama mwenye swali lake Mwantumu Dau Haji kwenda kulishuhudia ili tufupishe hayo maneno ya mazungumzo yalifanyika, yalifanyika kwa muda mrefu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo yalifanyika Mwezi Machi mwaka huu na huu ni mwezi Aprili. Kwa hiyo, kwa mradi mkubwa kama huu na daraja ambalo linaunganisha linategemewa liunganishe Bara na Zanzibar yako mambo mengi sana ambayo yatafanyika. Moja ya eneo ambalo tunafahamu ni Denmark lakini hata China wana madaraja mengi marefu. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla Serikali haijaanza kutekeleza lazima watajiridhisha kwa mambo mengi sana ikiwa ni pamoja na teknolojia mbalimbali ambazo zimetumika katika nchi nyingine ambazo wana madaraja marefu kama haya. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea ninamuita Mheshimiwa Jerry Silaa aulize swali lake.

Na. 195

**Serikali kuuza Nyumba za Kota za Ukonga**

**MHE. JUDITH S. KAPINGA K.n.y. MHE. JERRY W. SILAA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni ni busara kuuza nyumba kwa Wapangaji wa kota za Ukonga kwa kuwa wameishi miaka mingi bila kufanyiwa ukarabati?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka mpango mahsusi wa kukarabati na kuendeleza maeneo yote ya kota nchini ambazo ni nyumba zilizorejeshwa *TBA* kutoka TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka huu wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* imeanza kukarabati nyumba za kota za Ukonga ambapo kwa sasa *TBA* imekarabati maghorofa mawili yenye uwezo wa kubeba familia Nane. Ukarabati umehusisha maeneo ya paa, dari, mfumo wa umeme, mfumo wa majisafi na majitaka na upakaji wa rangi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Judith Kapinga swali la nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Jerry Silaa.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mzauri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuanza ukarabati wa majengo haya ila kwa kuwa yamekaa muda mrefu, nataka kufahamu kama mwaka huu wa fedha unaokuja fedha zimetengwa kwa ajili ya kumaliza ukarabati

kwa ajili ya majengo yote yaliyobakia na ukarabati utategemea kumalizika kwa muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ni kwamba Serikali haioni umuhimu wa kujenga mradi kama ule wa Magomeni, Ukonga ili wananchi waweze kupata nyumba na majengo mengine waweze kukodiwa watumishi ikiwemo watumishi wa Magereza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge yote kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo ya Ukonga kota ni majengo yale madogo na ya zamani na mpango wa Serikali kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi maeneo yote ambayo yalikuwa na majengo yale ya zamani yaboreshwe ama yabadilishwe na Ukonga ikiwa ni moja ya eneo ambalo mwezi huu wataalam wamekwenda ku–*assess* na kupata ukubwa wa eneo halisi ili paweze kubadilishwa na kujenga majengo makubwa ya ghorofa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mpango mzima ni kujenga majengo yanayokwenda juu badala ya kuejenga haya majengo madogo. Kwa hiyo, Ukonga kota ni sehemu mojawapo kama Temeke, Ilala kota, Kinondoni, Ghana Mwanza na hata Arusha. Kwa hiyo, maeneo yote haya tunafanya mabadiliko ya kujenga ghorofa kama ambavyo tumejenga Magomeni kota na tunavyoendelea Temeke, ahsante.

**MWNEYEKITI:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafsi ya kuuliza swali la nyongeza.

Manispaa ya Moshi tunazo Kata ambazo ziko katika maeneo ya Majengo Kiusa na kota hizo zimechoka sana na ni za miaka mingi sana. Wako wapangaji ambao wameishi pale mpaka sasa hivi wana wajukuu na vitukuu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha kota hizo au hata kama kuna uwezekano wa kuweza kuwauzia? Aahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu ssali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la pili kwenye majibu yangu ya nyongeza kwa Mheshimiwa Kapinga, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, awamu hii ya sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan; moja, ameshatoa maelekezo kwamba, pale ambapo mnaweza mkafanya na sekta binafsi, basi kuna haja ya kufanya hivyo. *TBA* kwa jinsi muundo wake ulivyokuwa, sasa hivi iko kwenye kubadilishwa ili iweze kufanya na *private sector* ili maeneo yote yale ambayo yalikuwa na *quarters* zilizochoka tuangalie uwezekano wa kuongea na wenzetu wa sekta binafsi ili kuharakisha kujenga majengo kwa ajili ya kutoa huduma kwa watumishi na viongozi wa Tanzania hii, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tarimba, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwa kuwa Serikali imekubali

maombi ya wananchi na wakazi wa *Magomeni Quarter,* familia 644 kuwauzia nyumba hizo na kuwapunguzia bei ya ununuzi na vilevile kuwaongezea muda wa kulipa kutoka miaka 15 hadi 30. Swali langu: Je, Serikali iko tayari kupokea shukrani zangu za dhati pamoja na wananchi wa *Magomeni Quarter* kwa uamuzi wa Serikali kuwauzia nyumba hizo na kuboresha familia zao, kitendo ambacho kinaonekana ni kuboresha maisha ya wananchi wa Tanzania? Shukrani hizi zimwendee Mheshimiwa Rais na Mtendaji Mkuu wa *TBA* Bwana Kondoro. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tarimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani alizotoa Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba nizipokee shukrani hizo ambapo ni kazi kubwa imefanyika, na kweli amejali wananchi waliokuwa wanaishi hapo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Namwita Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 196

**Kuongezeka bei ya zao la chai kwa wakulima wadogo**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kusaidia kuongezeka kwa bei ya zao la chai kwa wakulima nchini?

**MWENYEKITI:** Wizara ya Kilimo, Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bei ya zao la chai hutegemea mwenendo wa Soko la Dunia, soko la ndani na ubora wa chai sokoni. Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali kuhakikisha uwepo wa mazingira bora yanayoleta ushindani ili kuchochea bei ya chai. Katika hatua ya awali, kwa mwaka 2023 bei ya chai imeongezeka kutoka shilingi 312 hadi shilingi 366 kwa kilo. Aidha, mikakati mingine ya kupandisha bei ni kuongeza uzalishaji wa miche bora ya chai, kuendelea kuhamasisha matumizi ya chai nchini, kuanzisha mnada wa chai, kutoa ruzuku ya mbolea na miche bora ya chai ili kuongeza tija na uzalishaji na kuandaa mwongozo wa ubora wa majani mabichi ya chai na kuanzisha kiwanda cha kusindika chai maalumu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Bei hii inayosemwa imepanda sasa ilikaa zaidi ya miaka mitano bila kupanda, wakati kwenye Soko la Dunia bei ilikuwa ikipanda ukiacha kile kipindi cha *Covid-19:* Ni upi mkakati wa Serikali

sasa angalau kufanya mapitio kila mwaka ili kuhakikisha kwamba tunawasaidia wakulima wa nchi hii wakiwemo wakulima wa Tarafa ya Bungu kule Korogwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Moja ya njia ya kusaidia kupanda kwa bei ya chai ni kuwa na mnada wa kwetu Tanzania. Mheshimiwa Waziri, Serikali ilituahidi tangu mwaka 2019, ukiwa Naibu Waziri, kuanzisha mnada wa chai Tanzania, lakini mpaka leo mnada huo haujaanzishwa: Ni nini kauli ya Serikali juu ya kuanzisha mnada wa chai ndani ya nchi yetu ya Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa kilimo, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei iliyodumu kwa kipindi cha miaka mitano ni bei ya shilingi 312. Kikao cha wadau kilichofanyika mwanzoni mwa mwaka huu ndicho tulichobadilisha bei na kuipeleka kuwa shilingi 366 kwa maana ya bei ya chini ya chai. Sasa hivi katika baadhi ya maeneo, hasa maeneo ya Nyanda za Juu Kusini wakulima wanauza chai *grade one* mpaka shilingi 420. Kwa hiyo, mabadiliko ya bei yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo tunalifanya kwenye eneo la bei, Serikali inapitia mfumo mzima wa uchakataji na *importation* ya chai kutoka nje ili kuvifanya viwanda vya ndani na kuongeza *consumption* ya matumizi ya chai ya ndani na kuvipunguzia baadhi ya tozo mbalimbali. Mtaona kwenye bajeti itakapokuja Wizara ya Fedha, mtaona mabadiliko katika eneo hilo ili kuvifanya viwanda vya *blending* vya ndani viweze kutumia zaidi chai ya ndani na kupunguza *importation* ya chai kutoka nje na kuvitengenezea soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mnada. Nataka nilihakikishie Bunge lako, ni kweli, dhamira ya Serikali toka mwaka 2019 ilikuwa ni kuanzisha mnada, lakini nilihakikishie Bunge lako kwa uwezo wa Mungu, mwaka huu mnada utaanza. Tumeshakamilisha masulala ya miundombinu, tumeshakamilisha eneo la maabara, tumeshakamilisha mwongozo, na sasa hivi tuko hatua za mwisho kwa ajili ya kusajili ma-*broker* wa Kimataifa ambao watashiriki kwenye *trading* kwa sababu, uuzaji wa chai una utaratibu wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza:-

Je, Serikali inawasaidiaje kwa dharura wananchi wa Kata ya Ruaha Mbuyuni, Wilaya ya Kilolo kwa kuwa wameingia taharuki kubwa sana; mfereji umeacha njia, umehama, *intake* imeachwa peke yake, maji hayapo kabisa: Wananchi hawali, hawalali, maji hayapo kabisa na mashamba yamekauka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli eneo la Ruaha Mbuyuni mfereji umehama na mto umehama. Kwa hiyo, hatua ambayo Serikali inachukuwa sasa hivi, timu ya Wataalam wa Wizara ya Kilimo tayari iko Mkoani Iringa kwa ajili ya kuliangalia hilo eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la msingi ambalo nilitaka nilitaarifu Bunge lako na wakulima wa eneo la Ruaha

Mbuyuni, tatizo la Ruaha Mbuyuni halitofautiani na tatizo lililokuwepo kwenye maeneo ya Mlenge na Mkombozi. Kila mwaka mvua zikiwa nyingi mto huacha njia. Kwa hiyo, hatua tuliyoamua kama Wizara, tunaenda kulifanyia *detailed design* na kutangaza baadaye kwa mwaka ujao wa fedha ili ijengwe *comprehensive scheme* katika lile eneo na tuondokane na hili tatizo la kila mwaka kwenda kufanya *repair* katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana; je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kudhibiti bei ya kahawa, maana imekuwa ikipanda na kushuka kila mara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, na siyo tu bei ya kahawa, ni mazao yote bei inapanda na kushuka. Serikali haiwezi kudhibiti bei, bali Serikali jukumu letu la msingi ni kuongeza tija ili kupunguza gharama za uzalishaji ili wakulima waweze kupata faida baada ya gharama zao kupungua. Kwa hiyo, tunachukua hatua mbalimbali za kupunguza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii wakulima wa kahawa wametumia *almost* asilimia 7.5 ya mbolea yote ya ruzuku iliyosambazwa. Kwa hiyo, ile itawaongezea tija. Mwelekeo wa Serikali ni kuongeza tija kwa kuwapa miche bora ili kuwapunguzia gharama na kuwaongezea uzalishaji waweze kuwa *competitive*. Hatua ya pili ambayo tunataka kuweka

kwenye zao la kahawa ni uhamasishaji wa matumizi ya kahawa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi, tuna-*export* kahawa kwa wastani wa dola nne, lakini tuna *import made coffee* kwa wastani wa dola 20. Kwa hiyo, Serikali sasa tunaanza hatua, mtaona kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo, mfano kwenye maeneo ya Kagera tunaanza uwekezaji kwenye Kiwanda cha *TANICA* ili tuongeze *blending* na matumizi ya kahawa iliyokuwa *processed* ndani na kuongeza unywaji wa kahawa ndani ya nchi na kuwaongezea wakulima soko la uhakika na uhakika wa bei.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hali ya hewa ya Tarime na ardhi vinaruhusu kilimo cha zao la chai. Miaka ya nyuma wananchi walikuwa wakilima chai, lakini waliacha kutokana na kutokuwepo na masoko na bei kuwa chini. Sasa kwa mikakati ambayo Serikali imeainisha hapa, nataka kujua, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inahamasisha na kufufua zai la chai kwa Wilaya ya Tarime ili kuweza kukuza uchumi wa wana Tarime? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Tarime ilikuwa ni eneo mojawapo la uzalishaji wa chai na wananchi waliacha. Siyo Tarime tu, hata Mkoa wa Kagera na wenyewe ulikuwa ni eneo mojawapo la uzalishaji wa chai, na Serikali ilibinafsisha baadhi ya maeneo ambayo wawekezaji waliopewa maeneo

yale walishindwa kuyaendeleza. Kwa hiyo, kama Serikali sasa hivi, kwa mfano, maeneo ya Kagera tumeanza maongezi na mwekezaji aliyeshindwa ili tuweze ku-*take over* kile kiwanda kupitia ushirika na Serikali kuweza ku-*bail out* tuweze kufufua chai eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutafanya tathmini *economically,* kuangalia kama tuendelee na jitihada tunazozifanya kwenye mazao ya chakula na mazao ya kahawa kwenye eneo la Tarime, ama tulilete zao la chai na litatuathiri namna gani? Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mbunge tutafanya tathmini *and then* tutakuwa na majibu ya uhakika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mchafu.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nilitaka kujua ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha zao la korosho linarudi katika bei ya miaka ya nyuma ya shilingi 4,000 na kuondokana na bei ya sasa ya kilo shilingi 1,600? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee ya mazao ya kilimo kuwa na uhakika wa bei nzuri kwa mkulima na kuwa na uhakika wa soko ni njia mbili. Moja, kuongeza tija, kupunguza gharama za uzalishaji.

Pili, ni kuongeza thamani katika mazao kwa maana ya *value addition* na kuacha kuuza mazao yetu ghafi nje kwa sababu tunauza na ajira zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie watu wa korosho, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, 2025/2026 hatuta-

*export* korosho *raw,* tutabangua zote ndani ya nchi hii. Kuanzia mwaka ujao wa fedha tutatenga kiasi cha Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuanza safari ya ubanguaji ndani ya nchi yetu kwa kuwasaidia sekta binafsi ya Kitanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Moja kati ya sababu zinazowafanya vijana wa Nyanda za Juu Kusini, hususan Mkoa wa Njombe kutokupenda kulima zao hili la chai ni pamoja na bei ya chini ya zao la chai.

Je, ninyi kama Serikali mmejipanga vipi kuhakikisha kwamba mnawa-*motivate* vijana waweze kushiriki katika kilimo hiki cha chai ikiwa ni pamoja na kuanzisha *program* za *out growers* kwenye mashamba ya chai? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli zao la chai siyo vijana peke yake, baadhi ya maeneo wakulima wameanza kuling’oa. Tunapitia upya mfumo mzima wa chai. Ni sahihi kwamba, wakati bei ya chai inapanda ama pale ambapo tunakuwa tegemezi, mfumo wetu wa masoko kwa wenzetu walioko nje ya nchi, maana yake tunakuwa *vulnerable* siku zote. Kwa hiyo, kama Serikali kama hatua nilizozisema za mwanzo kuanzisha mnada, kuongeza *value addition* ndani ya nchi, kupunguza *importation* ya chai kutoka nje, *automatically* jambo hili litasaidia wakulima kuwa na uhakika wa soko na bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni safari, nawaomba wakulima wa chai nchini, Serikali imeanza kuchukua hizi hatua. Nawaomba wasing'oe chai na wale wote waliouziwa viwanda, hasa nyanda za Kaskazini na baadhi ya maeneo ya Nyanda za Juu, tumewaandikia barua wafufue mashamba na kuviendesha vile viwanda. Kama hawawezi tutafute watu wengine watakaoweza kuwekeza katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa uzalishaji wa tumbaku chini ya uongozi wako mzuri katika Wizara hii umeongezeka sana maradufu mwaka huu; na kwa kuwa, sasa hivi ndiyo tunaenda kwenye soko na uzalishaji ni mkubwa: Serikali imejipangaje kuisaidia Bodi ya Tumbaku kupeleka *classifiers* kwa wakati kufanya kazi hiyo ili soko lisichukue muda mrefu sana, wakulima waweze kuuza kwa wakati na wapate hela yao kwa wakati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunatumia mfumo wa *crop financing.* Bodi ya Tumbaku ilikuwa inategemea kampuni ziwape magari na mafuta ili kwenda kwenye masoko. Tumetengeneza utaratibu ambao kama bodi, itapata kipato kutokana na zao lenyewe bila kumuumiza mkulima, lakini wakati huo huo kama Wizara tumeanza utaratibu sasa hivi wa kuwatafutia magari Bodi ya Tumbaku ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kufanya usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tu wakulima wa tumbaku na kuwaomba kwa kuwa tumeanza minada sasa hivi, na minada hii imekuwa mizuri, tumbaku imefika mpaka Dola tatu safari hii kwenye minada na ushindani umekuwa wa wazi, nawaomba tu wakulima wahakikishe wanasimamia suala la ubora na wasichanganye kwenye mitumba takataka kwa sababu zitaenda kutuangushia zao letu. Mwaka huu tunatarajia tumbaku itafika tani 120,000 kutoka tani 60,000.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na kwamba zao la korosho limekuwa likiteremka mwaka hadi mwaka, lakini uzalishaji katika Wilaya ya Nanyumbu umekuwa ukiongezeka sana: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kufikiria kujenga kiwanda ndani ya Wilaya ya Nanyumbu ili kuhakikisha kwamba korosho zote za Msumbiji na zile za Wilaya ya Nanyumbu zinabanguliwa pale pale Wilayani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kumwahidi Mbunge mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba tutaenda kujenga kiwanda Nanyumbu. Bali, *approach* ya ubanguaji tunayoendanayo ni *private sector driven,* na tunaenda kuisaidia sekta binafsi ya kwetu ya Watanzania. Tutaangalia *economic reasons* za wapi kiwanda kikae. Kama kutakuwa kuna sababu ya kuweka kiwanda Nanyumbu, tutafanya hivyo, wala hatutasita, lakini kwa hatua ya kwanza, *Korosho Processing Center* tutakayoanza kuijenga, tutaijenga katika

Halmashauri ya Nanyamba na Serikali imeshaanza kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama Halmashauri yake inaweza kutenga eneo ambalo tutaanza kuliwekea miundombinu kwa ajili ya baadaye, tuanze huo mchakato sasa hivi, lakini sekta binafsi ndiyo itakayoamua ni wapi inataka kiwanda chake kiwepo, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Serikali imekuwa na utaratibu wa kuagiza mafuta ya kula nchini, ambayo yameua kabisa soko la mafuta ya alizeti ambayo Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara walihamasisha sana ulimaji wa alizeti. Sasa ni lini Serikali itaacha utaratibu huu ili kulinda bei ya mafuta na alizeti hapa nchini? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli msimu huu kidogo bei ya alizeti imeshuka kwa mkulima. Tunafahamu kwamba mkulima akiuza alizeti chini ya shilingi 900 mpaka ikafika shilingi 700, maana yake anapata hasara. Kama Wizara, tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya fedha kupitia upya maamuzi tuliyoyafanya mwaka 2022 ya ku-*reduce tax* ya *import* ya *refined palm oil* mpaka kufika asilimia 25, kuiangalia *impact* yake na athari yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka niliambie Bunge lako tukufu, *import substitution strategy* tuliyofanya kama Serikali na ninyi Waheshimiwa Wabunge ya kusaidia kuwekeza kwenye alizeti, ukiangalia *report* ya *BoT* ya mwezi huu wa Machi iliyotoka, inaonesha kwa kiwango gani hatua

tulizochukua zimepunguza *importation* ya mafuta ya kula kwa wakati huu wa uzalishaji wa mafuta ya alizeti yameongezeka. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hatutaruhusu zao la alizeti kufa kwa sababu Serikali inachukua hatua mbalimbali na tutapitia changamoto hizi zilizojitokeza kwa mwaka huu wa fedha ili kuweza kumlinda mkulima na kuhakikisha nchi inajitosheleza mafuta.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa majibu yako. Sasa tunakwenda Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Namwita Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mbunge wa Gando, aweze kuuliza swali lake.

Na. 197

**Kuandaa filamu za historia ya nchi**

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI K.n.y. MHE. SALIM MUSSA OMAR** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuandaa Filamu zenye kueleza Historia ya Nchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania kwa kushirikiana na wadau imewezesha uzalishaji wa filamu zinazohifadhi na kuelezea historia ya nchi yetu.

Mfano Makala ya Uzalendo iliyoandaliwa na Bodi ya Filamu mwaka 2021 kupitia muandaaji filamu Bwana Adam Juma inaelezea historia ya viongozi wetu na ushujaa wao katika kuipambania nchi. Pia, mwaka 2022 Bodi kupitia Studio za Wanene iliandaa makala inayotangaza mandhari ya kupiga picha za filamu na kuelezea maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Bodi ya Filamu inaendelea na maandalizi ya filamu inayohusu maisha ya Chifu Mkwawa iitwayo Mkwavinyika. Pia kwa kushirikiana na wadau wa filamu, Bodi inaratibu mpango mahsusi wa uandaaji wa filamu zinazohusu maisha ya viongozi wetu, ambapo itaanza na filamu ya Bibi Titi Mohammed, ikifuatiwa na ya Chifu Kingalu, Mtemi Mirambo pamoja na Mwalimu Nyerere.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassim Hassan Haji kwa niaba ya muuliza swali.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa watu wengi ambao wameiona historia ya Tanzania na Zanzibar wameandika vitabu katika historia hii.

Je, ni lini vitabu vile vitatafsiriwa, Serikali itachukua maamuzi ya kutengeneza filamu ya vitabu vile ili kizazi kinachokuja kiweze kujivunia na kuona uhalisia wa historia ya Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa lengo la Serikali siyo tu kuhifadhi historia ya nchi na mashujaa wetu kwenye filamu, lakini ni kuhifadhi katika kiwango na hadhi inayotazamika kwenye majukwaa ya Kitaifa na ya kimataifa. Kwa hivyo Serikali kwa sasa inafanya juhudi kubwa kuhakikisha uwekezaji mkubwa unaongezwa kwenye tasnia ya filamu nchini kuhakikisha hilo linatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kudhibitisha hilo, ni juma lililopita tu Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, mama yangu, Mheshimiwa Balozi Pindi Hazara Chana, alihudhuria utiaji saini mkataba wa makubaliano kati ya Bodi ya Filamu Tanzania na Taasisi ya Mashirikiano ya Kimataifa ya Korea Kusini *(BFIC)*, makubaliano ambayo pamoja na mambo mengine yanakwenda kuona uwekezaji mkubwa ukiongezeka kwenye tasnia ya filamu nchini ambapo filamu ambazo unazizungumzia Mheshimiwa zitakwenda kufanywa kwenye kiwango na hadhi inayotazamika kwenye majukwaa ya Kitaifa na ya kimataifa, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii inaangalia sana suala la maslahi ya wasanii na michezo kwa ujumla; ni lini Serikali itapitia upya makato inayokata katika mambo ya michezo? Kwa mfano juzi Simba wamepata milioni 180 katika 450; ni lini itapitia makato haya ambayo ni kandamizi?

**MWENYEKITI:** Swali lako halijasikika vizuri Mheshimiwa, unaweza kulirudia kwa ufupi? Na Mheshimiwa Naibu Waziri unayo hiari ya kulijibu.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itapitia upya makato inayokata; kwa mfano juzi Simba imepata milioni 450 kwenye mchezo lakini inaambulia milioni 180, makato mengi ambayo hayaeleweki; lini Serikali itapitia upya makato ili kuziokoa timu zetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na swali la Mheshimiwa Mbunge Isack kuwa liko pembeni kabisa ya swali la msingi, lakini kimsingi tunaangalia utaratibu ambao utawezesha vilabu vyetu viweze kuendelea kufaidika zaidi. Lakini kuna gharama kubwa za uendeshaji wa michezo inayotajwa na taasisi zetu zinaingia gharama kubwa ambayo inatoka mifukoni kwao kuweza kuifanya michezo hii ifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo pamoja na lengo letu la kuhakikisha timu zetu zinafaidika, lakini kuna gharama kubwa ambazo taasisi zetu zitashindwa kujiendesha kama tutazizuia moja kwa moja kukata makato yale, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis, unaweza kulileta swali hilo kama swali la msingi ili Serikali ichakate na kuona vilabu hivi vinanufaika kwa kiwango gani kwa sababu pia ni jukumu la Serikali kuwezesha taasisi zetu za Serikali.

Mheshimiwa Esther Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itawapa vitambulisho machifu wetu ili kuweza kuwatambua kwamba ni machifu wa nchi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kuhakikisha tunawekeza nguvu nyingi kuhakikisha utamaduni wetu haupotei. Na miongoni mwa mambo ambayo yanafanyika ni kutambua uwepo wa machifu wetu. Na hilo limefanywa hata na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukaa kikao na machifu mbalimbali – siyo mara moja – na kuwatambua kwenye masuala mbalimbali ya sherehe za Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, machifu bado wanatambulika na Serikali, lakini juhudi mbalimbali bado zinaendelea kufanyika ili kuhakikisha kutambulika kwao kunafahamika Kitaifa na kimataifa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika dhana ileile ya kuendelea kutangaza utalii wa Taifa letu, je, Serikali haioni ni wakati sahihi wa kutengeneza filamu maalum ya kueleza historia ya Ukoo wa Simba wa *Bob Junior* na namna ambavyo ilisisimua Taifa na dunia kuhusu kifo cha *Bob Junior*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazo zuri ambalo amelitoa, na sisi kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii tunaomba tulichukue na tutalifanyia kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma kwa majibu yako, unaweza kwenda kuketi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa *session* yetu ya maswali na majibu kutoka Serikalini, tunawashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu. Lakini hapa tunayo matangazo matatu.

Tangazo la kwanza limetoka kwa Katibu wa Bunge, anasema; naomba uwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wanawake na wanaume kuwa leo tarehe 28 Aprili, 2023 kutakuwa na sherehe ya Usiku wa Mwanamke wa Bunge itakayofanyika katika Viwanja vya Bunge mara baada ya kuahirisha Bunge jioni. Waheshimiwa Wabunge wote wanaalikwa kuhudhuria sherehe hiyo. Kwa hiyo, mnasisitizwa na mnakumbushwa Waheshimiwa Wabunge kuweza kushiriki kwenye shughuli hii muhimu kwa akinamama na sisi wenyewe. *(Makofi)*

Tangazo la pili pia limetoka kwa Katibu wa Bunge, anasema; naomba uwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba leo, Siku ya Ijumaa, tarehe 28 Aprili, 2023 kutakuwa na semina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji nchini mara baada ya kusitisha kikao cha Bunge saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa. Semina hiyo imeandaliwa na Wizara ya Maji, hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kuhudhuria semina hii muhimu. Tunaamini hakuna atakayekosekana kwenye semina hii.

La tatu ni wageni waliopo Bungeni leo asubuhi; kundi la kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, na hapa nitaanza na wageni 13 wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni Mabalozi wa Madini wa Chama cha Wachimba Madini Wanawake *(TOWAMA)* kutoka Mikoa mbalimbali Tanzania; karibuni sana mabalozi. *(Makofi)*

Kundi la pili ni wageni 45 wa Mheshimiwa Joseph Kakunda (Mb), ambao ni wanafunzi na walimu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe kutoka Mkoa wa Morogoro; karibuni sana wageni wetu kutoka Mzumbe, Morogoro. Na sisi wengine tulisoma huko pia. *(Makofi)*

Tatu ni wageni watatu wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka (Mb), ambao ni kaka zake kutoka Mkoa wa Bukoba, karibuni sana. *(Makofi)*

Nne ni wageni 24 wa Mheshimiwa Zaytun Swai (Mb), ambao ni Wanakwaya wa Mt. Don Bosco kutoka Jijini Arusha wakiongozwa na Rais wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki na mlezi wa kwaya hiyo, Jaji Nestor Kayobera. Wanakwaya na Rais wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki, Jaji Nestor Kayobera aliyewaongoza, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jafari Chege (Mb), ambao ni wapiga kura wake kutoka Rorya, Mkoa wa Mara, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Hamisi Taletale (Mb), ambao ni Viongozi wa Taasisi ya Hijja na Umrah ya *IBN Batuta Tours Limited* kutoka Mkoa wa Morogoro, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 100 wa Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo (Mb), ambao ni Viongozi wa CCM kutoka Jiji la Arusha. Sasa hawa nitawatambulisha kwa makundi: -

Wako Wajumbe wa Kamati ya Siasa; ahsante. *(Makofi)*

Wako Wenyeviti wa CCM wa Kata; *(Makofi)*

Wako Makatibu wa CCM wa Kata; *(Makofi)*

Lakini pia Mheshimiwa Mrisho Gambo ameita na Wenezi wa CCM wa Kata. *(Makofi)*

Wako na watu kutoka Soko la Utalii la *Masai Market; (Makofi)*

Pia wapo viongozi wa Bajaji; *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge hakuishia hapo, aliwaita na Viongozi wa Soko la Krokon. Haya, tunawashukuru na karibuni sana viongozi na wadau mbalimbali kutoka Jiji la Arusha. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Monni ambaye ni mfanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Riyaz Khan, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Daniel Awack ambao ni wapiga kura wake kutoka Karatu, Mkoani Arusha, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Awack. *(Makofi)*

Tuna wageni 30 wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ambao ni wanamichezo wa *FIFA Football Club* kutoka Mkoani Iringa, karibuni sana. Najua inawezekana na wa Mufindi wako hapo hapo. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Suma Fyandomo ambao ni vijana wake kutoka Mkoa wa Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Aidha, tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Hapa tunao wageni 53 na walimu nane kutoka Shule ya *Peace Academy* ya Jijini Arusha; karibuni sana wageni kutoka *Peace Academy* kuja kujifunza shughuli za uendeshaji wa Bunge letu. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 23 wa Shule ya Sekondari Sumaye ya Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Karibuni sana nyote wageni wetu mliofika leo kwenye Bunge letu. Kama mnavyoona shughuli zinaendelea na Spika wetu, ambaye ndio kiongozi wetu mkuu wa Mhimili yuko pale. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na majadiliano ya Wizara ya Madini, na hapa ninao wachangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, wakati huo Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo wakijiandaa.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kabla sijaenda kwenye hoja zangu, niungane na Waheshimiwa Wabunge ambao wanampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Biteko, pamoja na Naibu Waziri, kwa kufanya kazi vizuri sana katika Wizara hii na kuijengea

heshima kubwa sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huohuo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ambaye amemuamini Waziri huyu katika sekta hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo mawili ambayo ninatamani nichangie kidogo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza linahusu kutumia matokeo ya tafiti mbalimbali za madini ambazo zimefanyika hapa nchini. Zipo tafiti nyingi sana zimefanyika na kubaini uwepo wa madini maeneo mbalimbali. Moja katika maeneo hayo ni Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, Mkoa wa Ruvuma. Imechukua takribani miaka zaidi ya 20 kuanza kutumia baadhi ya tafiti ambazo zilifanyika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Halmashauri ya Madaba miaka 20 baadae baada ya kugundua uwepo wa madini aina ya makaa ya mawe ndipo tumeanza kutumia yale matokeo ya tafiti. Kimsingi tumechelewa sana, leo pengine Madaba tungekuwa mbali sana kiuchumi. Tumeanza kutumia matokeo yale leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri arudi kwenye makabati yake akaangalie matokeo ya tafiti za madini zinazohusu Madaba. Ndani ya Kijiji cha Ifinga katika Halmashauri ya Madaba kuna uwepo wa madini yenye thamani kubwa sana. Naomba kama itakupendeza Mheshimiwa Waziri, na ukiridhika, wasiliana na Dkt. Dalali Kafumu ambaye alishiriki kwenye utafiti huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utafiti ambao utaleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi kwenye Halmashauri ya

Madaba na kwa Taifa katika ujumla wake. Nikuombe sana fanya jitihada za pekee. Binafsi naendelea kufuatilia lakini naomba unisaidie kwenye eneo hilo kwa sababu Wanamadaba wanasubiri kuanza kunufaika na uwepo wa madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba uridhie turejee kwenye mradi muhimu sana kwa maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Njombe katika ujumla wake. Lakini manufaa haya hayaishii Njombe na Ruvuma pekee, manufaa ya mradi huu yanakwenda kugusa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi sana, zaidi ya miaka 30, nenda kwenye *Hansard* za Bunge hili utakuta tunazungumza mradi wa Liganga na Mchuchuma. Tunaposema Liganga – naomba Watanzania waelewe na Waheshimiwa Wabunge tuelewe na tuunganishe nguvu – tunaposema Liganga hii ni *deposit* ya chuma, chuma inayoweza kujenga reli, inayoweza kuwa malighafi ya kutengeneza magari, inayoweza kuwa malighafi ya kutengeneza pikipiki na baiskeli, ambayo inaweza kuwa malighafi ya kutengenezea nondo na kujengea majengo ya aina yoyote, ambayo inaweza kuwa malighafi ya bati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea utajiri huu mkubwa ambao upo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa inayopakana na Madaba ndani ya Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea huu mradi wa Liganga na Mchuchuma, Mchuchuma tunazungumzia makaa ya mawe, Liganga tunazungumzia chuma. Makaa ya mawe ya Mchuchuma yana uwezo wa kuzalisha umeme megawati 600. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyosema megawati 600 Watanzania wanielewe, hii ni zaidi ya nusu ya umeme wote ambao Tanzania ilikuwa nao miaka mitano iliyopita. Kwa hiyo, siyo umeme mdogo, tusiuchukulie mradi huu kitoto kitoto, hebu tuupe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa maana ya *multiplayer effect* mradi huu mimi ningesema, mradi huu unafuatia kwa umuhimu ukiondoa mradi wa maji wa Bwawa la maji la Mwalimu Nyerere. Ukiondoa mradi wa maji wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere mradi unaofuata kwa *multiplayer effect* na kwa umuhimu wa Tanzania na kwa uchumi wake ni mradi wa liganga na mchuchuma. Mradi huu ulikuwa unaambatana na ujenzi wa reli ya kusini, reli ambayo ingeleta maendeleo makubwa sana kwa nchi hii. Lakini tunapozungumzia mradi huu tunazungumza pia barabara ya lami ya Mkiu-Madaba ambayo ingetumika kusafirisha malighafi ya chuma na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti,hii miradi yote hatujaipata kwa sababu hatujaamua kuchimba hii chuma. Tumewanyima wana-Ruvuma haki ya maendeleo, tumewanyima haki wana-Njombe kupata maendeleo. Tumewakatalia fursa za ajira watoto wa Madaba, Njombe, Peramiho na Songea Mjini kwa kukataa kujenga mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninamwamini sana Mheshimiwa Dotto, ni mtu wa viwango, amefanya mapinduzi makubwa sana kwenye sekta ya madini lakini anaacha lile jiwe la chuma likae pale kwa miaka mingapi? Nani atakuja kulichimba lile jiwe? Watanzania watasubiri ajira mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema *mutliplayer* nyingi sana, sijasema kuhusu aakina mama, akina mama ntilie ambao wangepata ajira kwa kuuza chakula kwenye migodi ya chuma ile. Sijamwambia kuhusu idadi ya vijana ambao wangeajiriwa kwenye miradi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya sita ilipoingia madarakani kulioneshwa dalili ya kwenda kuanza kuchimba lile jiwe. Na mimi niseme, Watanzani nchi nzima tujue tumekalia utajiri mkubwa sana pale Ludewa; na kama nchi hii haipigi hatua za kutosha ni kwa sababu hatujaamua kutumia malighafi ambazo tumepewa na Mwenyezi Mungu pale Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana uendelee kukazia Serikali na Mheshimiwa Doctor Dotto uko hapa naomba jitahidi kabla Awamu ya Sita hii haijamaliza kipindi chake cha uongozi tuwe tumeshachimba jiwe la chuma la liganga? Tuwe tumeshatoa ajira kwa wana-Ruvuma na Watanzania, tuwe tumeshazalisha malighafi kwa ajili ya baiskeli, magari na vifaa vingine vya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daktari Joseph Kizito Mhagama, ahsante sana.

Wakati na tangaza nilisema ni wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari ya Sumaye, naomba isomeke ni watumishi 23 wa shule ya Sekondari ya Sumaye Mkoani Morogoro. Wapo hee? Hawa ni watumishi.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na uchangiaji, nilimwita Profesa Kitila Alexander Mkumbo aweze kuchangia.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukurukwa nafasi hii na mimi. Kwanza nitumie nafasi hii kwa kweli kuishukuru na kuipongeza Serikali na Rais wetu kwa kufanikisha kuwaondoa Watanzania kule Sudan katika uwanja wa vita; jambo hili limetujengea heshima. Hawakuondoa Watanzani tu lakini pia wameondoa raia wenzetu katika nchi nyingine za Kiafrika; na dunia yote ijue

kwamba hisia ambayo iliasisiwa na mwalimu Nyerere ikaongoza ukombozi wa Bara la Afrika bado ni ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili na mimi nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Madini na timu yake kwa kazi nzuri ya kusimamia sera na sheria za madini. Nilikuwa naangalia ule mpango wa maendeleo, nadhani ni moja ya Wizara chache ambazo zinaelekea kukamilisha lengo la mpango wa maendeleo ambao tumesema sekta hii ichangie asilimia kumi; kwa jinsi ambavyo tunakwenda tunaweza kufikia hapo. Kwa hiyo tunashukuru na kuwapongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niweke mchango wangu katika eneo moja tu. Ni suala la nafasi ya sekta ya madini kwenye kupambana na umaskini kwenye nchi hii. Hakuna shaka kitakwimu tunakwenda vizuri lakini ukweli ni kwamba sekta hii bado haijatusaidia kwenye kutuondoa kwenye umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nchi zote ambazo zimeendelea ni kwa sababu ya mambo mawili tu ama zina rasilimali watu au na asilimali asili na sisi tunayo rasilimali watu lakini tuna hii moja rasilimali asili muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano, mwezi uliopita, huu Februari kulikuwa na mkutano mkubwa sana pale *Cape town South Africa*, Engaba *Mining Conference*. Kwenye mkutano ule kwa mara ya kwanza Marekani ilipeleka ujumbe mkubwa sana; na ilimtuma mwakilishi wao maarufu Amos Horsen ambaye ni mwakilishi maalum kabisa wa Rais Joe Biden katika sekta ya madini, na hawakuficha. Malengo yao ni mawili, moja Marekani inataka kuona kwamba inatumia sekta ya madini kutatua changamoto za mabadiliko ya tabianchi hapa duniani lakini pili imeweka wazi kwamba imeshangazwa na imeshtushwa na ukweli kwamba kwa sasa biashara kwenye sekta ya madini kwa kiasi kikubwa inatawaliwa na China, kwa hiyo wanataka kuwa-*take over*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni kwamba kuna vita kubwa ya madini inakuja. Haya mataifa mawili yakishaamua kupambana kuna vita inakuja uko mbele. Wametaja madini kwa mfano *Lithium, graphite, Nickel, Cobalt,* wameyataja haya ndio madini wanayalenga. Jumla wameainisha aina hamsini za madini; maana yake ni nini, ni kwamba kuna haja ya kuangalia upya *model* yetu ya uendeshaji wa madini hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshapitia hatua tatu, kwanza tulianza na wakoloni, walipokuja wakoloni hapa Waingereza ule mradi wa Mwadui, wanafahamu watu wa madini, walikuwa wanamiliki *De Beers* ailimia 50, Serikali ya Uingereza asilimia 50. Sisi tulipokuja kwenye Azimio la Arusha tukatangaza kwamba madini yote katika nchi hii yatakuwa chini ya Serikali, ndipo tukaunda *STAMICO*. Haikufanya vizuri sana na sababu zinajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1990 tukahama tukaenda kwenye ubinafsishaji, na tukasema kazi ya Serikali ni kukusanya kodi na kuweka mazingira ya kuvutia wawekezaji basi, uchimbaji na kadhalika waende sekta binafsi. Hii ikatuletea matatizo, ndiyo ikatubakishia mashimo, hatujafaidika sana miaka 20 ya sera hiyo. Naiyo maana mwaka 2015 na 2017 tumekuja na Sheria hizo mbili, tumezitekeleza, tumebadilisha na tumefaidika kwa kiasi. Hata hivyo, kwakweli ambacho kimebadilika kikubwa tumebadilisha sana *numbers* lakini bado suala la umiliki liko mikononi mwa wawekezaji na wawekezaji wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mapendekezo yangu ni kwamba ile sera ambayo tulikuwa nayo mwanzoni, hapa tulipofika Serikali na sisi kama Bunge tukubaliane kuchagua baadhi ya madini ambayo piga ua asilimia mia moja yatakuwa chini ya Serikali. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwenye hotuba yake ameshaainisha madini haya yapo *vanadium*, *Nickel, Graphite,* yametajwa

pale, vizuri kabisa; na hii ambayo ameongea Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria hapo ya mambo ya Liganga na Mchuchuma, tuwekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia uwekezaji, ukiangalia katika miaka, wenzetu wa Tume ya Madini wameanisha madini mengi pale lakini nimechagua saba. Thamani ya uwekezaji wa madini haya kwa miaka kumi mpaka ishirini ijayo ni bilioni 4.385 sawa na tirioni kumi. Mauzo yatakayotokana na uwekezaji huu ni dola za Kimarekani bilioni 63, hii ni *GDP* ya Tanzania kwa sasa *almost*, sawa na trilioni 145. Sisi tutapata nini? Tutapata dola bilioni 17 sawa na trilioni 39 asilimia 27, sijui kama unanielewa hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani uwekezaji wote huo tutaambulia asilimia 27 ambayo ni chini hata ya *corporate tax;* na hapa tumeshachukua *royalty*, *inspection fee*, *corporate tax,* kodi zote, tutaishia kupata tirioni 39; na haya ni madini ambayo ni muhimu sana. Zipo *nickel* na *lithium* humo. Kwa hiyo ninachotaka kupendekeza hapa ni kwamba, tubadilishe *model* ili baadhi ya madini yaende *STAMICO, STAMICO* imarishwe, ipewe mtaji, ipewe watu sahihi ili iwe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na itakuwa siyo sisi peke yetu, wanafanya hivyo Botwana. Botswana yale madini yote ya dhahabu yapo chini ya Debswana *Company Limited* ambayo ni ya Serikali kwa asilimia mia moja. Botswana madini ya dhahabu hayachimbwi na *private sector*. Ukienda India wanayo *NMBC, South Africa* ambayo tunaiona hapo wakati wa Makaburu waliijenga tunayoiona ile kwa sababu ya dhahabu, na walikuwa wanamiliki Makaburu wenyewe. Kwa hiyo hii *model* ambayo tunayo tuchague baadhi ya madini tuwe na *model* tatu. Uwekezaji upo, ipo ya hamsini kwa hamsini lakini ya tatu asilimia mia moja yawe ya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho ni suala la umakini kwa wataalam wetu katika ushauri tunaoutoa kwa Serikali. Hapa tunapoongea nchi yetu ipo kwenye *disputes* mbalimbali za kimataifa ambazo zinatokana na uwekezaji. Nilikuwa napitia *website* ya *dispute and judgement navigator,* tuna kesi takriban saba, tatu za madini. Kampuni ya Montero**,** Nachingwea**,** *Wisher* tumeshitakiwa kule na watu wamepeleka madini; lakini ukiangalia sababu ni kwamba watalam wetu walitushauri wakaishauri Serikali hii, wakasema kwamba baada ya kubadilisha *Mining Act* ya 2017, wakabadilisha zile *regulation 2018,* wakashauri kwamba leseni ambazo zilikuwepo zifutwe, zile *provisional license,* wakasema hakutakuwa na shida, lakini shida ipo. Sasa wasomi wetu walete ushauri wa kisomi sio ushauri wa kishujaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa sekondari kulikuwa na methali inasema kwa mwoga huenda kicheko na kwa shujaa huenda kilio. Wale wanafunzi tuliokuwa tukisoma nao wanajifanya hawataki kusoma, hawasomi kwa bidii, wanakwenda *disco* wanajifanya mashujaa; akitoka *disco* anakwenda kwenye mtihani. Wale ambao walikuwa wanasoma wanaambiwa wanoko wanafanya *revision* kwa umakini wanafaulu, wale wanaopata *division four, division zero* wanalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wa kishujaa ndio huo. Kwamba unamwambia kiongozi hakuna shida usiwe na wasiwasi, humwambii ukweli, tunaingia kwenye kesi hizi na sasa hivi Serikali inalipa fedha nyingi. Wasomi wetu watupe ushauri wa kisomi. Ushauri wa kisomi ukweli ni kwamba huwa ni mchungu; unamwambia kiongozi ushauri ni mchungu, lakini ushauri wa kishujaa unampa kiongozi anachokitaka ili afurahi akupendelee sasa ushauri huo ni ushauri ambao hautusaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya madini imejaa wataalam wazuri wanajulikana nchi hii; hebu watueleze

ukweli ni nini, tusiingize nchi yetu kwenye matatizo makubwa. Si sahihi kabisa kutoa ushauri wa kishujaa ambao siku hizi ushauri wa kishujaa unaitwa ushauri wa kichawa, huo si mzuri na hautusaidii kama nchi. Kwa hiyo ni jambo ambalo niliona niliweke mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti,lakini mwisho, ameongea Mwenyekiti wa Sheria pale; hili la Liganga na Mchuchuma sipendi kuliongelea kwa sababu na mimi nilishapitia huko, wanafahamu Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Mwijage, ni heshima kubwa. Ule mradi *investment cost* yake ni bilioni tatu, kwa nini Serikali kupitia *STAMICO*, kutokana na umuhimu wa mradi huu; kwa nini tusiachane na mambo ya uwekezaji na tutafute fedha, tukope tuwekeze kwenye mradi huu? Kama Serikali imekubali kukopa mradi wa *SGR,* imekubali kukopa kwenye mradi wa bwawa ambao *returns* yake ni *long term*, mradi huu ukishakamilika tunaanza kupata fedha sasa, hii ni muhimu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa mradi huu utatupa *investment* ni *three billion* lakini kwa mwaka tutakuwa tunapata *more than 1.4 billion dollars.* Kwa hiyo maana yake ndani ya miaka kumi tumepata Dola za Marekani bilioni 14; sasa tatizo ni nini? Kwa hiyo naomba Mheshimiwa wa Madini na Waziri wa Viwanda ile *failure* ambayo sisi tuliowahi kuwa mawaziri kwenye sekta hii tumepitia naomba iwaepuke kabisa. Shaurini mamlaka, tuachane na uwekezaji kwenye sekta, hii Serikali ikope fedha tuwekeze wenyewe ili Watanzania waweze kufaidika na mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kitila Mkumbo kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo wakati huo wafuatao wanajiandaa, Mheshimiwa

Zuberi Mohamed Kuchauka na Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga.

**MHE. MRISHO M. GAMBO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nitumie fursa hii kwanza kabisa kushukuru kwa kupata fursa ya kuweza kuchangia Wizara yetu ya Madini. Mimi kwa sababu ya muda nitajielekeza kwenye mambo manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kuhusiana na madini ya tanzanite kuweza kuuzwa kwenye masoko yote ya madini nchini. Hiki kimekuwa ni kilio chetu cha muda mrefu sana. Tunafahamu kwamba tarehe 7 mwezi Julai mwaka 2021 Serikali ilitoa tamko la kuelekeza kuwa madini ya Tanzanite yauzwe kwenye soko moja la Mererani peke yake. Lakini masoko haya ya madini ni masoko ambayo yapo kwa mujibu wa Sheria; na sisi watu wa Arusha tuna bahati moja kubwa sana. Wakati nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ndugu yangu na rafiki yangu Mheshimiwa Daktari Dotto Biteko alikuja pale Arusha akatuzindulia soko letu la madini, na soko hili limekuwa ni soko lenye mafanikio makubwa sana kwenye nchi hii ya Tanzania lakini cha kushangaza baadaye Serikali hiyo hiyo na chini ya Waziri huyo huyo ikaja na kanuni zilizobadilisha mfumo wa kufanya biashara ya madini hasa biashara ya madini ya tanzanite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya *consultations* nyingi na Mheshimiwa Waziri wa Madini kama sekta husika na wadau wote wa masuala ya madini. Kwa pamoja wameona changamoto ambazo zimetokana na matamko hayo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kimsingi ningependa leo niwape taarifa ifuatayo; kwamba wakati ule Mheshimiwa Waziri alipokuja kuonesha soko la Madini mwaka 2019 kwa mwezi wa saba mpaka wa kumi na mbili 2019 tuliweza kupata madini ya tanzanite yaliyosanifiwa na kung'arishwa

*karat* 76,303 na thamani yake ilikuwa ni bilioni 24. Kodi iliyopatikana Serikalini ilikuwa ni milioni 487. Lakini kwa madini hayo hayo ya tanzanite ambayo yalisanifiwa na kung'arishwa baada ya kuhamishiwa Mererani sasa mwaka 2021kuanzia Januari hadi Disemba tuliweza kuwa na karati 15,820 kutoka karati 76,000. Tuliweza kupata thamani yake ya shilingi bilioni mbili mia sita thelathini na sana kutoka bilioni ishirini na nne, mia tatu na sitini na moja; lakini pia na kodi au ada iliyolipwa ilikuwa milioni 52 kutoka milioni 487.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pia kwenye upande wa madini ya tanzanite ambayo ni ghafi yaliyo chini ya *two grams,* kwa upande wa soko la Arusha kwa *July-December* 2019 utakuta *karat* ambazo zilipatikana zilikuwa ni 7,920,000, thamani yake ilikuwa ni bilioni 12, kodi na ada zilikuwa ni milioni 848, na jumla ya thamani ilikuwa ni bilioni 36 na jumla ya kodi yote ilikuwa ni 1,336,000,000. Kwa upande wa Mererani kuanzia *July* hadi *December* 2021 utakuta madini hayo ambayo ni ghafi chini ya *gram* mbili tulipata shilingi 3,467,000,000 kutoka bilioni 12, lakini pia walipata *karat* 10,000 kutoka *karat* 7,920,000,000. Jumla ya mapato yake yalikuja milioni 39 kutoka 1,336,000,000. Tumepata hasara si chini ya asilimia 70. Kwa hiyo vielelezo kama hivi vinaonesha kabisa Serikali inayo sababu, inayo haja na kuna tija kabisa ya kutafakari maamuzi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiacha hasara hiyo bado pia tumeweza kupata hasara kwenye upande wa ajira. Kuna ma-*broker* pale kati ya 2,500 hadi 3,000 ambao leo wamekosa ajira kwa sababu ya fursa hii ambayo imeondoka kwenda kwenye eneo jingine. Yawezekana Wizara ya Madini kwa data zao ma-*broker* wakawa ni wachache kwa sababu wengine wengi wameacha kukata leseni kwa sababu mwisho wa siku wameona fursa hiyo imeondoka kwenye eneo hilo. Bado pia kuna majengo ya Serikali ukienda *AICC, NSSF*, *PSSSF* nako pia kulikuwa na mashine 437 zimefungwa, ambapo zile mashine leo hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiangalia na hiyo bado kuna kodi ambayo Serikali ilikuwa inapata kwa kila *square meter* katika jengo lile. Kwa hiyo, kwa ujumla wake naona maamuzi haya kwa kweli hayana tija na yameitia hasara nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia sizungumziii Arusha tu peke yake, hizi *data* ni za sehemu moja tu, nenda Mkoa wa Dar es Salaam, nenda Mkoa wa Mwanza, nenda Mbeya, nenda Zanzibar, nenda kwenye masoko ya madini yote nchi nzima utagundua kwamba hasara ni kubwa kupita kiasi na Serikali yetu chini ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Serikali ambayo imetoa motisha sana kwa wafanyabiashara. Kwa hiyo ni imani yangu Serikali ya Awamu ya Sita itakwenda kupitia maamuzi haya ili mwisho wa siku tuweze kurejesha furasa hii kwenye masoko yote ya madini nchi nzima ambayo yapo kwa mujibu wa sheria na watu waendelee kunufaika na fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tulikuwa tumeendelea kujenga hoja kwamba siku za nyuma kulikuwa kuna minada ya madini inafanyika, pia kulikuwa kuna maonesho ya madini yalikuwa yanafanyika, hapa katikati yamepotea. Minada ile na maonesho yalikuwa yanasaidia pia kwenye utalii, inaleta wageni wengi kutoka nje ya nchi. Siku za nyuma tulikuwa tunafanyia pale kwenye Hoteli yetu ya *Mount* Meru, leo kuna hoteli nzuri nyingine ya Melia na Hoteli nyingine nzuri zaidi zimejengwa kwenye mji wetu. Kwa hiyo, fursa ikirudishwa itasaidia kwanza kuleta wageni ambao watalala kwenye mahoteli, watanunua bidhaa mbalimbali na mwisho wa siku fursa zitakuwa ni kubwa zaidi. Kwa hiyo tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Madini atusaidie kuhakikisha kwamba maonesho yanarudishwa, minada inarudishwa ili kuongeza fursa mbalimbali katika biashara na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusiana na changamoto ya wafanyabiashara ya vito, watengenezaji na wauzaji nwa bidhaa za usonara kwa maana ya urembo na dhahabu nchini. Hapa ndio sielewi kabisa, sijui kuna changamoto kubwa kiasi gani. Ukiangalia Sera ya Madini ya mwaka 2009 inasisistiza kuwahamasisha Watanzania na wananchi wote duniani kuweza kuongeza thamani ya madini yetu. Hata hivyo, ukiangalia Sera inavyosema na ukiangalia matakwa ya kisheria yaani ni mbingu na ardhi, ni vitu viwili tofauti kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015, Serikali yetu ilianzisha Mchakato wa Rasimu ya Sheria ya Uongezaji wa Thamani ya Madini, ilikuwa iitwe *Mineral Value-Added Act,* lakini kabla ya hapo kulikuwa na sheria ambayo Sheria hii kama ingeanzishwa ililenga kufuta ile Sheria ya *Gold Smith and Silver Smith Act, CAP 228.* Hii Sheria ya nyuma hata sielewi nchi yetu ina changamoto kubwa kiasi gani. Ukiangalia kwenye upande wa biashara ya Usonara. Ili mtu aweze kufanya biashara ya Usonara anahitaji kuwa na leseni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leseni ya kwanza ni *Metallic mineral dealers license,* kuna maombi dola 200 na kuna kulipia leseni dola 1000; Kuna *Game stone dealers license,* kuna maombi dola 200, kulipia leseni dola1000; Kuna *Diamond dealers license* maombi dola 200, kulipia *dealer* dola 2000; *Gold dealers license* maombi dola 200, ada ya leseni dola 1000; na *Business license* 300,000 unalipia Wizara ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijumlisha gharama zake zote zinakuja sio chini ya Shilingi Milioni 13. Sasa unajiuliza hivi leseni na yenyewe ni chanzo cha mapato au leseni ni namna ya kumtambua mfanyabiashara aingie kwenye mfumo ili mwisho wa siku sasa Serikali iweze kumtambua, afanye

biashara na aweze kulipa kodi. Mwisho wa siku sasa tunajikuta na leseni imekuwa ni chanzo cha mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ile sheria ambayo ilikuwa inatakiwa kutungwa ya *Mineral Value Added Act* mchakato wake ambao uliishia mwaka 2016 kwenye kikao cha Makatibu Wakuu, Waziri achukue Sheria hiyo iendelee na mwisho wa siku alete Bungeni hapa tuweze kuhitimisha na Watanzania waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kumalizia tunalo ombi pia, tunaomba uwepo wa leseni moja ya wafanyabiashara wa madini nchi nzima, ikishindikana kabisa basi watoe angalau kikanda. Leo mtu anaomba leseni akienda Mererani awe na leseni, akienda Arusha aende na leseni, akienda Shinyanga afungue leseni halafu kwenye kila Mkoa *TRA* wanawaita wale watu kwa ajili ya kuangalia masuala ya kodi na masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona Mtanzania ana kitambulisho kimoja tu cha *NIDA*? Kwa nini pia na leseni isiwe moja ila waweke mfumo mzuri kila anapokwenda kufanya biashara kwenye Mkoa fulani aende akaripoti kwa Afisa Madini wa Mkoa huo na mwisho wa siku aweze kuendelea na shughuli zake. Huo urasimu wa kuwa na leseni kila mahali, hauna tija na unawaongezea tu gharama wafanyabiashara lakini pia usumbufu na kuwapa fursa *TRA* kuendelea kuwachungulia chungulia kwenye masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuhusiana na kodi ya *PAYEE* na *SDL* kwa wachimbaji wadogo wa Mererani. Siku za nyuma hili suala lilizungumzwa sana na nadhani lilieleweka, kwa sababu kutokana na *nature* ya biashara ya madini ukimwambia mchimbaji mdogo wa madini leo alipe *PAYEE* na *SDL …*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mrisho Gambo kwa mchango wako, muda wako umekwisha.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa Zuberi Mohammed Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji kwenye hotuba hii. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai wa kuweza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu leo na kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya madini kwa kazi kubwa anayoifanya. Kwa kweli kazi yake tumeiona akisaidiana na Naibu wake, lakini hata watumishi wengine wakiongozwa na Katibu Mkuu kwenye idara hii wanafanya vizuri, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze na hawa jamaa wanaitwa *GST*. Nashukuru sana Waziri aliwaleta vijana wake wakaja pale Mpigamiti, wamekaa mwezi mzima. Pamoja na kazi nzuri waliyoifanya ya utafiti wa madini pale Mpigamiti wametuachia uchumi vile vile na wajomba tunao pale. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba wale vijana watarudi pale kuja kusalimia wajomba zetu wale. Kwa hiyo, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo hili naomba niseme kidogo. Pamoja na utafiti ule, lakini matokeo yale ya utafiti yamebaki kuwa kwenye Ofisi zao. Sisi watu wa Liwale hata Madiwani kushirikishwa wakafahamu matokeo ya utafiti

ule hayajaachwa pale. Kwa hiyo, nini kinachotokea? Kinachotokea kwa sababu wamekwisha ingiza kwenye mambo yao ya mitandao huko, tayari tumekwisha anza kupokea wageni kutoka kwenye mikoa mbalimbali wakija kuchukua vitalu pale kwa ajili ya uwekezaji wa madini, lakini wenyeji wa pale hatuna habari yoyote. Matokeo yake ni nini? Matokeo yake sasa sisi tutakuwa wasindikizaji badala ya kuwa sisi washiriki kwenye shughuli hiyo ya uchimbaji wa madini. Ukizingatia sisi Mkoa wa Lindi tasnia hii ya madini ni ngeni kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa ni vizuri baada ya utafiti ule kukamilika, basi wangewaacha wale vijana wakaja kutupatia matokeo, angalau kuongea na Madiwani, kuongea na Viongozi wa Vijiji kwamba jamani kwenye utafiti wetu kwenye hii wilaya yenu tumekuta hiki na hiki, ili na sisi tuweze kuwa ni miongoni mwa watu wanaoshiriki katika huu uchimbaji wa madini hasa wale wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, pamoja na matokeo hayo ya kuonesha kwamba Liwale kuna madini ya aina mbalimbali, sasa hivi kule kuna wachimbaji wadogo wadogo wameanza kuchimba dhahabu, lakini vile vile kuna wawekezaji wameanza kuchukua vitalu, Kuna *nickel* pale na *graphite*, madini haya yote yamekwisha onekana kwamba kwa ukanda ule wa Liwale ni mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba mpaka leo hii wale wachimbaji wetu wadogo wanapata shida sana kwa sababu hatuna soko. Liwale hakuna duka la uuzaji wa madini, matokeo yake vijana wale, wachimbaji wadogo wanalazimika kusafiri kutoka Liwale kwenda Tunduru ama kwenda Ruangwa, jambo ambalo linaleta usumbufu kidogo. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, ili kuonekana kama kweli ile kazi waliofanya wale watu wa *GST* ina manufaa kwa watu wa Liwale, basi watufungulie duka ili

vijana wale waendelee kufanya uchimbaji ule na kupata fedha pale pale Liwale Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hata kwenye ile Idara yenyewe ya Madini, pale hatuna Mtumishi hata mmoja. Kwa hiyo, unapopata jambo fulani linalohitaji ufafanuzi au umepata jiwe fulani huna hata mahali pa kwenda kuuliza kwamba hii ni madini ya aina gani na thamani yake ni nini? Matokeo yake watu wengine wanaibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri mwaka 2022, kuna jamaa mmoja ameokota jiwe pale amekwenda mpaka Tunduru. Alipofika Tunduru akalala, asubuhi akaonana na tajiri akampa milioni 10 akasema chukua hii milioni 10m kesho uje tufanye biashara. Yule alipopata ile milioni 10 akaishia mitini, akijua kwamba hawa jamaa wanataka kunitapeli, wataninyang'anya hii milioni 10, kumbe madini yale yalikuwa na thamani kubwa sana. Kwa hiyo alipoteza kwa sababu ya kukosa hiyo elimu. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, ahakikishe Liwale tunapata duka la uuzaji wa madini, lakini vile vile tunaomba tupate mtaalam ambaye atakaa pale Liwale kwa ajili ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukiangalia umbali kutoka Liwale kwenda Nachingwea ni zaidi ya kilomita 120 na kutoka Liwale kwenda Tunduru ni umbali wa zaidi ya kilomita 200. Kwa hiyo mara nyingi wale wachimbaji wetu wadogo wanaibiwa njiani, wanatekwa na wanafanyiwa mambo mabaya. Kwa hiyo, niombe sana jambo hili lichukuliwe kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hivyo tu ninapozungumzia kuwapa elimu Madiwani wetu ni kwa sababu nasikia kwenye hayo machimbo ya madini kuna kitu kinaitwa *CSR,* sisi Liwale tunachinba madini sasa hivi ni mwaka wa tano kama sio wa sita, lakini Halmashauri haijawahi kupata hata thumni na wala haijui tunapataje fedha kutokana na ule uchimbaji mdogo

wa madini. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, nimeomba dakika tano hizi nizungumze ili hili jambo lifike na naomba alitilie mkazo sana na elimu kwa wachimbaji wadogo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho kabisa, kama nilivyosema baada ya kugundulika kuwa kuna madini, vitabu vimeoneshwa watu wa Liwale hawana taarifa, lakini kwenye vitalu wameandika vipo na watu tayari wanaingia kwenye tovuti wanaangalia. Sasa hivi vitalu vyote vya Liwale vimekwishachukuliwa na watu. Ukienda pale unakuta kuna madini na una mwekezaji unaambiwa kuna mtu, ukiingia kitalu hiki unaambiwa kuna mtu, lakini hao wawekezaji ambao tayari wamekwishachukua leseni kule wako wapi? Hivi kuna utaratibu gani mtu anachukua kitalu mwaka mzima hajawekeza chochote. Sasa pale kwa mfano, alikuja mwekezaji mmoja kwa wananchi, akasema kwamba yeye eneo lile amekuta kuna madini ya *nickel,* anataka kuchimba *nickel* pale, akaja akarubuni rubuni watu, ameondoka sasa hivi ana mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jamaa mwingine amekuja mwaka 2023 kuchukua leseni tukamwambia lile eneo lina mtu tayari, sasa huyu mtu anawacheleweshea wale wanakijiji maendeleo yao pale, kwa sababu yeye hajawekeza, sasa amekuja mwekezaji lakini eneo lina mtu. Kwa hiyo, nimwombe Waziri, sijui taratibu za leseni zikoje, sijui mtu mmoja anatakiwa kumiliki hilo eneo kwa muda gani? Kama kuna uwezekano ombi langu, wale watu ambao wamechukua vitalu muda mrefu na hawajaanza uwekezaji wowote, basi leseni zao zifutwe ili hawa wawekezaji wapya wakija na sisi tuweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo tu. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nilimwita Mheshimiwa Asia Halamga wakati huo Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya pamoja na Mheshimiwa Salome Makamba wanajiandaa.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi nami ya kupata kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Madini 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo anaendelea kutengeneza mazingira bora ya wawekezaji, lakini na wawekezaji wa ndani na kuendelea kuangalia Wizara ya Madini kama sehemu ya kuongeza kipato ndani ya Taifa letu. Vile vile bila kusahau niendelee kupongeza kazi kubwa ambayo inafanywa na Waziri, Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko pamoja na Naibu wake na timu nzima ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, sisi watu wa Manyara tunasema tunamwombea kwa Mungu afya njema lakini kura tulishamaliza kupiga, tunasubiri sanduku tuletewe ili tuweze kuzidumbukiza na ni kura za ndio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya hivyo kwa sababu, tunamshukuru alituletea zaidi ya Shilingi Bilioni 5.9 kujenga *one stop center* ya ununuzi wa madini katika Mji wa Mererani. Vile vile, tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kupitia kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mpaka sasa tayari tumeshapokea kiasi cha fedha cha Shilingi Bilioni 1.59 ambao ujenzi umeshaanza ghorofa la kisasa la soko liliwekwa pale katika Mji wa Mererani na sisi tumepata sehemu ya kuwa tunakwenda kupigia picha kwa sababu ni kazi nzuri ambayo imefanywa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi *floor* hizo nne tayari Serikali ya Mkoa imeshaanza kupata maombi ya wafanyabiashara, yaani jengo halijakamilika lakini wafanyabiashara tayari wamekuja wanahitaji kupangisha. Hakika hongera sana kwa Wizara ya Madini, ahsante sana Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupongeza jitihada zizo, tuendelee kumshukuru kwa namna ya kipekee, Watanzania wote kwa ujumla kwa sababu wanaochimba Mererani ni Watanzania kutoka pande zote za nchi yetu. Tuna kila sababu ya kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kuruhusu Kitalu C ambacho kilifungwa zaidi ya miaka minne huko nyuma na sasa vijana zaidi ya 100 wameshapata ajira na ajira zinaendelea kutoka, lakini pia kipato kinaendelea kuongezeka kwa wananchi mmoja mmoja, kwa wachimbaji, lakini pia pato kubwa kwa Serikali. Ahsante sana Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuishukuru Serikali yetu Tukufu ya Chama cha Mapinduzi, niombe Serikali mambo yafuatayo katika Mji wa Merelani kwa maana ya machimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, Mji wa Mererani ili kupata madini yale kupasua miamba kunatumia baruti na vumbi ni kubwa na wananchi wetu wanapata ugonjwa wa *TB*. Katika Mji wa Merelani *TB* ni kubwa sana na ukiangalia kwenye takwimu mara ya mwisho mwezi wa Nane mwaka 2022, watu waliojitokeza kupima ni watu 2,024, lakini watu waliokutwa na maambukizi kwa wale ambao walipima kwa hiari ni watu 382 na ambao wanapata dawa mpaka sasa ni watu 371.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu kwa Serikali, kwanza kabisa tunaomba wachimbaji hao wadogo matibabu yao na hasa vumbi hili na athari ya ugonjwa wa *TB,* matibabu

wanaenda kupata katika Mkoa wa Kilimanjaro Hospitali ya Kibong'oto. Mheshimiwa Waziri tunalo eneo kubwa linaloweza kujengwa hospitali na kuweza kuwasaidia idadi kubwa ya wananchi walioko Mererani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *shift* moja wanapoingia kufanya kazi kwenye ile migodi ni zaidi ya wananchi 2,000 mpaka 3,000 na idadi kubwa ni kundi la vijana. Kwa hiyo, ili tuweze kulinda rasilimali na nguvu kazi ya vijana wa Kitanzania, basi tuweze kupeleka huduma ya afya katika Mji wa Mererani kwa sababu ni idadi kubwa ya vijana wa Kitanzania wanafanya kazi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Mheshimiwa Rais nia yake ni njema, dhamira yake ni njema na lengo ni jema. Sambamba na kujengwa Mji wa *One Stop Centre* pale Mererani, tumuombe sasa Wizara ya Maji iende sambamba na ujenzi huu ili kukuza, kwa sababu mji ule sasa hivi una watu wengi, una wakazi wengi ambao ni Watanzania kutoka maeneo yote, lakini changamoto ya maji ni kubwa. Tuendelee kuomba japo tunamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji anaendelea kupambana, lakini bado tuombe *speed* iongezeke ili kuweza kutatua changamoto hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunaomba ujenzi wa barabra. Barabara zilizopo ni mbovu, zimekuwa ni shida. kwa hiyo, tunaomba sana Wizara nyingine ziende sambamba na lengo la Mheshimiwa Rais la kuhakikisha *One Stop Center* hiyo inakuwa ni ya kisasa na Mji wa Mererani unafanana na kile ambacho kinatoka katika pato la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe *GST* iweze kuja kuendelea kufanya utafiti, lakini pia kuleta vifaa. Ndani ya Mkoa wa Manyara hatutegemei tu madini ya *tanzanite,* yapo madini mengi mfano kule Simanjiro kuna *green garnet*

lakini changamoto iliyopo ni umeme, barabara pamoja na maji. Kwa hiyo, tukipata umeme itasaidia sana wananchi wadogo wadogo kutokutumia gharama za kutumia jenereta na kununua *diesel*. Kwa hiyo, tunaomba sana ili kuendelea kukuza pato la wananchi na pato la Taifa, basi miundombinu kama umeme, maji yaweze kupelekwa pamoja na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo madini mengine ya dhahabu kule Mbulu ambapo mashapo yapo ya kutosha, lakini wananchi hawa wa kawaida wadogo wadogo hawana sehemu rasmi ambapo wanaweza wakatoboa wakajua mwamba upo hapa. Kwa hiyo, tuiombe sana *GST* iweze kuja kufanya kazi ili kuwarahisishia wananchi wetu wadogo wadogo wafanye kazi si kwa muda mrefu, lakini kazi yenye faida na kulinda uchumi wao mdogo na mtaji wao mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo madini Kiteto, Mkoa wa Manyara karibu maeneo yote yana madini, lakini kwa namna ya kipekee niongelee Wilaya ninayotoka Wilaya ya Hanang. Hanang ukienda Gehandu, ukienda Mogitu, ukienda Gendabi, tuna madini ya chumvi wanakuja watu kutoka nchi zingine wananufaika, tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri tunaomba mtoe *support* kwa wawekezaji wetu wadogowadogo wa ndani ili waweze kukuza uchumi na waweze kuvuna rasilimali hii kubwa katika nchi yetu na iweze kuleta mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao uwezo wa kuchimba simenti kule badala ya kuendelea kutumia simenti kwa kununua kwa bei ghali, tunaweza kuwaleta watu kule na wakaweza kutusaidia. Hali kadhalika ipo chumvi ya kutosha tunaomba sana Serikali yetu sikivu ituletee wawekezaji ili na sisi siku moja wananchi wa Hanang waweze kuona kuna kiwanda kiko kule na waweze kupata ajira na kusaidia wananchi wa chini na kusaidia pato la Taifa la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwa heshima na taadhima Wizara ya Kazi, mwanzoni kulikuwa kuna kampuni ya Tanzanite ambayo ilikuwa na wafanyakazi wengi sana na kamapuni hiyo ilikuwa ina muunganiko na *STAMICO* lakini baada ya kampuni hiyo kuondoka ama kuacha kufanya kazi ya uchimbaji, zaidi ya Watanzania wafanyakazi 540 wanadai zaidi ya Bilioni 2.5 tunaiomba sana Wizara ya Kazi iendelee kuwasikiliza wananchi hawa itatue kero, maana imekuwa ni kero kwa viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi wanapokuja Mkoani wananchi hawa ndio wamekuwa ni kimbilio lakini tunaiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Kazi iweze kuliangalia jambo hili na wananchi wale wajivunie kufanya kazi ndani ya nchi yao ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia mabadiliko ya Sheria ya Muundo wa Utumishi, tuombe sana Mheshimiwa Waziri mabadiliko haya hebu yamalizike mchakato wake ili kuweza kuwasaidia watumishi wako wa Wizara kuweza kupata kipato wanachostahili, kwa sababu kazi wanayoifanya ni kubwa wanaletea nchi yetu kipato kikubwa, lakini maslahi yao ukienda kuangalia watumishi hawa hakika hayastahili na tunahitaji kupata watu ambao watazidi kuwa waaminifu, kuwa wazalendo japo sasa hatuna shaka na uadilifu wao na uzalendo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa mimi binafsi na ninaamini na Watanzania wote na hasa Wabunge tuliomo huku ndani, ni nani kama Samia Suluhu Hassan, ni nani kama Samia Suluhu Hassan? Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia tunampongeza sana mama yetu kipenzi Rais Samia, Watanzania tumemuelewa Serikali ya Awamu ya Sita inafanya kazi, tunayaona wananchi huko chini, mimi kama kijana na vijana wenzangu tutasema mema yanayofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana Serikali ya Awamu ya

Sita, ahsante sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asia Halamga kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Salome Makamba, wakati huo Dkt. Pius Stephen Chaya pamoja na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa wanajiandaa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie bajeti hii ya madini kwa mwaka 2023/2024. Nami niungane tu Wabunge wenzangu kuwapongeza Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanafanya ya kusimamia sekta hii nyeti ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunajisifu kwamba tumefanikiwa sana kukusanya mapato kudhibiti wizi katika sekta ya madini bado tunalo jukumu moja kubwa la msingi ambalo hatujalitimiza la kuhakikisha maeneo au watu wanaoishi kwenye maeneo yenye madini wanafanana na thamani ya madini yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nitaliongelea kwa maeneo mawili tu kama maeno ya mfano eneo la kwanza ni eneo la fidia kwa watu ambao wanapisha wawekezaji wa maeneo ya madini. Hawa wananchi ukienda kufanya tathmini ya haraka, kabla hawajapisha maeneo yale walikuwa wana maisha mazuri wakishalipwa fidia ni kweli wanalipwa fedha nyingi lakini miaka kadhaa baada ya kulipwa fidia wale watu wanarudi kwenye ufukara na umaskini uliokithiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa sababu mwisho wa siku kumpisha Mwekezaji siyo lazima akulipe fidia peke yake, kwa nini Wizara isitengeneze mipango ya muda mrefu angalau hao watu wanaoishi kwenye maeneo ya madini waweze kupewa hisa nao wawe sehemu ya makampuni hayo ambayo yanawekeza. Jambo hili litawafanya hao watu

wawe na pesa za muda mrefu, zitawafanya wawe na Maisha ya muda mrefu, itawafanya hata kama watapoteza fidia kidogo waliyopewa ile awali basi wanaweza kuendelea kuboresha uchumi wao kupitia hisa zile ambazo watakuwa wanalipwa mwaka hadi mwaka *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilisisitize ni eneo linaitwa *corporate social responsibility*. Watu wanaoishi kwenye maeneo ya madini hawafanani, na mimi nimetoka Shinyanga, hawafanani na madini yanayochimbwa, hawafanani na utajiri ambao Mwenyezi Mungu ametujalia. Kwa mfano, ukienda Tarime pale tulienda juzi na Kamati yetu ya TAMISEMI wale watu wamepewa Bilioni Saba hela ya *corporate social responsibility* ile pesa waliyopewa ukifika pale hauoni matokeo ya Bilioni Saba kuingia katika Halmashauri ya Tarime huioni! Ukiuliza wanasema sisi Halmashauri sheria iko vizuri inaonesha kwamba Halmashauri lazima uishirikishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri inashirikishwa kwa maana ya kuchagua miradi ya kutekelezwa lakini Mkandarasi anayeenda kutekeleza mradi ule anaamuriwa na mgodi, aina ya *class* ya Mkandarasi na ujenzi wa jengo inaamuriwa na mgodi! Kama Serikali inaweza kujenga madarasa kwa Shilingi Milioni 20 ni kwa nini tumruhusu mgodi alete Mkandarasi ambaye anakuja kujenga shule ya aina ileile kwa gharama ya zaidi ya Milioni 500 kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi….

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Waitara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**TAARIFA**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Salome Makamba kwamba anaendelea kuchangia vizuri lakini pia mimi ni Mjumbe mwenzake wa Kamati ya TAMISEMI, nadhani amechanganya maelezo Jimbo la Tarime Vijijini ambalo mimi ndiye Mbunge wake na Halmashauri tunaongoza, hizo shilingi bilioni 7.3 ambazo zimetolewa sasa hivi, ziko zinazunguka kwenye Kata 26 tunatumia *Force Account* siyo Mkandarasi kutoka mgodini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika fedha ambazo zilitolewa mwaka 2019/2020 wakati ule sikuwa Mbunge wala hatukuwa tunaongoza Halmashauri, shilingi bilioni 5.7 ndiyo ambazo alikuwa analipa Mkandarasi na miradi ina viporo mpaka leo, hilo ndilo ambalo lilielezwa kwa Kamati hiyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba unapokea taarifa?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona jamaa anadhani tunafanya kampeni hapa. Wamemsikia watu wa Tarime nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa inayotolewa ya *CSR* sheria iko wazi Mheshimiwa Waziri tusaidie, Mkandarasi aamuliwe na Halmashauri na *Force Account* ndiyo iamue nani ajenge, nani alipwe, wakati gani na mradi gani utekelezwe ambao utaacha alama kwenye maeneo ambayo yana madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye suala la mikopo ya wachimbaji. Mheshimiwa Waziri

mimi niliwahi kuchangia hapa nikakuomba sana uwasaidie wachimbaji wadogo wapate mikopo kwa sababu na wale wanafanya uwekezaji na wanachangia kwenye nchi hii. Mheshimiwa Waziri uliniahidi na kweli umeenda kuwapelekea mikopo, sasa mikopo uliyowapelekea Mheshimiwa hizo benki ulizowapelekea zinazotoa mikopo wanataka hati za nyumba, hizo benki wanaopelekewa mikopo riba zao ni za kibiashara, marejesho yao ni kwa mwezi, bado mazingira ni magumu sana kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Serikali inalo fungu la pesa kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo, Serikali inakusanya pesa kupitia wachimbaji wadogo, ni kwa nini Serikali isitenge ruzuku kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji ili mwisho wa siku na wao waweze kuchangia katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema leo tunaenda kuwatoza, hawa wachimbaji wadogo tozo nyingi wanazotozwa wanatozwa katika mitaji yao, uwekezaji katika sekta ya uchimbaji mdogomdogo mtu anaweza akawekeza mpaka mwaka mpaka miezi miaka miwili lakini kodi analazimishwa kulipa kila mwezi, na Halmashauri kila siku inatunga sheria, utasikia sijua Afisa Biashara anataka kodi, Afisa Mazingira anataka kodi, mlundikano wa kodi ni mkubwa sana. Tusiwape mikopo ya kibiashara wachimbaji wadogo hatuwasaidii, tunawanyonya ndiyo maana watu wanaishia kukwama huku wanatelekeza famila zao.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye masuala ya mabwawa ya matope na mabwawa ya sumu. Nchi hii ilichafuka sana kipindi cha nyuma kule kwenye Mgodi wa *Barrick* wa Nyamongo, bwawa lilipasuka la sumu na watu wakapata madhara, tukapelekwa Mahakamani tukashitakiwa na nini na hekaheka zikawa nyingi sana. Juzi pale Mwadui bwawa la tope limepasuka pia, tunamshukuru Mungu madhara hayakuwa makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningeomba nipendekeze Serikali ifanye tathmini ya haya mabwawa mara kwa mara, kwa maana ya kwamba iwe angalau kila baada ya Miezi Sita Serikali ipite ifanye tathmini ili kuhakikisha kwamba mabwawa haya ni salama kwa maisha ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali inapokuja kujibu inipe majibu, maana mimi ni Mbunge ninatokea Shinyanga lakini sijaipata ripoti ya tathmini ya madhara ya kupasuka kwa bwawa la tope la Mwadui, ninataka nijue ushiriki wa Serikali katika kufanya tathmini, ushiriki wa Serikali katika kutoa fidia na kuwarejesha wale watu katika maisha yao bora kuliko walivyokuwa zamani. Kwa sababu lile bwawa lilipasuka tope lilifunika nyumba, mali zilipotea, sasa nataka nijue nini ilikuwa ushiriki wa Serikali katika kudhibiti kupasuka kwa bwawa la tope la Mwadui na *compensation* waliyopewa wale watu, tathmini ilifanyikaje ningetamani sana kupata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa yote naendelea kusisitiza kwa Mheshimiwa Waziri anakusanya mapato, anachangia kwenye bajeti ya Serikali lakini na sisi wananchi kutoka kwenye maeneo ya uchimbaji, tunataka tufanane na rasilimali zilizoko katika maeneo yetu, fidia peke yake haitoshi tunataka tulipwe fidia lakini tuwe sehemu ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana leo mwekezaji anajenga shule anajenga vituo vya afya mwisho wa siku watu wana *vandalize* kwa sababu mtu anaona hiki ni kituo cha afya cha mwekezaji, hiki ni kituo cha afya cha mgodi, lakini kama mimi mwananchi ninayetoka Shinyanga ninayetoka Kakola ninayetoka Mwadui nitaona kwamba huu mgodi ni sehemu ya mimi na unaninufaisha lazima nilinde rasilimali zote ambazo zinajengwa na mgodi, lazima nilinde mali zote ambazo tunajenga mimi pamoja na mgodi nikiwa

kama sehemu ya uwekezaji wa mwekezaji huyo. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamba. Nilimuita Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya aweze kuchangia.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukua nafasi hii kukushukuru wewe kunipa hii nafasi ya kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Madini. Kipekee ninamshukuru sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika Taifa letu la Tanzania, namshukuru Ndugu yangu mtani wangu, Waziri wa Madini Dkt. Biteko na Kaka yangu pale Naibu Waziri wa Madini Dkt. Kiruswa. Pia ninampongeza na kumshukuru Afisa Madini wa Mkoa wa Singida kwa ushirikiano mkubwa ambao anaendela kutupatia watu wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nitaongelea mambo mawili jambo la kwanza nitaongelea fursa ya madini ya dhahabu - Manyoni lakini jambo la pili nitaongelea fursa ya madini ya chumvi - Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na fursa ya madini ya dhahabu Manyoni. Mika miwili iliyopita Rais wetu wakati akiwaapisha Makatibu Wakuu kama sijakosea aliwahi kutamka na alitoa *challenge* kwa Wizara mbili, Wizara ya Madini na Wizara ya Maliasili aliwaambia kuna baadhi ya mapori ya akiba na hifadhi yanasemekana kwamba yana madini, lakini inaonekana hakuna jitihada zozote zile za kuhakikisha yale madini yanachimbwa, na akasema kwamba hivi wale Tembo na Digidigi watakula hayo madini, hizo dhahabu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki na katika Wilaya ya Manyoni tuna mapori ya akiba matatu, tuna Pori la Akiba la Kizigo, tuna Pori la

Akiba la Muhesi na tuna Pori la Akiba la Rungwa. Katika haya mapori yote matatu kuna viashiria vya madini. Huko nyuma iliwahi kutokea *booming* ya madini ya dhahabu katika Kata ya Sasilo, eneo linajulikana Iruma ambako kuna Pori la Akiba la Muhesi na Kizigo. Vilevile katika Kata ya ya Rungwa, Kata ya Mwamagembe kuna madini ya dhahabu na kule nako kuna pori la akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Iseke Kijiji cha Simbangulu kuna eneo linaitwa Myunga, hili ni eneo mabalo ni *very popular* kwa watu wanotoka Kata ya Isseke, kila nikienda kufanya mikutano kwanza wananchi wanalalamika sana, kila wakati wanafukuzwa na watu wa Maliasili, kule kunasemekana vilevile kuna viashiria vya madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi sasa kwenye ile kauli aliyoitoa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, aliwapa *challenge* hizi Wizara mbili waende wakatafakari watuambie, kwa nini kama kuna maeneo ambayo yana madini ni Hifadhi za Taifa au Mapori ya Akiba, kwa nini tusije na utaratibu rafiki wa kuhakikisha kwamba tunakuwa *it is a win-win situation,* wafanye *cost benefit analysis,* watuambie hivi tukisogeza mpaka tukachimba madini, je italeta athari kwenye hizo hifadhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni nini? Ningemshauri Waziri wa Madini na Waziri wa Maliasili na Utalii watuletee taarifa kutokana na kauli aliyoitoa Rais mmeifikia wapi, hatujaona utekelezaji wa agizo la Rais. Rais akishatamka ni agizo lakini mpaka leo hii tukienda kwenye mikutano watu wanauliza mbona Rais alishauri, aliagiza hatuoni utekelezaji? Kwa hiyo, nawashauri hawa ndugu zangu wawili Waziri wa Madini na Waziri wa Maliasili na Utalii hebu nendeni mkalichakate hili, mtuambie kama kuna *potentiality* ya sisi kuchimba yale madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingene sanjari na hili ukiangalia kwa mfano yale mapori ya akiba ukiangalia michango yao hata kwenye ile *service levy* ya Halmashauri ni ndogo sana, kwa mwaka sijuwanachangia Milioni 30 tu, sasa ukiangalia *contribution* yake *is almost insignificant*. Kwa hiyo, mimi ningeshauri kwa kweli tuangalie kama hayo maeneo tunaweza tukawachia wenzetu wa madini, wakachimba na yakawa na *impact* kubwa kwenye *GDP* lakini yakawa na *impact* kubwa kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri mimi ningeweza kushauri hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tuna madini eneo linaitwa Londoni ya dhahabu, ndugu yangu mtani wango Dotto unayafahamu. Ndugu yangu Dotto wewe ni mtani wangu siyo ndugu yangu, pale kinachokosekana ni umeme tu, ukipeleka tu umeme utaongeza kiwango cha uchimbaji wa madini pale Londoni Makulu. Kwa hiyo ninaomba mtani wangu Mheshimiwa Dotto hebu nisaidie hili, wapelekee umeme wale wachimbaji wadogowadogo pale Londoni ili tuongeze uchimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho na la pili ni fursa ya madini ya chumvi. Leo nilipitia madukani nimekutana na chumvi inatoka India, nimekutana na chumvi inatoka Kenya, Mheshimiwa Halamga hapa ameeleza tuna-*deposit* za chumvi nyingi sana Tanzania, tuna kiwanda cha chumvi Kigoma, tuna kiwanda cha chumvi Tanga na Dar es Salaam. Tuna chumvi Lindi, Simiyu na Manyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Manyoni Mashariki kuna eneo linajulikana kama Kinangali na ile chumvi inajulikana kama chumvi ya Kinangali. Naibu Waziri ulishafika mwaka jana ninakushukuru sana, ulitembelea zile *site* zote tatu kuanzia Mahaka, Majiri, Kinangali na Mpandagani, ukaagiza Afisa Madini wa Mkoa wafanye utafiti, sasa mpaka sasa hivi taarifa ya utafiti siifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ipo katika maeneo makubwa mawili, kwanza mimi tangu nizaliwe natumia chumvi ya Kinangali mpaka leo hii hakuna uwekezaji wowote wa Serikali katika eneo la Kinangali! Sasa najiuliza kama mimi tangu nizaliwe sasa hivi nakimbilia miaka 50 natumia hiyo chumvi, *then* utaniambia kwamba chumvi hakuna pale Kinangali hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali watuambie Je, ni kwa kiwango gani ile chumvi ipo pale *in terms of quantity,* pili watuambie Je, ile chumvi ina ubora? Tatu watushauri sasa kwamba Je, tunaweza kuweka uwekezaji wa aina gani? Tunahitaji viwanda vya *size* ya kati, lakini viwanda vidogovidogo kwa ajili ya kuwasaidia ndugu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nirudie kumshukuru sana Waziri wa Madini.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chaya kabla haujahitimisha naona kuna taarifa hapa, kutoka kwa Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**TAARIFA**

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Chaya kwamba kuna uzembe mkubwa sana ufanyika kwenye uwekezaji wa chumvi, ukiangalia eneo la Bahari toka Lindi mpaka Tanga eneo hili lote lina chumvi lakini bado wawekezaji wanaruhusiwa kuingiza chumvi nchini kitu ambacho siyo sahihi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya unapokea taarifa.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa ya Mheshimiwa Cecil na labda kabla sijamalizia kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Cecil, sisi kama Nchi hatujawekeza vizuri kwenye fursa ya chumvi hususan katika eneo langu la Manyoni katika Kata ya Majiri hususan Kinangari. Nadhani ni fursa ambayo ingeweza kukuza ajira. Ile chumvi inachukuliwa na watu kutoka Congo, Rwanda na Burundi wanachukua kama *raw material* wanaenda ku-*process* wanai-*process* halafu wanaturudishia tunakuja kununua kwa bei ya jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Daktari Pius Stephen Chaya kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa wakati huo Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo na Daktari Ritta Enespher Kabati wanajiandaa.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii kwa kuchangia Wizara hii. Kwanza nianze moja kwa moja kuomba Serikali iwaangalie sana wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu hali ya ajira kwa kweli ni mbaya sana katika Taifa letu la Tanzania na kama wamejitolea kujiajiri wenyewe basi ni vizuri au ni vyema wakaangaliwa kwa jicho la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna maeneo ambayo wamechukua wawekezaji wakubwa ambayo yamekaa muda mrefu na hawajafanyia kazi yamekwisha rudishwa Serikalini. Sasa basi ni vyema Serikali ikaona ni jinsi gani ya kuangalia kuwagawia maeneo hayo wawekezaji wadogo wadogo ili na wao waweze kufaidi sungura katika Taifa lao la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ni vyema sasa yakaangaliwa maeneo yote ambayo wanachimba

wachimbaji wadogo wadogo wakafikishiwa umeme. Hili kwa kweli limekuwa ni tatizo kubwa sana na haswa Mkoani kwangu Mara Wilayani Bunda, Wilaya ya Musoma ya Vijijini, Wilaya ya Tarime, lakini na kote kule ambako kuna wachimbaji wadogo wadogo katika Taifa hili la Tanzania. Naamini kabisa umeme umekuwa ni tatizo kubwa sana na wao pia kwa sababu wanajisimamia ili kupata kipato basi ni vyema wakaangaliwa kwa jicho la ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri wetu Doto Biteko pale walipokuwa wasikivu walinikubalia tukaenda nao kwenye Mgodi wa *North* Mara Nyamongo tukaongea na wale wawekezaji na wale wawekezaji pia ni wasikivu. Kuna mara nyingine tunawapiga lakini kuna kipindi pia inabidi tuwapongeze pale wanapofanya vizuri. Kwa kweli wamejenga baadhi ya shule kwa mfano wamejenga Shule ya Julius Kambarage Nyerere wamejenga Shule ya Bulege wamejenga pia Sekondari Nyarokoba lakini pia wamejenga Ingwe Sekondari, wamejenga hosteli ambazo baadhi wamerekebisha majengo lakini pia wamejenga hosteli na baadhi ya vituo vya afya wametujengea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tuna jambo moja ambalo kidogo lina utata, kutokana na kwamba sisi Wanamara lakini pia Wanatarime kama ninavyokuwa naongea mara kwa mara lakini hata watu wote wanajua kwamba ametokea muasisi wa Taifa hili Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Katika mazingira hayo basi mkoa wetu unatakiwa uonekane mkoa wa mfano lakini mkoa wa kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo,wawekezaji wamekwishwa pata faida kubwa sana kutokana na Mgodi wa *North* Mara lakini pia kule Butiama ambako pia walimaliza na walipata faida za kutosha. Basi ni vyema wakatuwekea barabara wao kama wawekezaji sio wawe wanasubiri tu

Serikali itoe pesa ya barabara. Hata wao faida walizopata pia wanaweza kutuwekea basi barabara nzuri ya lami na sisi tukaoneka tukafanana fanana na dhahabu naamini kabisa bado hatujafanana na dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niende moja kwa moja kwa kuishauri Serikali kwenye hili suala la malipo ya wale wanaolipwa fidia. Haya malipo yametumia muda mrefu sana ni muda mrefu sana sasa Serikali ikiwa inavutana na wale ambao wametoa ardhi yao kwa ajili ya wawekezaji. Naamini kabisa Serikali imekwisha faidika na uwekezaji ambao umewekwa katika Mgodi wa Nyamongo (*North* Mara) ambako mwazo ilikuwa *Barrick* na sasa jina limebadilika limekuwa ni *North* Mara ambayo ipo ndani ya *Barrick*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira hayo sasa ni muda mrefu, toka mwaka 1995 ambapo wananchi wale walitoa ardhi yao kwa ajili ya wawekezaji. Naamini kabisa wamekwisha pata faida ya kutosha na bahati nzuri Dada yangu Mheshimiwa Angeline Mabula, Waziri wa Ardhi alitoa ufafanuzi hapa juzi lakini pia wanapaswa kuliangalia hili. Basi akae Waziri wa Madini, akae na Waziri wa Ardhi waliangalie hili, ili kusudi na wale wananchi pia waweze kumaliza tatizo hili, lakini Sheria ya Ardhi inasema mtu anapofanyiwa uthamini wa ardhi yake na ardhi ikarudi Serikalini baada ya miezi sita, ikivuka miezi sita alipe pia faida ya ile ardhi yake kwa sababu haitumii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tokea mwaka 1995 ni miaka 20 na zaidi. Naamini kabisa Serikali sikivu italifanya hili na kutokana na kwamba wananchi wa Tanzania sasa wana hali ngumu sana, huo ndio ukweli hali ni ngumu, vitu vimepanda bei, gharama ni kubwa wale watu wanajenga nyumba ambazo kwa kweli inakuwa thamani yake ni ndogo sana na wengine wanashindwa kumalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nimuombe Waziri atakapokuja hapa ku *wind up* atuelezee ni jinsi gani atafanya ili kusudi wale wananchi, kwa sababu sasa ni miaka mingi imepita wapewa riba yao. Katika ile pesa yao, katika ardhi yao ambayo waliitowa kwa ajili ya wawekezaji ambayo naamini kabisa tunapofanya tathmini au uthamini kwa ardhi inapokuja kwetu itakuwa ni fundisho pia ambalo watalipwa haraka wanaokuwa wameshafanyiwa uthamini kwa sababu sasa hili tatizo linatokea. Naamini kabisa sio tu mkoani kwangu Mara hata maeneo mengine ya Tanzania naamini hili tatizo limekuwa ni kubwa sana la kutolipwa mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niende moja kwa moja kwa kusema nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, unachapa kazi Mwenyezi Mungu akubariki sana kwa kweli unaweza na unaiweza Wizara Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio chetu kikubwa kwa Wanamara na Wanatarime tunaomba…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tulipwe pesa zetu za uthamini kwa sababu hadi sasa mashimo yamekwishwa kuwa makubwa sana, wawekezaji wamekwisha pata pesa nyingi sana. Hivyo tunaomba basi na sisi tulipwe ili kusudi na sisi tufaidi ile dhahabu yetu ambayo sisi wenzenu Tarime tulikuwa hatujui biashara ya kulima..

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, … na kilimo chetu sisi ilikuwa ni dhahabu sasa kama wametutoa kwenye dhahabu na sasa wanataka tulime au tufanye shughuli nyingine basi nafikiri ni vyema tukalipwa ili kusudi na sisi tufaidi. Tufaidi angalau kasungura ka Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na Mungu akubariki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Agnes Marwa kwa mchango wako. Namwita Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo aweze kuchangia.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii. Nianze kwa kuunga hoja kwa matumaini kwamba Wizara inaenda kubadilika. Ukweli ni kwamba ukisikiliza fedha, unaelezwa mabilioni kama huna uzoefu na hii sekta utaona ni fedha nyingi sana lakini niwaeleze ukweli ni kwamba Sekta ya Madini haijachangia ipasavyo na sababu ni hizi; Sekta ya Madini ingechangia ipasavyo ukuaji wetu wa uchumi unaopaswa kuondoa umaskini lazima ukue kwa asilimia nane mpaka kumi. Narudia tena ukiwa chini ya hapo hata ukifurahiaje hautautoa umaskini. Umaskini wetu lazima upungue utoke kwenye asilimia ishirini na mpaka kumi na tano na inayoweza kutupeleka huko ni sekta ya madini, gesi na vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mwaka toka 1961, miaka 60 iliyofuata mpaka 2021 ukitaka kukubaliana nayoyasema ni kwamba Sekta ya Madini muda mwingi imejishughulisha na utawala wa Sekta ya Madini *(Administration of the Mineral Sector)* na ndio maana madini yanayochimbwa ni hayo hayo yaani dhahabu, almasi, na

vito hasa *Tanzanite* na rubi. Ndio maana ya Liganga na Mchuchuma nitayaongea siku nyingine, wasingeshughulika na mambo ya utawala sana Chuma ya Liganga toka miaka ya 60 tungeshachimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uchumi wa dunia ya leo msemaji mmoja ameongea vizuri sana sijui kama walimuelewa Profesa Mkumbo ameongea vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa leo wa dunia *whether* wewe ni m-*socialist*, m–*Marxist* kwanza ni vitu vimepitwa na wakati havijadiliwi sasa hivi. Uchumi wa dunia sasa hivi unaoongoza ni wa aina mbili, ni private *wealth* yaani *capitalism* ya ubinafsi ambayo ndio nchi za magharibi na uchumi mwingine ambao umekuja kuibuka kwa nguvu sana ni *state capitalism*, nadhani ndio Profesa Mkumbo alikua anaongelea hiyo. Hii *state capitalism* inafanywa China imefanikiwa, India imefanikiwa, Brazili imefanikiwa, Norway inafanikiwa. Brazili ile kampuni ya *PetrolBras* ni ya Serikali, Norway kampuni tunayofanya nayo gesi ni ya Serikali hiyo ndio inaitwa *state capitalism*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sekta hii ya madini ni lazima itupeleke huko na ndio maana yule nilimsikiliza kwa makini ni lazima iwepo migodi inayomilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la hivyo hatutatoka tutakuwa tunadhani hizo bilioni ni hela nyingi lakini ni ndogo sana. Sasa kuanzia 2023 na kuendelea ndio maana nimesema naunga mkono nadhani tutakuja na *hybrid*. Tuchanganye hizi kampuni binafsi lakini za Serikali lazima ziwepo. Sasa ina maanisha kwamba Sekta ya Madini kuanzia sasa ijihusishe na uwekezaji, *development* na kufanya haya tunahitaji taasisi mbili muhimu sana, ya kwanza ni *geological survey*. Ni ajabu kwamba Tume ya Madini inapewa umuhimu bado ni makosa

yale yale ya kushughulika na mambo ya utawala wa madini badala ya kuwekeza *geological survey. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *geological survey* ni lazima tuwekeze ndio itatueleza tuna madini ya aina gani, kiasi gani ambayo tunataka kuendelea na utawala wa madini lakini *geological survey* haijawekezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara ya Madini sio lazima ione kwamba hii ni Wizara ya Elimu. Huko zamani tulivyokuwa chuo kikuu sisi, tulikuwa tunafanya kazi na *geological survey* kwa sababu ukitaka wataalam wengi wapo *UDOM*, wako Chuo Kikuu Dar es Salaam. Maabara zile lazima ziwezeshwe, haya madini mapya tunayoyaingia haya ninavyoelewa hatuna maabara zinazoweza kutusaidia hapa nchini. Kwa hiyo, mtaendelea kupokea ripoti kutoka nje ambazo nyie hamuwezi kuthibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna mapungufu makubwa sana na ndio maana tunaanzisha sheria hata hazijatumika tunakuja tunazibadili. Sheria moja ambayo ina mapungufu sana lakini mtu anaweza kushangilia akaifurahia ni hii mpya inayosema tunapata hisa asilimia 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanaonisikiliza hili ni kosa kubwa tunalolifanya. Asilimia 16 hiyo tunaweza tusipate kitu kwa sababu moja hivi. Hatuko kwenye bodi inayofanya maamuzi, kwenye menejimenti ya juu haupo, haujui unazalisha kiasi gani, haujui unauza kiasi gani, wewe umekaa pembeni unasubiri tu uletewe fedha eti una hisa asilimia 16. Maana ya kuwa mwanahisa ni kwamba ni lazima ushirikiane na mwenzako kuwekeza, kwenye faida mshirikiane na lazima mshirikiane nae kwenye hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa cha kujifunza Watanzania na naomba hii Wizara iende pale Mwadui, mwingine alitaja

Mwadui ichukue ripoti ya Marehemu Ally Nuhu Kassim. Kassim alikuwa anafanya kazi nchi za nje akaomba nafasi amepata cheo kwenye *UN* lakini mwalimu akamrudisha mwaka 69 akampeleka pale Mwadui. Msomi mzuri wa Uingereza akamwambia hebu tunataka kutaifisha hebu angalia Mwadui inavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alitoa ripoti ambayo kwa kifupi inasema kwamba hawaelewi nini kilikuwa kinaendelea pale Mwadui. Watanzania hawaelewi, kwa hiyo, Mwadui tulianza na *shares* 50 kwa 50. Tumekwenda *De Beers* ilivyokuja kuchukua, *De Beers* ikachukua 50 kwa 50 wakasema wanajenga *plant* mpya nzuri ya kisasa Tanzania, mwenzetu changia hela, sisi hatuna tutaelewana huko huko. Wewe leta tu *plant* wakasema sawa wakaleta *plant shares* zetu zikashuka kutoka 50 zikabaki 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui kama Mwadui kama Tanzania kama bado ina *share* kama Serikali. Kwa hiyo, hii asilimia 16 ndugu zangu Waheshimiwa nawaambia ni kosa ambalo lazima tulirekebishe kwa sababu hatuna nazo *control*. Huenda hata tusipate kitu, au tukipata inakuwa kidogo sana. Kingine ambacho tunahitaji umakini mkubwa na Wizara ifanye ni madini mapya na leseni wanazotoa. Nitawatolea mfano hapa, leseni zimeshatolewa za *PGM* (*Platinum Group Metals)*. Je, tunajua huko wanaenda kuchimba nini? Maana yake *PGM* hii *group* ina madini kama saba na yote yana thamani ndio kuna *platinum*, kuna *palladium* kuna nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nawapa mfano mmoja hapa kwenye hii *group*, kuna madini yanaitwa *rhodium*, wakati dhahabu ilikuwa ni dola 1,850 kwa *ounce*, *rhodium* ilikuwa ni dola 10,300 kwa *ounce*. Je, sisi tunajua hawa tuliowapa leseni watayachimba hayo? Unakuja kwenye *rare earth elements* wanasema madini ya mkakati, je ni ya mkakati kwako au ni ya mkakati kwa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii *rare earth element* kama mtu haielewi anaiongea tu kwa mzaha mzaha ni madini 17, *element* 17 ziko kwenye hii *group* na zote zina thamani kubwa ndio hayo Marekani wanaita ya kimkakati, Ujerumani, Japan. Sasa katika haya madini yapo matatu makubwa kabisa, lutetium, lanthanum, scandium. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue moja nieleze, lutetium inatumika kwenye *X-Ray* hata kwenye *treatment* ya kansa. *Treatment* ya kansa ikiwa na haya madini ambayo yanaitwa *177 PSMA*, kozi moja ni dola 10,000 na *treatment* inataka kozi moja mpaka nne. Kwa hiyo, ni *between 30 and 40 thousand US Dollars*. Ndio maana wanasema haya madini ukitaka kuyanunua unaweza ukaingia kwenye mabilioni ya dola. Je, leseni tunazozitoa za *rare earth elements* tunajua ni madini gani tumewaambia wachimbe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana badala ya kuwekeza hela nyingi sana kwenye Tume, mimi ningewekeza *geological survey* na kwenye taasisi zetu za *geology*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna madini mengine la mfano ni *scandium* inatumika kwenye *aerospace*, kwenye *mid fighters* hasa za Warusi hata wanaocheza *golf* wanaitumia hii. Yenyewe *kilogram* moja ni dola 3,912 na duniani kwa mwaka zinahitajika tani kati ya 15 na 20 *tons* mwaka mzima. Haya yako kweye *rare earth elements*. Je, tunajua leseni tunazozitoa? Je, tunajua hiyo 16% tuliyopewa ya bure tunaijua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije *topic* nyingine ambayo nimeiongelea kwa muda leo naichukua kwa njia nyingine na ninashukuru Wabunge nao wameongelea suala la kuwa na *reserve* ya dhahabu *(gold reserve)*. Niliongea leo sitarudia ila nachukua *angle* nyingine ya kuwapa taarifa wale ambao bado wanasita sita kwamba kwa nini unahitaji kuwa na *gold reserve?* Kwa hiyo, nimeenda kwa wale wanaotukopesha,

nimeenda kwenye *World Bank* nikaangalia hisa za *World Bank* ambazo zinaendana na *voting powers.* Yaani unavyozidi kuwa na hisa nyingi ndivyo ambavyo kura yako inazidi kuwa nzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *World Bank* nimechukua tatu. Marekani *voting powers* za Marekani ni *around* 17%. Japan ni *around* 8.55%. China ni 2.25%. Sasa angalia Marekani mwenye *voting power* kubwa kwenye *World Bank* ana dhahabu *reserve* tani 8,133 *tons gold reserve*. Huyu Japan anayo *vote* kwenye hii *IDA (International Development Association) World Bank* ina mikopo ya aina mbili. Hii *IDA* ndiyo yetu ya sisi masikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko huyu Japan yeye *voting powers* zake 8.55% ana *reserve* kwenye Benki yake ya Taifa tani 846. China ana *voting power* ya 2.25% ana *reserve* ya dhahabu tani 1,948. Wewe Tanzania kwa nini bado una sita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Madini na Benki Kuu kwa nini bado mnasita? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana *Professor*.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia sasa. Nimalizie kwa kusema kwamba lazima tuwe na hiyo na kuwa na hiyo ni lazima *refineries* zetu mbili zifanye kazi. Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba *refinery* mbili za dhahabu tulizonazo ya Geita inaweza ika-*process kilogram* 600 kwa siku ya Mwanza 480 kwa siku. Lakini Waheshimiwa Wabunge hizi *refineries* hazina dhahabu na huenda zitafungwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzji)*

**MWENYEKITI:** Haya tunakushukuru sana *Professor* Sospeter Muhongo kwa mchango wako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nilimwita Mheshimiwa Ritta Kabati wakati huo Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu anajiandaa.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini vile vile nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata hii nafasi ya kuchangia saa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa leo ni siku ya Mwanamke wa Bunge naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Spika wetu wa Bunge ambaye ni mwanamke namba moja kwa kazi nzuri sana ambazo amekuwa akizifanya hapa Bungeni, lakini vile vile hata katika Jimbo lake hata kwa tuzo nyingi ambazo amekuwa akizipata kwa kweli anastahili. Tunampongeza sana sana sisi wanawake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pongezi zangu nyingi sana kwa Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwa kweli Wizara hii ya ameitendea haki. Ameitendea haki kwa sababu amekumbuka hata wanawake wachimba madini. Tunamshukuru pia tumeweza kutembelea wanawake wengi sana wachimba madini, wengi wanamshukuru. Kuna fursa nyingi sana sasa hivi wana hamu hata ya kuchimba madini kwa ajili yake. Mwenyezi Mungu ambariki sana Doto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumpongeze Naibu Waziri Dkt. Kiruswa na yeye amekuwa msaada sana katika hii Wizara na kuhakikisha kwamba inakwenda vizuri. Nimpongeze pia Katibu Mkuu wa Wizara kaka yetu Heri anafanya kazi nzuri sana pamoja na watendaji wote wa

Wizara hii ya Madini niombe wachukue, niwapongeze pia Kamati ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kupongeza Wizara hii kwanza kwa kuweza kuongeza pato la Taifa kutoka walikuwa wana 7.8% mwaka 1921 na sasa hivi wamefikisha *point* tisa *point* saba mwaka 2022. Mheshimiwa Rais wetu aliwawekea lengo kwamba wafikishe angalau 10% na unaona sasa hivi wana 0.3% tu na ninaimani kabisa kutokana na kazi yao nzuri watavuka lengo kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Iringa pia na sisi tuna Mgodi unaitwa Nyakavangala. Huu Mgodi uko katika Jimbo la Isimani nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri ulikuja Nyakavangala tulipouliza maswali hapa Bungeni na ukakutana na wawekezaji wa Nyakavangala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru kwamba ulikuja kuona kulikuwa kuna changamoto nyingi sana na bado zipo vilevile. Ulikuwa umeagiza *GST* wawasaidie ule mgodi lakini toka ulivyotoka bado hawajaenda kufanya kitu chochote. Kwa hiyo, tunakuomba endelea kuwahimiza waende ili hawa *GST* wakasaidie huu mgodi na sisi tuweze kupata wawekezaji pia lakini waweze kupatiwa fedha ili nasisi tuwe kama, tupate wawekezaji kama *GGM* ili na sisi Wanairinga tuweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Iringa wapo wachimbaji wadogo wadogo. Kwa mfano Mwenyekiti kule kwake kule Mufindi wananchi wanachimba wadogo wadogo lakini hawajapimiwa wanachimba tu bila kujua kwamba wanatakiwa wafanyaje. Kwa hiyo, tunaomba sasa Wizara hii *GST* waje wapime katika Mkoa wetu wote wa Iringa ili wachimbaji wadogo wajue maeneo halisi ya uchimbaji ili kinamama, vijana, na Wanayalukolo wote wa Iringa waweze

pia kujiajiri kupitia madini na pia tuongeze pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana *STAMICO*, nimpongeze Mtendaji Mkuu wa *STAMICO* na Bodi nzima kwa sababu *STAMICO* zamani tulikuwa tunajua ni shirika ambalo linaweza likafa wakati wowote lakini sasa hivi huu uongozi umefanya tunaona *STAMICO* sasa inafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona wameweza kubuni miradi ya kupunguza hata uharibifu wa mazingira kwenye migodi nchini lakini pia kuna mradi ule wa kuongeza kipato mkaa wa mawe wameendelea kuingia ubia kazi ya uchorongaji pamoja na *GGM* na tulishuhudia siku ile tulivyokuja Geita wameingia Mkataba wa karibu shilingi bilioni 52.2 kwa hiyo, ni kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *STAMICO* wamekuwa mara nyingi sana wakiwasaidia watu wenye ulemavu vifaa vya uchimbaji. Tunawapongeza sana. Tunaomba pia hata wako, hawa tunaona watu wenye ulemavu wanaume lakini wako pia watoto wa kike pia wako wana kikundi chao, tunaomba pia muwasaidieni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mara nyingi wamekuwa wakiwasaidia pia hata wanawake wachimbaji. Tunaomba muendelee sasa kulea wanawake wachimbaji nchini kwa sababu wameonyesha mwamko mkubwa sana na muweke kabisa jicho la kipekee ili kuwapatia sasa utaalam maana yake ndiyo vitu ambavyo wanavikosa; utaalam na vifaa vya uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunashukuru hata Mheshimiwa Waziri alikiri kuwa wanawake wengi ambao wameingia kwenye mambo ya uchimbaji wamekuwa

wakilipa vizuri kodi na mapato na kwa uaminifu sana kwa hiyo tunazidi kuwapongeza wanawake wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuwapongeza wanawake wote wachimba madini nchini. Kupitia Chama chao cha *TAOMA* tumeweza kubaini changamoto nyingi sana baada ya kukutana na chama hiki cha wachimba madini nchini pamoja na wanawake wanaochimba madini. Kwanza kabisa hawana mitaji ya kutosha katika kuweza kuchimba haya madini lakini vilevile tunaona kwamba vifaa, hawana vifaa kabisa vya kuchimbia na uchenjuaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi hawakopesheki kabisa kwa sababu hawana dhamana za kuweka. Kwa hiyo sasa naomba sasa mabenki wawakopeshe basi hawa wanawake wachimba madini. Tunawaomba *STAMICO* kwa sababu wao ni walezi basi watoe dhamana wawadhamini hawa wanawake waweze kukopesheka ili wachime kwa urahisi na waweze kufanya kazi yao vizuri kwa sababu kina mama wengi zamani walikuwa wanakuwa tu mama lishe, hawafanyi kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba tumpongeze Mwanamke mwenzetu ambaye yeye amekuwa mwekezaji wa Mgodi wa *GGR* pale Geita. Kwa kweli na amekubali pia kuwa mlezi wa wachimbaji wanawake wadogo wadogo nchini Dada yetu Sarah Masasi, tunampongeza sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaomba sasa Wizara iweke mkakati wa kuwasaidia Watanzania waliowekeza katika hizi *refinery* ili wapate malighafi kwa sababu changamoto pia wamewekeza, wameweka fedha zao nyingi wamekopa benki lakini unakuta malighafi za kwenda kwenye hizi *refineries* hakuna. Kwa hiyo, kuwepo na mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba malighafi inakwenda

pale ili wathaminishe hizi dhahabu kabla hazijapelekwa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nikushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwashukuru na Wabunge wenzangu wote na pia nishukuru wanawake wote kwa sababu leo ni siku yetu basi tunawashukuru pia Uongozi wa Bunge kwa kuona umuhimu na sisi wanawake tuwe na usiku wetu na Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Ritta Kabati, sasa namwita Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara aweze kuchangia.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia kwa kazi nzuri ambayo anafanya kwa ujumla wake lakini pia kwa kuchukua hatua na kutoa maelekezo kwa Waziri wa Madini Dkt. Biteko na wenzake kutanzua mgogoro mkubwa ambao ulikuwa pale Tarime wa mambo ya miradi ya CSR. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa sasa kwa kweli siyo kama hali ilivyokuwa hapo awali, kuna mabadiliko makubwa sana katika miradi hii ya *CSR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana niseme tu kwamba ule Mgodi unaitwa *Barrick North Mara* na mgodi huo ume-*take over* kutoka *Acacia* tangu mwaka 1995/1996. Kwa hiyo, ilirithi madeni pamoja na mkataba na uchimbaji na kila kitu. Kile ambacho wananchi walikuwa wanadai kutoka nyuma maana yake *Barrick* kwa sasa wanawajibika kulipa kwa sababu ilikuwa kwenye mkataba na walikubaliana. Nilitaka niweke maelezo *very clear. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaipongeza *Barrick* pamoja na mvutano ambao ulikuwepo tangu nimekuwa Mbunge katika jimbo lile 2020 mpaka leo kuna mabadiliko makubwa sana. *Barrick* zile ajira 46% wanatoa katika vijiji 11

pale pale kwenye Mgodi wa *Barrick North Mara*. Vilevile hata bidhaa ilikuwa inatoka nje ya hata ya nchi. 80% ya bidhaa pale mgodini inatoka ndani ya nchi na wengi akina mama na vijana wana-*supply* katika Mgodi wa *Barrick North Mara*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile walikuwa wanamsikia Rais wa *Barrick*, leo navyozungumza anakaa na wale wananchi wanazungumza na viongozi wa vijiji wanapanga mipango pale mtaani kabisa katika jengo la sekondari na wanazungumza na wanapeleka maombi kadhaa ambayo mgodi umepokea na wanaendelea kuyafanyia kazi. Hayo ni maendeleo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwenye miradi ya *CSR* kuna mambo mawili hapa; la kwanza kuna fedha ya kwanza ambayo ilienda *Barrick* wameweza kutoa fedha mara mbili tu. Mara ya kwanza ni mwaka 2019/2020 wakati huo nilikuwa Mbunge wa Ukonga. Katika fedha hiyo ililipwa shilingi bilioni 5.7. Nimelalamika hapa Bungeni na ningeomba Mheshimiwa Waziri hili jambo la miradi ambayo fedha ilipelekwa kwenye miradi mbalimbali. Miradi mingi imekuwa viporo, nondo zimekuwa *stranded*, ma-*cement* yameharibika mpaka leo. Ripoti ya *CAG* haijatoa taarifa nani mhusika, hiki kitendo kimekwaza Wananchi wa Tarime na kama Mbunge sifurahii. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri asimamie jambo hili ile ripoti itoke fedha hazikutumika vizuri miradi haikukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya awamu ya pili ambayo tumepokea mwaka jana yaani 2022/2023 navyozungumza shilingi bilioni 7.3 ipo kwenye miradi mbalimbali ya Halmashauri ya Tarime Vijijini na tumebadilisha utaratibu, hii miradi ipo kwenye kata 26. Mheshimiwa Naibu Waziri amekuja tulizungumza vikao mbalimbali tunamshukuru mabadiliko ni makubwa sana. Kilichotokea kwamba fedha hii Kamati ya TAMISEMI ambayo ni mjumbe ilikwenda pale ni

kwamba kwa kuwa kuna changamoto nyingi hakuna madawati, hakuna visima vya maji, hakuna zahanati, watoto wanakaa chini. Kwa hiyo, tulikubaliana kwamba fedha ile ukiipeleka kwenye kata, Diwani wa kata husika kupitia *WDC* wanaangalia wenye kipaumbele ni kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini baada ya *batch* hii kwenda tumejenga madarasa ya kutosha, tukaweka madawati, tukachimba visima, tukajenga majengo ya mama na mtoto, tukapeleka hata vitanda tu vya kina mama kujifungulia, ina maana awamu nyingine ijayo tunaenda kuteua miradi ya kimkakati ambayo sasa itaonekana kwa macho na kwa sababu *Barrick* wamekubaliana kuwachukua baadhi ya viongozi kutoka Nyamongo, kutoka katika Halmashauri yetu ya Tarime *DC* wataenda kujifunza wenzetu wa Msalala kazi ambayo imefanyika na pale Kahama. Tunaamini kwamba tunaendelea vizuri kwa maana ya Mgodi wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wameahidi kujenga uwanja wa mpira pale, wana-*supply* maji katika vijiji 11 kwenye kata tano kutoka kwenye chanzo chao ili kuondoa sintofahamu kwamba maji yale ni ya sumu walikuwa hawawezi kuyaamini kuyatumia lakini Mheshimiwa Waziri yako mambo ya Wizara kufanya katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano amezungumza mwenzangu kwamba kuna watu wana dai. Kule kulikuwa na vijiji vitano ambavyo viliingia mkataba na Mgodi wa *Barrick* kutoka *Acacia* kwamba katika uzalishaji watapata 1%. Hiyo fedha mara ya mwisho wamelipwa mwaka 2012. Mpaka leo fedha haijwahi kulipwa, ni mgogoro mkubwa kwa sababu kila wakikutana wanajadiliana walipwe fedha zao. Hili ni Wizara isimamie lipo kwenye mkataba na hiyo fedha walilipwa dola milioni mbili mpaka walienda mahakamani na jalada lipo. Waliambiwa msiende mahakamani, msigombane

na mgodi mulipwe fedha. Kwa hiyo, naomba jambo hili litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ile ikienda kuna wananchi wanadai maduara 360 mpaka leo. Wamezunguka sana wamesaga lami. Wameenda kila mahali mpaka kwa Rais na Mheshimiwa Naibu Waziri ulikuja pale. Kama vijiji vile vitano vikilipwa 1% ndiyo watalipwa wenye maduara. Hawawezi wenye maduara yakalipwa fedha ambayo haifiki. Kwa hiyo, kama kweli tunataka kuwasaidia wale watu.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita kuna taarifa?

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa muongeaji taarifa kwamba tena kati ya hao ambao hawajalipwa mpaka sasa hivi kuna baadhi yao wengi wao wamekwisha fariki. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita unapokea taarifa?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni wengi wamefariki dunia na wameacha haki zao zinapotea. Kwa hiyo, nasema kwamba wale watu wakilipwa vijiji vile vitano vikilipwa 1%, watafanya miradi ya maendeleo lakini watu wa maduara watalipwa lakini kwa sasa ilivyo wale watu wanagombana wenye maduara ndiyo fedha yao kwa sababu waliwekeza hawajalipwa, vijiji vinasema hatuwezi kulipa kwa sababu hatujalipwa. Mgodi unasema kwamba wao hawajaendeleza maeneo yale, kama hawajaendeleza maeneo warudishe kwenye vijiji, vijiji vitafute muwekezaji mwingine watachimba ili kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine ambalo nataka niseme hapa. Kuna mgogoro mkubwa katika eneo langu na

hili jambo mlisikilize vizuri. Mgogoro uliopo ni kwamba mgodi unafanya *evaluation* ya kutoa maeneo ya watu. Tuna maeneo kama Nyamichere tangu mwaka 2012 maeneo kama Murwambe yamekuwa mabovu majengo ya watu, maeneo kama Kewanja, Komalela, Nyabichune. Hapa tunazungumza kata tano zinazozunguka ule mgodi. Watu hawa wamefanyiwa tathmini lakini mpaka leo hawajalipwa. Sasa kuna ugomvi pale, ukienda kwenye mgodi wanasema sisi tunalipa tulichoambiwa tulipe, mdhamini mkuu yupo Wizara ya Ardhi kwa Mheshimiwa Angeline Mabula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanavutana, ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Madini usimame katikati. Kitendo cha watu wale kutolipwa fedha zao na tena wanalipwa kiasi kidogo, ekari moja ya ardhi ambayo ina dhahabu chini wanalipwa shilingi milioni tano tu. Ndiyo maana umasikini hauwezi kwisha, unachukua ardhi, ulipe shilingi milioni tano aende atafute eneo lingine ajenge, aanze kuwekeza, na ana familia kubwa, *extended family* pale. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili jambo limeleta taharuki. Kuna ugomvi ambao siyo wa lazima. Kama Wizara ya Ardhi itafanya tathmini vizuri, ikapandisha bei ya ardhi, ikafanya tathmini kwa wakati, mgodi wanasema tukiambiwa na Serikali lipa shilingi milini 10 tutalipa. Tumeambiwa tulipe shilingi milioni tano ndiyo tulichoambiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba mtanzue huu mgogoro ili wale watu wafanye kazi ya uwekezaji wapate ushirikiano na wananchi wale, wafanye kazi nzuri. Mgodi wa Barrick ndiyo walipaji wakubwa wa kodi kuliko migodi yote hapa Tanzania. Lakini malalamiko ni mengi kwa sababu wale watu wanatambua haki zao. Wanajua chini ya

ardhi kuna dhahabu, kuna matrilioni lakini hizo fedha hazilipwi zinalipwa kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mgogoro ule kati ya *Barrick* na wananchi niutanzue, na hii ni kwa Wizara ya Madini na Wizara ya Ardhi kufanya kazi pamoja ili watatue jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine, migogoro mingi iliyopo katika maeneo yetu ni kwa sababu kwa kweli ukiangalia hali za watu katika maeneo ya migodi, ikiwepo Nyamongo, hasa wale wananchi wa kawaida maisha yao hayafanani. Sasa hivi Nyamongo imechangamka sana, mgodi umetengeneza mahusiano, umewekeza, watu wamepata kazi, lakini wengi ni wageni ambao wamekaa pale. Wananchi wa kawaida wenye ardhi wanalipwa kidogo sana. Kwa hiyo ningeomba jambo hili Mheshimiwa Dotto Biteko…

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:**…umesifiwa sana kwa kuwawezesha wachimbaji wadogo kuendesha maisha yao. Sasa njoo Nyamongo nenda maeneo ya machimbo, wezesha wananchi wa kawaida, wale wanaozunguka migodi wapate maisha mazuri, wafanane. Ametuleza Mheshimiwa Salome Makamba, ni kweli kwamba ukimlipa fedha kidogo…

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** … anaenda kuanza maisha, lakini akipata hisa, akapata *share* kidogo maana yake atakula yeye na kizazi chake na ndugu zake na mahusiano

yataimarika. Vilvile nikiangalia bei ya mazao na bei ya ardhi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara muda wako umekwisha nakuongeza dakika moja nyingine malizia hoja yako.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru sana, niombe Mheshimiwa Waziri wa Madini ufanye tathmini nzuri sana…

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:**…, je wananchi wale ambao wanalipwa fedha wanaboreshewa maisha au fedha inapita mlango mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nilitaka nikuombe, fanya tathmini, uchunguzi wa kimadini ya Locoba, Kuihanchat, Koronga, Nanungu na Hifadhi ya Serengeti. Migogoro mingi iliyopo pale watu wanaamini pale kuna dhahabu na inafichwa haijulikani. Nenda ufanye uchunguzi mtangaze kuna dhahabu ufanyike uchimbaji halali ili kuondoa migogoro iliyopo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba niunge mkono Bajeti ya Mheshimiwa Dotto Biteko ameiheshimisha amekuja na mambo wakati wa shida, watu wanakusikiliza lakini lile Bwawa la Nyamongo la maji machafu Mheshimiwa Rais aliagiza akiwa Makamu wa Rais kwamba lichimbwe jipya mpaka leo halijachimbwa, tunaomba utekelezaji, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara. Nilimwita Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, wakati huo Mheshimiwa Naibu Waziri unajiandaa.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi leo kuchangia Mpango huu wa Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoweza kuisimamia Serikali vizuri na maendeleo yanakimbia kweli kweli. Pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Madini pamoja na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwanza kabisa mimi naomba uelekee kwenye eneo moja, ambalo Serikali kwa sasa imeweka zuio ama inaweka zuio la matumizi ya kemikali aina ya *mercury* ama zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaweka zuio la kutumia *mercury* na badala yake wanataka kuruhusu matumizi ya kemikali aina ya *cyanide* ndiyo itumike mbdala wa zebaki. Sasa mimi naomba niishauri Serikali kupitia Wizara ya Madini; na niliwahi kuuliza swali hapa namna ya usalama wa watumiaji wa kemikali ile ya *cyanide* usalama wao utakuwaje, na nilijibiwa na Wizara ya Afya badala ya kujibiwa na Wizara ya Madini. Kwa sababu, matumizi makubwa ya *Mercury* yanatumiwa na wachimbaji wadogo wadogo si Wizara ya Afya, si na watabibu; watabibu ni asilimia ndogo sana; lakini kwa upande wa wachimbaji wanategemea sana matumizi ya mercury, tena hasa wachimbaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachomaanisha mimi ni kwamba kemikali aina ya *cyanide* ni hatari sana kwa matumizi ya binadamu. Kwanza kabisa namna ya upatikanaji wake ni gharama kubwa mno kuipata, kwa sababu ili uweze kuagiza lazima uwe na kibali maalum na kibali kile unalipia fedha nyingi kweli kweli ambapo mchimbaji mdogo hawezi kumudu hiyo gharama ya kulipia hicho kibali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni namna ya kuweza kuitumia ama kui-*handle* inahitaji utaalam wa kutosha mno. Ndipo najiuliza, je, Serikali imetoa elimu kwa kiasi gani kwa wachimbaji wadogo wadogo ili kuweza kuitumia ile kemikali hatari ili isiweze kuleta madhara? Kwa sababu ukiangalia madhara ya *mercury* na madhara ya *cyanide, mercury* ina madhara madogo sana, katika asilimia 100 labda ni asilimia 10 tu lakini *cyanide* madhara yake ni makubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *cyanide* ni hatari; kwa nini nasema hivyo? kama mtu yoyote anaweza kuweka kijiko kimoja cha *cyanide* kwenye maji ama kwenye mto wa maji ambayo yanatiririka basi maji yale mtu yeyote atakayeweza kuoga, akitoka hapo anakuwa ni mwekundu si mweupe tena, hata kama akiwa mweusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama bahati mbaya tone moja la maji lenye *cyanide* binadamu yoyote akaliweka mdomoni basi huyo tunamzika kwa dakika mbili tu, madhara yake ni hatari kweli kweli kuliko *mercury*. Mercury tumeitumia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mchimbaji, nafahamu na nimeitumia sana *mercury. Mercury* tumeitumia kwa muda mrefu sana, kwa miaka mingi, tunaona madhara yake ni machache na ni madogo sana kuliko *cyanide*. Lakini achilia mbali ya mdhara yanayopatikana ni kwamba sasa upatikanaji wa hiyo *cyanide* ni mgumu na ni mdogo ukilinganisha; wachimbaji wadogo wadogo wametapakaa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiidhinisha matumizi ya *cyanide* maana yake watakaokuwa na uwezo wa kuleta ile *cyanide* na kuitumia ni kampuni kubwa tu. Yaani tunazungumiza Barrick Geita huko na maeneo mengine. Lakini Ukienda kule Tunduru, Ruangwa na maeneo mengine hawana uwezo wa kuagiza *cyanide* na kuitumia. Lakini hasa

zaidi wachimbaji hawa hawana kabisa elimu ya hiyo kemikali ya *cyanide*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU: …**Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili nataka kuzungumzia suala la…

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi, Mheshimiwa Matiko, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nataka nimpe taarifa mzungumzaji ameeleza vyema kwamba *cyanide* ni gharama kubwa lakini pia ina madhara. Lakini *mercury* ameeleza ina madhara kidogo kulinganisha na *cyanide,* lakini kwa sasa hivi inavyosemekana na nilishauliza swali hapa Bungeni bado wachimbaji wadogo wadogo wanaona *mercury* ni bei ghali zaidi. Pia inasemekana wanatumia mbolea, hizi mbolea ambazo tunatumia kwenye kilimo wanazitumia sasa hivi kusafishia madini. Nataka nimpe taarifa anavyochangia aendelee kuishauri Serikali wafanye tafiti ya kina kama kweli mbolea zinaweza kutumika na tukajua hazina madhara ziweze kutumika kwenye madini pia tuachane na *cyanide*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kungu unapokea taarifa.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa lakini kwa maelezo yafuatayo. Nilipokuwa nasema zebaki kwa maana ya *mercury* gharama yake ni ndogo yaani mchimbaji anao uwezo wa kununua *mercury*

kwa shilingi 10,000 tena mpaka shilingi 5,000 akaenda kukamatisha dhahabu yake na ina uwezo wa kukamata 0.1 ikashika kulikoni na *cyanide*. Sasa *cyanide* kuinunua kibali tu peke yake si chini ya milioni 30 ni kibali tu hapo, hujainunua bado. Sasa najiuliza hawa wachimbaji wadogo wadogo watawezaje kumudu gharama za *cyanide*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nashauri…

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi, Mheshimiwa Hussein Amar.

**TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji anapozungumzia kwamba madhara ya *cyanide* pamoja na *mercury* kwamba *mercury* haina madhara. *Mercury* ina madhara makubwa na matumizi ya *mercury* na *cyanide* ni vitu viwili tofauti. *Cyanide* inatumika kwenye makinikia lakini *mercury* kwenye unga *fresh*. Lazima aeleze vizuri asilete tishio la kusema kwamba *cyanide* ni mbaya, *cyanide* tunaitumia na mimi nimeshaitumia zaidi ya miaka ishirini, nipo kwenye hiyo fani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kungu unapokea taarifa.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hii taarifa lakini nadhani mtoa taarifa hajanielewa vizuri nini namaanisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napozungumzia madhara makubwa kati ya zebaki na *cyanide* lazima nieleweke. *Cyanide* kwanza utunzaji wake ni wa hali ya gharama kubwa ukilinganisha na *mercury*. *Mercury* hata mimi leo naweza

nikawa nayo hapa nikakaa nayo nikaenda nayo popote bila shida yoyote lakini *cyanide* siwezi hata kuigusa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wale ambao wanaitumia, wanatumia kwa vifaa maalum, tena kwa uangalizi mkubwa, watu wa usalama lazima wawepo. Sasa, je, yule mchimbaji ambaye hayuko kwenye kampuni atawezaje kutafuta dhahabu yake ya *point* mbili, tatu na atapataje uwezo wa kuipata hiyo *cyanide*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima …

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MWITA. M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kungu utaendelea kuchangia mpaka leo Spika atakapotoa maelekezo mengine.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba niendelee na mchango wangu. Mimi nimeona matumizi ya *cyanide* na mimi nimetumia *mercury* kwa muda mrefu sana. Leo hii unaweza kuweka *mercury* ndani ya ndoo ya maji ya kuoga kwa bahati mbaya ukaoga na usipate madhara, lakini leo hii ukiweka tone moja tu la *cyanide* kwenye ndoo ya kuoga hata ukitumbukiza tu mkono usioge mwili mzima mkono huo unakuwa sio mkono wako tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ninachomaanisha? Nachomaanisha ni kwamba kabla ya kuidhinisha matumizi haya *cyanide* Serikali kwanza iende ikatoe elimu ya kutosha, kwa wachimbaji wadogo wadogo waelewe namna ya kuitumia, waelewe madhara yake, pia waelewe namna ya kujikinga na madhara yatakayotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara ya *cyanide* ni hatari tena kwa muda mfupi sana. Naomba nihame eneo hilo niende…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kungu na muda wako umekwisha.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba nisome tangazo la wageni. Wako wageni 38 wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu (Mb), ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Tawi la Mkwawa Iringa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeno wa Mheshimiwa Abeid Ighondo ambaye ni Katibu wa CCM kutoka Singida kaskazini Ndugu Joseph Hongoa, karibu sana katibu wa chama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Deus Sangu ambaye ni mtafiti wa gesi ya Hellium kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Josepho Uiso.

Tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 297 kutoka Taasisi ya Umoja wa Amani Kwanza wakitokea mikoa mbalimbali ya Tanzania. Karibuni sana wageni wetu kutoka Taasisi ya Umoja wa Amani Kwanza ambao tumeelezwa mnatoka nchi nzima. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna wanafunzi 32 wanaosoma kozi ya Takwimu na Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ahsante karibuni sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Madini, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Madini, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika kuboresha maisha ya wananchi na pia utayari wetu wa Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafaninikio ya sekta ya madini, Serikali inashauriwa kuchukua hatua za kuimarisha zaidi sekta hii muhimu ili kukabiliana na athari za kiuchumi kutokana *COVID-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine. Kutokana na athari ya kiuchumi iliyoikumba dunia nzima, hii inaweza kuwa fursa kwa Serikali kuvutia uwekezaji zaidi kwenye madini hasa dhahabu, madini ya chuma na madini ya *calcium carbonate, lime* na *phosphate*. Dhahabu ina historia ya bei kutoyumba kwenye soko la dunia kwa vile mabenki yanatumia dhahabu kwenye kuwekeza na kutokana pia na kuyumba kwa thamani ya shillingi na hata

dola ya Marekani, Serikali inaweza kutumia dhahabu kama mbadala wa kuwekeza amana zake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya kiuchumi kidunia, Benki Kuu nyingi duniani zimeanza kuwekeza zaidi kwenye dhahabu na hii ni ishara nzuri kwa bei ya dhahabu kuendelea kuimarika kwenye soko la dunia ambapo kwa mwezi Aprili, 2023 bei imepanda kwa zaidi ya asilimia 11 ukilinganisha na bei za Desemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, vita vya Urusi na Ukraine vimesabisha upungufu mkubwa wa uzalishaji wa mbolea, na hii ni fursa kwa Serikali kuwekeza kwenye viwanda vya mbolea kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini kama vile *phosphates, calcium carbonate, limestone* na *natural gas.* Katika kipindi cha mtikisiko wa uchumi, bei ya madini ya chuma na hata makaa ya mawe haiyumbi na Serikali inaweza kupata mapato mengi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kuchukua hatua za makusudi na kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa chuma *(Liganga Iron Ore)* ikiwa ni pamoja na makaa ya mawe *(The Mchuchuma Coal Mining and Power Projects)*. Mradi wa Liganga na Mchuchuma ulitarajia uwekezaji wa *US$ 3 billion* na kuzalisha ajira zaidi ya 30,000 na hii inaweza kuwa fursa nzuri katika hiki kipindi cha balaa la athari za *COVID-19* na vita vya Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya *Niobium* ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha *Ferroniobium (FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,* kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji,

Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapa kwetu. Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya *Niobium* ambayo inapatikana Milima ya Pandahill Wilaya ya Mbeya, na mahitaji ya *Ferroniobium (FeNb end product)* yanaendelea kuwa makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahitaji kujiwekekea mikakati ya haraka *(quick wins)* ili kuhakikisha inaimarisha uchumi ikiwemo kuboresha urari wa biashara kukabiliana na athari za *COVID-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa *Niobium* na Kiwanda cha *Ferroniobium,* ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs 7,000.* Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million)* uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(Modern Manufacturing Plant and Smelter)*. Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itakuwa itachangia huduma za kijamii *(Corporate Social Investment in Community)* na chanza cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Madini Dkt. Doto Biteko na Naibu wake Dkt. Stephen Kiruswa na watendaji wote wa Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Wizara na wadau wa sekta ya madini kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kwenye uchimbaji wa mawe ya kutengeneza saruji *(gypsum),* na bidhaa nyingine huko Makanya, Mkoani Kilimanjaro, na maeneo

mengine hapa Tanzania. Madini haya ni muhimu kwani hugusa maisha ya Mtanzania moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, saruji itokanayo na madini haya hutumiwa na idadi kubwa ya Watanzania kwenye ujenzi wa nyumba, miundombinu ya maji ya kunywa na umwagiliaji, barabara na maghala.

Mheshimiwa Spika, mawe ya kutengeneza saruji, chaki, *gypsum powder, plaster of Paris (P.O.P)* na mbolea ya kilimo ya kupambana na magadi hupatikana katika eneo la Makanya na maeneo mengine ya Tanzania kama Kilwa (*Cement* ya Dangote), Dodoma, Tanga, Singida na maeneo mengine. Katika maeneo haya kuna kiasi kikubwa cha rasilimali ya mawe ambayo hutumika kutengeneza saruji (sementi) viwandani. Kwa maoni yangu, bado uchimbaji huu haujawa na tija tarajiwa.

Mheshimiwa Spika, wapo watu wengi ambao wameibukia kuwa matajiri wakubwa kutokana na kujihusisha na kazi hii ya uchimbaji wa mawe haya ya kutengenezea saruji *(cement)* katika eneo la Makanya na maeneo mengine yaliyotajwa hapo juu. Kwa maoni yangu, madini haya hayajapewa kipaumbele kikubwa, kwani bidhaa zake kama saruji ina mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi yetu. Idadi ndogo ya wachimbaji wazawa hushiriki katika biashara hii muhimu kutokana na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuchimba mawe haya ni ngumu na sasa ni wakati muafaka wa kuwashirikisha wachimbaji wazawa kwa kuwawezesha kushiriki katika shughuli hii ili kujiongezea kipato na kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, changamoto inayowakabili wachimbaji wazawa ni matumizi ya teknolojia za kizamani,

upatikanaji wa zana za kisasa za uchimbaji, na mitaji midogo kwa kundi hili.

Mheshimiwa Spika, bei ya zana za uchimbaji ni kubwa, na vilevile hutozwa kodi kubwa. Hapa nchini Tanzania ni wafanyabiashara wachache wanajihusisha na biashara ya zana za uchimbaji kutokana na kodi nyingi kwenye bidhaa hizi. Kwa hali ilivyo sasa hivi vifaa hivi vikiingizwa nchini wachimbaji wadogo wadogo wazawa hushindwa kumudu gharama.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto nilizotaja hapo juu, naishauri Serikali yafuatayo; kwanza, Serikali ihamasishe wazawa kuwekeza katika uchimbaji wa haya madini ya *gypsum*; pili, Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha washauriane na kuondoa kodi kwa wazawa wanaoagiza na kufanya biashara ya vifaa ili viingie kwa wingi, madini yachimbwe na wengi na kodi iongezeke kutoka kwenye mauzo ya *gypsum* na *cement* badala ya ile ya kwenye vifaa.

Tatu, tunazishukuru benki za biashara kwani zimeongeza mikopo kwa wachimbaji wa madini wadogo wadogo kutoka shilingi bilioni 36 mwaka 2022 hadi shilingi bilioni 145 kufikia mwezi Machi, 2023. Hata hivyo, ninaishauri Serikali iendelee kujadiliana na benki za biashara nchini ili ziendelee kutoa mikopo ya mitaji ya kuchimba na ya kununulia vifaa vya kuchimba mawe ya kutengeneza *cement* kwa wachimbaji wadogo wadogo kwenye maeneo yote husika nchini.

Nne, Serikali ifanye tafiti za kina katika maeneo mengine Mkoani Kilimanjaro na maeneo mengine hapa nchini ili kujua maeneo mengine yenye madini ya *gypsum*. Utafiti huu uoneshe madini yako maeneo gani ili kurahisisha uchimbaji kwa wachimbaji wazawa. Kwa kufanya hivi, kanzidata hiyo itatumika kurahisisha uwekezaji na uchimbani na kuipatia Serikali kipato cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali ihamasishe wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vya kuzalisha vifaa na mitambo ya kutumika migodini hapa nchini; na sita, Serikali ihamasishe wawekezaji wajenge viwanda vya saruji katika maeneo yaliyo karibu na machimbo ili kupunguza gharama za kusafirisha mawe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji nilimwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini Mheshimiwa Daktari Kiruswa.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika bajeti yetu ya Wizara ya Madini. Kabla sijapitia hoja chache ambazo nitazipitia na Waziri wangu atakuja kufanya hitimisho na kujibu hoja zingine nitumie fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya kuwa msaidizi wa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa nafasi ya Naibu Waziri. Pia nikushukuru wewe Mwenyekiti na uongozi mzima wa Bunge ukiongozwa na mama yetu Mheshimiwa Daktari Tulia Ackson Spika wetu na Naibu Wake na ninyi Wenyeviti wetu kwa jinsi mnavyotuongoza vizuri katika Bunge hili tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa dakika hizi chache ambazo nimepewa pia kumshukuru Waziri wangu kwa uongozi wake madhubuti anavyotuongoza sisi katika Wizara hii ya Madini na watendaji wote wa wizara yetu ambayo sisi kauli mbiu yetu katika utendaji tunajiita familia ya madini. Kwa pamoja haya yote ambayo yanasifiwa katika Bunge hili ambayo tumeyafanya ni kazi ambayo imefanywa na sisi sote kama timu. Zaidi ya yote kwa kweli tumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye ametupa neema hii ya

kuwa watendaji kazi katika Wizara hii kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hoja zilizoletwa hapa kuna hoja katika vifungu viwili; kifungu cha kwanza ni kazi inayofanywa na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Taarifa yao imewasilishwa hapa na maoni yao sisi kama Wizara tumeyapokea na uzuri wa Kamati hii inayoongozwa na Mheshimiwa Kitandula na dada yetu Mheshimiwa Sylvia ni kamati mahiri sana na ambayo ushauri wao, maoni yao na mapendekezo yametufikisha hapa tulipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wizara hii ni changa imeanza tu hata haijafikisha mwongo mmoja lakini sifa zilizomiminika hapa zinaonesha ni kwa jinsi gani wizara hii iko katika safari njema ya kulipeleka taifa hili kuwa tajiri kutokana na rasilimali madini. Safari bado ni ndefu, Wachina walisema kwamba safari ya maili mia moja huanza nah atua moja. Sisi pia tumeshapiga hiyo hatua moja, na ndiyo maana mapato yamezidi kuongezeka kutoka asilimia nne wizara ilipoanzishwa kwenye pato la taifa mpaka asilimia 9.7 tuliyonayo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kujibu tu hoja chache za Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwenye Wizara hii na wale wote ambao wamechangia ambao muda hautaruhusu tuweze kutoa mrejesho hapa; Wizara yetu iko makini katika kutoa mrejesho wa maandishi pia Waziri wangu atapitia baadhi ya hoja zao. Kwa hawa wachache ambao nitawatamka waelewe tu kwamba hoja za wote zimechukuliwa kwa umakini mkubwa na zitatolewa maelezo ya kina kimaandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja moja ambayo Mheshimiwa Omary Mohamed Kigua aliileta hapa kwenye mchango wake jana, akishauri kwamba Wizara ya Madini iangaliwe kuhusu haki ya mwenye leseni na mwenye haki juu

ya ardhi. Nipende tu kumjulisha kwamba katika Sheria yetu ya Madini Sura ya 123 Kifungu cha 95 mpaka 97 imeweka bayana haki za kila mmoja. Mwenye ardhi ana haki ya kutathminiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mdhamini Mkuu wa Serikali chini ya Wizara ya Ardhi na kupewa fidia apishe eneo. Pia kuna utaratibu wa maridhiano kati ya aliyepewa haki leseni ya madini na mwenye haki juu ya ardhi. Wakiridhiana kwamba atapewa fungu fulani au asilimia kidogo wanaweza wakaendelea, kwa hiyo hakuna mtu anayepoteza haki yake kwa msingi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo la utoaji wa leseni ambalo pia alikuwa anasema kwamba kuna leseni zinatolewa halafu barabara inapita mahala halafu kunakuwa na migogoro ambayo inaonekana kwamba leseni zetu zinakwaza uwekaji wa miundombinu ya barabara. Na kwa hili nipende tu kumwakikishia ya kwamba hili si tatizo, sheria zipo. Barabara inapopita sehemu yenye madini kuna utaratibu mzima na umeshatumika wa kumfidia mwenye eneo lenye madini barabara iweze kupita. Kwa hiyo hilo pia lina maelezo yanayoeleweka na sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Bryceson Tumaini Magessa katika mchango wake jana aliongelea suala la asilimia ya fedha ya maendeleo iliyotolewa katika Wizara yetu mwaka huu, hasa *STAMICO,* kuwa imeshuka. Nipende tu kumjulisha kwamba fedha za maendeleo kwenye sekta ya madini zinatengwa kulingana na miradi iliyoainishwa. Katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 kulikuwa na fedha nyingi ya miradi ya maendeleo ambayo ilikuwa bado haijatolewa, na sasa hivi zimetolewa miradi inaendelea. Hivyo ilioongezewa kwa mwaka huu wa 2024 ni hela ambayo itaenda kuendeleza miradi yote iliyokusudiwa kwa taasisi ya *STAMICO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yake nyingine alikuwa anaelezea kwamba iainishwe kwamba *STAMICO*

inapenda kugawa mitambo ambayo inaagizwa kwa fedha hizi za maendeleo, kwamba inaenda kugawiwa kwa usawa katika nchi nzima. Nipende tu kumwakikishia Mheshimiwa Mbunge kuna  mitambo mitano ambayo ilishaagizwa kwa fedha za mwaka huu na kuna mitambo ambayo imewekwa kwenye fedha tunazoomba Bunge lako Tukufu lipitishe leo hapa. Mitambo hiyo itagawiwa  kwa usawa kulingana na mahitaji ya kila eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambapo mitambo hii mahususi kwa ajili ya kusaidia wachimbaji wadogo itakwenda kusaidia kufanya utafiti kwa bei nafuu na kwa masharti nafuu na ili wachimbaji wetu waache uchimbaji wa kubahatisha wa ramli bali wachimbe katika maeneo ambayo taarifa sahihi za kijiolojia zimeshapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda ni mfupi na hoja zingine Waziri wangu atakuja kuzipitia…

**MWENYEKITI:** Kimsingi muda wako umekwisha, lakini unaweza ukahitimisha hoja yako.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende basi kuhitimisha hoja hii kwa kuendelea tu kusisitiza kwamba, sisi kama Wizara ya Madini chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wetu tumejizatiti kuhakikisha kwamba maono ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ya kutamani kuona sekta hii ikikua na kuwa moja ya sekta zinazozalisha rasilimali fedha za kuleta maendeleo katika nchi hii, zinakwenda kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu tumepanua uwanda wa uwekezaji kutoka madini yale tunasema *traditional,* yale ambayo yamezoeleka kama dhahabu na vitu kama alivyosema Profesa Muhongo, kwenda kwenye madini ya kimkakati ambayo wote ni mashuhuda wameona mikataba mikubwa mitatu iliyosainiwa

mwezi huu wa Nne na Wawekezaji wa Madini ya Mkakati na Madini adimu ambayo uwekezaji wake ulikuwa ni zaidi ya dola milioni 667, huo ni uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu kwenye mitandao nimalizie, walikuwa wanadhani Tanzania imepigika kwa sababu ya kukubali kuuza migodi yenye madini ya thamani kubwa kwa dola milioni 667. Ile ni gharama tu ya kuwekeza, miradi ile ambayo mingine ina miaka mpaka 18 mpaka 20 katika uwekezaji thamani yake ya mapato yatakayoingia katika Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ni thamani kubwa mno ambayo hata makadirio yake bado hayajaweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila aina ya madini yatakayogundulika kama Profesa alikuwa anasema mnajua aina 17 za *rare earth element* ambazo pengine mmepewa tu leseni bila kujua kuna madini gani au mtapata nini, ndiyo tunajua. Tunajua madini hayo yote na ile Mikataba asilimia kumi na sita ya Serikali ni asilimia ambayo imetengwa na inasimamiwa kupitia kampuni tanzu ambayo Serikali na wawekezaji wanaweka. Kila aina ya madini yanayopatikana kwa sababu bodi zipo zinazosimamia, zinathaminiwa na Serikali inakwenda kupata haki yake na Watanzania wanaendelea kuneemeka kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru kwa kunipa nafasi na niahidi tu kwamba sisi tutaendelea kufanyia kazi maoni yote na ushauri uliotolewa na Bunge lako Tukufu na niwaombe kwa moyo mmoja na kwa dhati wakubali kutupitishia bajeti yetu, tuweze kupiga kazi ambayo Mama Samia ametuamini na ametupa dhamana tuifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini.

Sasa namwita mtoa hoja, Dkt. Doto Mashaka Biteko. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuhitimisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Wizara imepokea michango ya Waheshimiwa Wabunge waliyoitoa kwa kuzungumza na walioandika. Tumepata ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo ni muhimu kwetu katika utekelezaji wa majukumu yetu kama Wizara na katika usimamizi wa Sekta yetu ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla ushauri na maoni yaliyotolewa au mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ya muhimu sana kwetu na yana lengo moja tu kuimarisha Sekta ya Madini na kuifanya sekta hii ichangie zaidi kuliko inavyochangia hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliyopata nafasi ya kuchangia Hotuba yangu. Jumla ya Wabunge 30 wamechangia Hotuba hii kwa kusema na kwa kuandika, ambapo Waheshimiwa Wabunge 29 wamechangia kwa kuzungumza na Mbunge mmoja amechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii vilevile kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba hoja zote zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge kwenye mjadala uliokuwepo hapa toka jana, Wizara tumezichukua kwa uzito wa aina ya pekee na kwa kweli hakuna hoja hata moja tunayoipuuza au tunayoifanya kuwa ndogo, zote tumezichua

kwa uzito wake na kwetu sisi wametupa kazi ya kwenda kufanya katika kipindi hiki cha mwaka fedha ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kuzitolea ufafanuzi hoja zote kwa sababu iliyo dhahiri kwamba muda hautoshi, hoja ni nyingi na maelezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge yote ni ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi mchache kwa mambo ya jumla na mambo mahususi pengine kwa mifano tu. Kabla sijafanya hivyo naomba tena nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa jukumu la kusimamia Sekta hii ya Madini. Nimshukuru sana Dkt. Philip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakituelekeza kutekeleza mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata pongezi nyingi katika michango ya Waheshimiwa Wabunge. Tunazichukua pongezi hizo kwa tahadhari kubwa ya mgema kusifiwa tembo asije litia maji, lakini kuwaeleza tu Waheshimiwa Wabunge, kama kuna watu wanastahili pongezi ya mafanikio ya Sekta hii ya Madini, wa kwanza ni Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania; wa pili ni Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania; na wa tatu ni Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kazi zote tunazozifanya zinatokana na maelekezo ya viongozi hawa ambayo nia yao ni kuiona sekta hii inakwenda mbele na sisi tunafanya kazi ile ambayo wametutuma. Kwa kweli

naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi hizo. Nataka niwahakikishie kwamba pongezi walizotupa na changamoto walizotupa zitatuongezea nguvu zaidi ya kufanya kazi ili tutakaporudi hapa mwakani Mungu akipenda, basi sekta hii ije ieleze mambo yaliyo bora zaidi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyashauri katika michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nisije nikasahau kuwashukuru sana sana wasaidizi wangu Wizarani. Nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kiruswa, Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna wa Madini, Watendaji wote wa Taasisi za Wizara zilizoko hapa ambao kwa kiwango kikubwa wao ndiyo wasimamizi wakuu wa mambo yote ambayo tumeyafanya Wizarani. Naomba niwashukuru wafanyazi wote wa Wizara kuanzia kada ya chini mpaka ya juu kwa kuwa naamini bila wao tusingefika hapa. Nawashukuru sana kwa *support* wanayonipa Wizarani na nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awabariki sana wao na familia zao ili waendelee kuchapa kazi hii kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameendelea kutamani itokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee mambo ya jumla machache. Jambo la kwanza limeelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Kwanza, tunapaswa kufanya zaidi ya hiki tunachofanya, wote tunakubaliana, ni kweli tunaweza kuhubiri kwamba tuna mafanikio, lakini maoni ya Waheshimiwa Wabunge na Watanzania ni kwamba bado hatujafanya vizuri zaidi. Tufanye vizuri zaidi kwa kuongeza mchango wa Sekta ya Madini, lakini tuwasaidie wachimbaji wadogo na tuvutie uwekezaji mwingi zaidi nchini ili tuweze kupata zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameenda mbali zaidi, wamekuja na mfumo mwingine wanaopendekeza na nakubaliana nao kwamba ni muhimu

sasa Serikali na yenyewe iwe mwekezaji. Tukubaliane hapa jambo moja ile dhana ya zamani ya kuwaona Watanzania wao kazi yao ni kuuza vitunguu, juisi, madini ni ya watu wengine Bunge hili leo limethibitisha tumehama. Wote tunawaona Watanzania kama watu wanaostahili kupewa fursa na wakipewa fursa tutapata mapato kutokana na wao na hiki ndicho kinachotupa ujasiri wa kusimama hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona watu wanasema leseni zisizoendelezwa zifutwe wapewe watu wengine, hiki ndicho tunachotaka ku–*empower* watu wetu na leo nawaambia wenzangu pale Wizarani kwamba ni vizuri tukaweka maono makubwa hadi tuogope *if you have a vision that doesn't scare you* hiyo *vision* ni ndogo sana. Tuwe na maono makubwa yatutishe wote mpaka tufike mahali tuseme hili ninaloliweka kweli nitalifikia? Ili litupe kazi ya kwenda kulisimamia kwa nguvu zote bila kupumzika na nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge sekta hii kama Wabunge wanavyosema, itachangia zaidi kwa sababu *potential* ipo na nitawaambia baadhi ya maeneo ambayo tunayaona ni *potential* yapo kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa kipindi cha zaidi ya miaka 15 iliyopita hatukuwahi kufungua mgodi mkubwa, tunaingiza kwenye *pipeline* migodi mipya mingine ambayo Wabunge wameona tumesaini mikataba na niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge wale wanaosema kwamba tumeingia mikataba, *free courage interests* hatuwezi kupata, nataka niwaambie iko migodi imeanza kulipa *free courage interests* hapa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie pia kwenye Bodi ya Makampuni yote tuliyoingia ubia siyo kweli kwamba hatuna Wajumbe kwenye Bodi. Tunao kwenye bodi na kwenye mikataba ile hata kwenye *management* kuna watu tunateua kuwaingiza na kuna baadhi ya watu ili mgodi uweze kumteua ni lazima awe *approved* na Serikali, huko

nyuma haikuwa hivyo, ilikuwa mtu mwenyewe mwenye leseni anateua watu wanaendesha shughuli halafu wewe huwezi kujua. Hata *financial model* tunafanya *joint financial modeling* hafanyi peke yake mwekezaji, tunajua kila aina ya madini, kila aina ya kitakachochimbwa na faida tutakazozipata ndiyo maana tunaweza tuka-*project* tutapata kiasi gani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan iko makini sana kulinda mali za Watanzania, kuhakikisha kwamba hatuwezi kuona tunapoteza hata milimita moja. Nafahamu yako mambo mengine ambayo kadri tunavyoendelea tutaona tuna mahali fulani pa ku–*improve*. Hili nilieleze kurekebisha sheria kwa maoni yangu mimi si dhambi, kurekebisha sheria ni uungwana, kwamba huwezi kukomaa na jambo ambalo *practically* halifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tukiliona jambo ambalo tukienda *site* halifanyi kazi tunarudi hapa kwa wale wanaotunga sheria tunawaambia jamani mtusaidie hili jambo huko *site* halifanyi kazi na tunazungumza kwa haki kabisa na Waheshimiwa Wabunge wamekuwa rahimu wanatukubalia, tunarekebisha. Lengo ni kuifanya sekta hii ikue, hatufanyi jambo lolote la kuonyesha kwamba Serikali ina mabavu zaidi tufahamu Waheshimiwa Wabunge, asilimia kubwa ya Sekta ya Madini inaendeshwa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi ili iweze kufanya kazi, ni lazima uiwekee mazingira rafiki ya kibiashara, upunguze userikali, uwe mfanyabiashara na wewe, *STAMICO* yuko hapo anafanya kazi ya kuwekeza kwa niaba ya Serikali, anafanya biashara kwa niaba ya Serikali, lazima akili yake na yeye afikiri kibiashara. Leo tunapata kandarasi kwa mara kwanza toka tumepata uhuru, *STAMICO* anapata kazi za kufanya uchorongaji anapambana na makampuni makubwa ya nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huku ndani ukija *STAMICO* anataka kununua kipuli kwa mfano *rig machine* imeharibika kitu kidogo kinahitaji labda dola laki moja spea. Wewe ukirudi huku ndani unataka ufate Sheria ya Manunuzi ambayo itatangaza tenda siku 14, wakati kuna mkandarasi mwingine kifaa kimeharibika leo, kesho saa tisa kimekuja amefunga, biashara inaendelea, hawezi kufanya biashara, ndiyo maana Mheshimiwa Rais akasema tuiangalie na Sheria ya Manunuzi ile ambayo inazuia biashara, tuirekebishe. Nataka niwahakikishie Wizara ya Fedha wanafanyia kazi hiyo ili tuwe na sheria ambayo ni rafiki itakayoruhusu biashara hapa nchini ili mwisho wa siku sekta hii iweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa habari ya *GST,* asingeweza kufanya utafiti kwa sababu ya sheria aliyokuwa nayo, kazi yake ilikuwa ni ku– *rospect* peke yake anaishia hapo, *explorations* haikuwa kazi yake, tulikuja hapa baada ya maoni ya Waheshimiwa Wabunge, tukaleta hoja wakatukubalia, tumebadilisha sheria tumempaka Mamlaka *GST,* sasa kwa Bunge hili aweze na yeye kufanya utafiti hasa kwa madini mkakati kwa sababu lazima tukubaliane dunia inaelekea huko. Sasa hivi *GST* anafanya *explorations* na ataingia mikataba na makampuni mengine binafsi na Serikali itaweka fedha pale kwa ajili kuweza kumpa mamlaka zaidi ya kufanya utafiti. Nataka niwaambie hili jambo ni jipya, twende nalo taratibu, lakini mwisho wa siku tutaona kile tulichokusudia kukipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gambo na wengine wamezungumza juu ya minada, naelewa *concern* ya kubadilisha kanuni ile ya Mererani *controlled area* ni ya kuzuia madini yote kuuzwa nje ya Mererani. Lengo lilikuwa ni kufanya Mererani uwe Mji wa kuchangamka. Mheshimiwa Rais ameshatupa maelekezo na tumelifanyia kazi. Nataka niwaambie tunarejesha minada ya madini, tunarejesha

maonyesho ya madini ya vito hapa nchini kama ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliacha kufanya hivyo nadhani ilikuwa mwaka 2017, tunarejesha sasa na tunaweka utaratibu na hivi ninavyozungumza tuna timu ya wataalam ambayo imekwenda kuangalia minada mingine inavyofanyika Thailand, India ili tuweze kufanya jambo hili na wale wote wanaoendesha minada huko duniani wako wengi wamekubali kuja kutuendeshea minada hii ili tuweze kuwapa bei nzuri zaidi wachimbaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusilaumiane, tuamini kwamba kila jambo tunalolifanya nia yetu ni njema kuifanya sekta hii ikue. Nataka niwahakikishie Wabunge kwamba mambo yote haya yatakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja limezungumzwa la migogoro na kwamba Wizara kunapotokea mgogoro hatua ya kwanza tunaenda kuwafukuza watu na kwamba kuna mahali pengine wachimbaji wakipata madini wanakwenda kuwafukuza. Tuweke rekodi sahihi, toka Serikali ya Awamu ya Sita sikumbuki eneo lolote ambalo wachimbaji wadogo wamefukuzwa. Nataka niwaambie eneo ambalo wachimbaji wadogo wanaweza kusimamishiwa biashara ya uchimbaji kunakuwa na sababu za kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Getere amezungumza hapa Kinyambwiga, Kinyambwiga usingeweza kuruhusu waendelee kuchimba kwa sababu ni eneo ambalo watu wenyewe walitaka kuonyesha wana nguvu kuliko hata wasimamizi wenyewe. Tumepeleka Polisi pale, Polisi amepigwa, tumepeleka walinzi, walinzi wamepigwa. Hatua ya kwanza, ni ku–*restore peace* ili uweze kuchimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuchimba mahali penye mapigano na lazima niwaombe wachimbaji wetu nchini waelewe kwamba Serikali hii inatoa mazingira yote ya kuchimba, tunafuta maeneo mengi ambayo Serikali inalaumiwa tuwapatie wachimbaji wadogo, haiwezekana tena hata wale wanaokuja kusimamia pale na wao waweze kufanyiwa vurugu. Tulifanya hivyo kwa sababu moja na baada ya amani kurudi mgodi ule tuliufungua na biashara inaendelea. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuendelee kutoa elimu kwa wachimbaji wetu kwamba, madini haya ni yetu tuyachimbe kwa amani yaweze kutupatia manufaa na mwisho wa siku tuweze kupata faida ambayo tunakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie jambo la *refinery* kwa sababu ni jambo kubwa. Katika Sheria tulizorekebisha mwaka 2017, Serikali ilielekeza au Bunge lilielekeza kwamba sasa madini yote yaongezwe thamani hapa nchini. Kazi ya kwanza ilikuwa ni kuvutia watu waje wajenge mitambo ya kusafisha dhahabu ili tupate *refinery*. *Refinery* ili uweze kupata *certifications process* yake ina inachukua muda mrefu, wako waliyofikia hatua ya *ISO,* wako wengine wanakamilisha taratibu ili mambo haya yaweze kufanyika. Sasa tumefanya nini sisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichoamua na Benki Kuu walikuja kwenye Kamati ya Mheshimiwa Kitandula, wakatoa taarifa, kanuni ya kununua dhahabu tayari imekamilika na wameanza kununua dhahabu na hivi ninavyozungumza wameshanunua kilo mia nne kama Benki Kuu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka sasa tunakamilisha taratibu zilizoko kwenye *refinery* ili tuweze kuanza kununua dhahabu kama Serikali na kuanzisha hicho kinachoitwa *National Gold Reserve* kwa ajili ya kuhimarisha *currency* yetu. Tutaenda taratibu lakini tunataka twende kwa

uhakika ili makosa yaliyotokea huko nyuma yasije yakajitokeza. Wale wenye *refinery* nawaomba wenye mabenki wawape muda, kwa sababu kuna mambo mengine ambayo ni kisera ambayo bado tunayarekebisha. Kwa mfano ni lazima kwenye *refinery* uweke *incentive,* tumepunguza kupitia Bunge hili mrabaha kwa wale wanaouza dhahabu kwenye *refinery* kutoka asilimia sita hadi asilimia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia gharama ya ku–*refine,* isiwe kwa mchimbaji iwe kwa *BOT* na Benki Kuu wamekubali kuchukua gharama, lakini tunaangalia vile vile kama *inspection fee* tunaweza tukaona kiasi fulani kibaki kwa ajili ya *refinery* ili mchimbaji anapopeleka madini yake asipate gharama yeyote. Kwa kufanya hivyo dhahabu itakuja. Mwisho wa siku kwa sababu sheria inaturuhusu, tutazuia kabisa kama nchi nyingine kusafirisha dhahabu ambayo haijasafishwa kwa sababu viwanda vya kufanya hivyo viko hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nirudie tena kuwashukuru sana sana Waheshimiwa Wabunge wote kwanza kwa namna wanavyotusaidia kusimamia Sekta ya Madini. Mimi huwa nawaambia wenzangu sekta hii hatusimamii Wizara, tunasimamia wote, maoni na michango ya Waheshimiwa wabunge ndiyo inayotufanya sisi twende kwenye *drawing table* tuone jambo gani turekebishe na jambo gani tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata haya mambo mengine, Mheshimiwa Hassan amezungumza habari ya *cyanide* na *mercury*, nilieleze tu tulishapitisha azimio hapa la kupiga marufuku matumizi ya *mercury* na matumizi ya *cyanide* na *mercury* ni tofauti, lakini vile vile *recovery* ya dhahabu labda tu kwa taarifa ya faida ya Bunge, *recovery* ya *mercury* ni ndogo ni chini ya asilimia ishirini wakati *cyanide* hutumii kwa mkono kama unavyotumia *mercury,* yenyewe unatumia

*either* kwa *VAT leaching* au kwa *CIP* au *CIL.* Hii ni ya kiwanda kabisa siyo uchenjuaji wa kawaida kama wa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe nchi nyingi sana na wanaotuzunguka wamehama kwenye matumizi ya zebaki kwa sababu ni hatari zaidi kwa afya za watu, tuwa-*support* watu wetu kwamba waanze kutumia teknolojia ya kisasa kwa ajili ya uchenjuaji wa dhahabu badala ya kutumia kemikali ambayo ina athari kwa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema maneno hayo nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi, lakini vile vile nikushukuru sana kwa namna ulivyotusimamia pamoja na Mheshimiwa Spika, Naibu Spika kwa namna ambavyo mnatuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba sasa Bunge lako likubali kutupitishia fedha hizi ili tuweze kwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na inaungwa mkono hatua inayofuata Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Katibu *(Makofi)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Kamati yako ijielekeze katika Kitabu cha Pili, Matumizi ya Kawaida, Fungu Na. 100 Wizara ya Madini, ambalo liko ukurasa wa 628 katika kitabu, pia Waheshimiwa Wabunge wakifungua katika kishikwambi lipo ukurasa wa 714.

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*................................Sh. 5,200,471,167

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na kuna Wabunge ambao wameomba kupata ufafanuzi wa mambo ya kisera kwenye eneo hili, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba ufafanuzi. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa ya kuuliza masuala ya kisera katika Wizara hii ya Madini. Tunaipongeza Serikali kwa kazi kubwa na Wizara ya Madini kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya, hususan sasa hivi kuna uwekezaji mkubwa sana katika sekta hii ya madini. Katika uwekezaji huu kuna maeneo ambayo sasa hivi wanayatwaa kwa ajili ya uchimbaji wa *rare mineral hub* hususan na kwangu kule Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto imekuwa ni mchakato wa utwaaji wa ardhi mpaka kuja kuvuna yale madini na wananchi wamekuwa wanataabika kwa muda mrefu sana. Sasa nilitaka nimuulize Mheshimiwa Waziri wamejipangaje kimkakati na kisera kuhakikisha kwamba haki za wananchi wale zinalindwa na ucheleweshwaji upungue ili wananchi waweze kunufaika na zile fidia ambazo wanazipata kutoka katika ardhi yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile hilo ni tatizo la maeneo mengi au ni kwako Kigamboni?

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeliuliza ni suala la kisera tu ni suala la uwekezaji *vis a vis* kulinda haki za wananchi ambao maeneo yao yanatwaliwa kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya madini.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa kwa sababu maeneo yanatwaliwa sehemu nyingi hii changamoto ipo maeneo mengine au ipo kwako tu Kigamboni? Maana kama ipo kwako tu peke yake siyo suala la kisera hilo, hatuwezi kutunga sera kwa ajili ya Kigamboni peke yake, kwa hiyo nadhani umenielewa hoja yangu. Mheshimiwa nakupa tena nafasi usiwe na wasiwasi.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetolea *case study* ya kwangu Kigamboni kwa hiyo kama lakini nadhani Mheshimiwa Waziri amenielewa.

**MWENYEKITI:** Sasa kama ni hivyo, kama ni hoja ya Kigamboni inabidi liulizwe kama swali ili ujibiwe mahsusi kuhusu huko. Kwa sababu kama ni sera kwamba nchi itatunga sera kwa ajili ya Kigamboni peke yake itakuwa kidogo mtihani. Kwa hiyo, utauliza kama swali ili Serikali

ikupatie majibu mahsusi kwa ajili ya wananchi wako wa Kigamboni.

Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni pamoja na sheria ambayo inaruhusu *GST* kufanya utafiti, tumefanya marekebisho ya sheria ili kuiongezea Wizara nguvu ya kunyang'anya leseni kwa wawekezaji ambao wamehodhi maeneo kwa muda mrefu lakini hawajayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kutoka kwa Serikali, hilo limetekelezwa kwa kiwango gani na kama Wizara wanaweza kutupa mifano miwili, mitatu ambayo inaonesha utekelezaji wa sera hii ambayo tuliitungia sheria, hussani kwenye mradi wa Liganga na Mchuchuma kama moja ya *case study* ambazo Wizara nataka waoneshe utekelezaji wake. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, yakiishaanza maeneo mahsusi kwa Kanuni zetu inanipa wasiwasi kidogo. Kwa nini? Kwa sababu kwenye Kanuni hii lazima usimame kwenye jambo la kisera, sasa likiwa ni jambo moja inakuwa kidogo mtihani, ukishaanza hususani kwenye Jimbo langu, ukishaanza hususani barabara ya kutoka hapa na pale inakuwa kidogo mtihani. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mhagama. Kwanza ni kweli kwamba sheria inatoa masharti mtu akipewa leseni toka amepewa anapewa muda maalum, kwamba baada ya muda fulani anatarajiwa awe ameanza kuendeleza eneo hilo, kama hakuendeleza basi walau atoe taarifa kwa nini hakuwahi kuendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengi sana ambayo yalikuwa hayajaendelezwa na ambayo Tume ya Madini kwa kutumia sheria hiyo imeshayafuta, tulishafuta zaidi ya leseni 5,000 za aina mbalimbali ambazo watu walikuwa hawaendelezi. Sasa kwa umahsusi huo huo, kwamba yako maeneo ambayo labda yaliingiwa na mikataba kabisa ambayo inatufunga kwa hiyo lazima uangalie pia na upande huo wa pili ili usije ukasababisha kupelekana Mahakamani na kuchukua muda mwingi badala ya kujadiliana na kuyamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo alilolisema Wizara tunalifanyia kazi na tumeshafuta leseni nyingi na tunaendelea, hata huko kwenye makaa ya mawe tunaendelea na zoezi hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhagama naona ameketi kwa hiyo ameridhika na majibu yaliyotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Waheshimiwa Wabunge tutaendelea mpaka tutakapomaliza kazi ya kupitisha haya Mafungu kwa sababu Kanuni zetu zinataka hivyo, tukishaingia kwenye hatua ambayo lazima tufanye maamuzi lazima tumalize hilo jambo. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Ukiangalia leo unapozungumza wachimbaji wadogo Waheshimiwa Wabunge wengi humu wamezungumza kwamba na wao ni baadhi ya wachimbaji lakini hawako kwenye kundi la wachimbaji wadogo. Sasa wale wachimbaji wadogo wako wa aina mbili. Wapo hao ambao tayari Serikali imewawekea mazingira ya kuweza hata kupata mikopo, lakini wapo wale wachimbaji wanaotumia tindo, wale wadogo kabisa ambao wanahangaika sana. Sasa hao Mheshimiwa Waziri amesema vizuri kwamba *STAMICO* wamenunua mitambo mitano

ambayo wanatumia kwa wanachimbia kwa gharama nafuu, lakini wanahitaji tuwatafutie maeneo tuwapimie na tuone namna ambavyo wao moja kwa moja watachimba. Sasa mimi nilidhani ni vizuri Wizara kupitia *STAMICO* ingeweka Kurugenzi ambazo zinashughulika na hao moja kwa moja kuliko hali ilivyo sasa, ambayo nadhani itawasaidia vizuri zaidi ili wachimbaji wadogo nao waweze kuendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nadhani huo ulikuwa ni ushauri, kwa hiyo ninyi uchukueni huo ushauri uliotolewa nadhani hoja ya Mheshimiwa Mbunge hapo ni kwamba kuna wachimbaji wadogo halafu kuna wachimbaji wadogo wadogo. Kwa hiyo wale wadogo wa wachimbaji wadogo muangalie namna ya kulifanyia kazi. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nipate ufafanuzi na *commitment* ya Wizara kwamba katika zoezi la kutwaa maeneo ya wananchi ili kuendeleza uchimbaji, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu maeneo mengi tu ukija amezungumza Mheshimiwa wa Kigamboni hapa najua kule Mbogo lipo, Chunya kuna malalamiko, Bunda kuna malalamiko na maeneo mengine, hii ni hoja ambayo ipo ya muda mrefu. Kwa hiyo, naomba nijue commitment ya Serikali kwamba wanapokuwa wamechukua maeneo ya watu kwa muda mrefu bila kulipa fidia na wawekezaji wanatengeneza migogoro katika meneo yale, nini msimamo wa Serikali katika jambo hili, kutwaa maeneo kwa wakati, kuwalipa fidia kwa wakati na kutengeneza na mahusiano ili uchimbaji uendelee vizuri zaidi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa ili kutenda haki naona hapo tumepata mifano ya hoja ya Mheshimiwa Ndugulile kutoka kwenye maeneo mengine, kwa hivyo hoja hii ili kutenda haki

ilikuwa ni ya Mheshimiwa Ndugulile, sasa Mheshimiwa Ndugulile nikupe nafasi.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waitara ameiweka vizuri, sina maneno mengine ya ziada kuiongeza katika hilo, tunaomba ridhaa ya Kiti chako ili tuweze kupata majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yoyote akipewa leseni kuna hatua za kufuata. Hatua ya kwanza lazima aende kwenye eneo husika lakini hatua ya pili ni kwenda kutambua yale maeneo atafute mtu amfanyie uthamini, akishamaliza kufanya uthamini kisha alipe fidia ndiyo aanze uchimbaji, huo ndiyo utaratibu. Sasa yako maeneo mengine ambayo unakuta mtu amefanya uthamini mpaka muda umepita ni kazi yetu Wizara ya Madini pamoja na Wizara ya Ardhi kuwakumbusha wale wawekezaji wote kwamba hili jambo ni lazima lifuate *workplan* ambayo wametuwasilishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niieleze tu Kamati hii kwamba utaratibu upo ni wajibu wetu kama Wizara pamoja na Wizara ya Ardhi kuhakikisha kwamba zile *valuation* zinazofanywa basi zinatekelezwa kwa wakati kwa mujibu wa *plan* waliyotuwekea. Ndiyo maana utaona maeneo mengi ambayo yana leseni tumetoa taratibu za kulipa zinaendana isipokuwa kuna *case by case* ambako labda mwekezaji amekutana na *resistance* ya watu wenye ardhi na hivyo na yeye anachelewa kwa sababu hizo, lakini kusema kwamba kuna mtu anaweza kutwaa eneo tu akaanza kuchimba bila kulipa fidia, sheria hairuhusu na tunacho kifungu maalum ambacho tumekirekebisha hapa kwamba ni lazima apate *consent* ya mwenye ardhi ili aweze kuendelea na uchimbaji.

**MWENYEKITI:** Sasa yule mwenye ardhi ikishajulikana pale kwake kuna madini fulani anaweza kuendeleza hilo eneo, maana yake nadhani ndiyo hoja ya Mheshimiwa Waitara. Kwamba hilo eneo, huyu mwekezaji imeshaonekana kwamba pale kuna madini lakini ni eneo lake lakini fidia hajalipwa na huyo, yaani lipo tu hilo eneo kwa sababu akiendeleza sasa fidia itakuwa kwamba tulishafanya utafiti, wakati tukifanya utafiti, nyumba yako ilifika hapa sasa umekamilisha kwa hiyo ulikuwa unajua maana yake tutalipa mpaka hapa, nadhani ndiyo hoja hiyo kwamba watu wakishaambiwa haya maeneo huruhusiwi kuendeleza hawapewi ile fidia kwa wakati. Nadhani ndiyo hoja iliyopo. Sasa kwa maneno uliyoyatoa ni kana kwamba hilo halipo? Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaenda kwenye umahsusi kwa maana maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Waitara ya Komalela na Nyabichune na maeneo mengine, yale yalikuwa ni maeneo ambayo mwanzo mgodi uliyahitaji, baadae walivyokuja kufanya *modeling* mpya wakayaacha nje kwamba hawayahitaji, sasa wale wananchi ulikuwa umeshawatumainisha kwamba utawalipa hiyo ardhi hauihitaji unafanyaje? Ndiyo tumekubaliana sasa kwamba hawa watu watalipwa kifuta machozi cha asilimia fulani na tumepeleka timu kule *Chief Valuer,* pamoja na watu wa Halmashauri wameshakubaliana, imani yangu ni kwamba kama mwezi wa Sita hautaisha wale watu wa Nyamichele na maeneo ya Komolela watakuwa wamelipwa kile kifuta jasho ambacho walikuwa wanasubiri kulipwa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, wanalipwa na ardhi yao wanarejeshewa?

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu. Mheshimiwa Waitara naona umesimama tena.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubali maelezo kidogo ya Mheshimiwa Waziri wa Madini. Kuna kesi mbili hapa na kwa sababu tunaenda *specific* hoja ni kwamba, eneo la Nyamichele ndiyo ambalo walitwaa kwa makubaliano kwamba watalichukua, baadaye mgodi ukasema kwamba haulihitaji, nazungumza eneo tangu mwaka 2012 hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Komalela, Numwambe Nyabichune, Kewanja ni maeneo ambayo ni ya watu, mgodi ukasema kuna dhahabu tunahitaji eneo hili halafu Wizara ya Ardhi ikafanya tathmini wakatofautiana kwa hiyo hawajalipwa mpaka leo, hiyo timu anayoizungumza Mheshimiwa Waziri siijui, wale wananchi hawaijui, ndiyo maana kila siku wakija wanasiasa hapa wanaitumia kama sehemu ya ajenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kwamba kama anaahidi kweli hao watu wanasikiliza sasa hivi Bunge hili ni kweli kwamba wamefanya tathmini watalipwa fedha yao, na kama hawalipwi, Je, warudishiwe maeneo waendeleze wenyewe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, hapa ulipofikia kwenye maelezo yako haya ya ngazi ya pili ndiyo yanatuondoa kabisa kwenye Kanuni hii ambayo inataka ufafanuzi wa aina fulani. Kwa sababu hayo ni mahsusi lazima Waziri aje nayo kama maelezo mahsusi kwa ajili ya maeneo husika. Yeye ametoa ufafanuzi wa sera inasemaje kuhusu mambo kama hayo, ndiyo maana na mimi niliongezea hapo maswali, kwamba majibu yake yakoje kwenye maeneo kama hayo, lakini sasa ukishaenda kwenye mahsusi lazima akuletee majibu mahsusi, ili asikuambie majibu ambayo hayana uhakika itabidi *either* mtafutane ama ulete swali ili

Mheshimiwa Waziri apate nafasi ya kukujibu kwa ajili ya hayo maeneo ambayo yamecheleweshewa hiyo fidia. Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka kupata ufafanuzi juu ya suala la kisera ambalo linahusiana na *cyanide* na *mercury* kwa maana moja kubwa ili matumizi ya *cyanide* yafanyike maana yake unahitaji kukusanya *raw material* kwa muda mrefu sana, siyo chini ya miezi sita mpaka mwaka ndio utumie *cyanide* kupata zile dhahabu. Sasa kwa hawa wachimbaji wadogo wadogo ambao wao wanafanya kazi kila siku ziendazo kwa Mungu, kwa kutumia *mercury* nataka Waziri anifafanulie. Je, wale watasaidiwaje ili waweze kutafuta mkate wao wa kila siku badala ya kuzuia hiyo zebaki. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais tumesaini mkataba wa *Minamata* wa kupiga marufuku matumizi ya zebaki kwenye uchenjuaji madini, lilikuja Azimio hapa na tukalipitisha, lakini tumeweka *phases* kwa kuwa yunajua uwezo wetu wa watu wetu kutumia teknolojia nyingine kufanya uchenjuaji mdogomdogo bado ni ndogo sana. Zipo teknolojia nyingi ambazo zimetumika kule Chunya tumekuta kuna wachimbaji wanatumia *shaking table* hawatumii sana *cyadine* wala kemikali yoyote, maji na *shaking table* wana-*extract* dhahabu wanaipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwamba tunawasaidiaje ndiyo kazi ambayo tunaendelea nayo. Idara yetu ya mazingira pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais tunashirikiana nao kwa pamoja kuendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wetu juu ya teknolojia mpya. Ni jambo jipya ambalo wachimbaji walishazoea *mercury* kwa muda mrefu kuwahamisha tunakwenda nao kwa awamu, ndiyo maana

hatukukurupuka kusema kuanzia kesho hakuna matumizi ya *cyanide*. Lazima tufahamu kwamba sisi ni *signatory* wa mikataba hii ya Kimataifa ni lazima tuondoe matumizi ya zebaki kwenye uchimbaji wa madini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zidadu Kungu, naona ameketi kwa hivyo ameridhika na ufafanuzi. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru na naomba ufafanuzi, maelezo na utayari wa Serikali kwenye kutekeleza sheria mahsusi, sheria muhimu zinazohusiana na sekta ya madini, *especially* rasilimali na maliasili za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Namba Sita (6) ya mwaka 2017 inayoitwa *The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of unconscionable Terms) Act, No. 6 2017,* ambayo inaipa nguvu Bunge hili katika kufuatilia kujua mikataba na makubaliano yanayoingiwa na Serikali kuhusiana na rasilimali zetu na maliasili za nchi yetu.

Mheshimiwa mwenyekiti, hususan ukiniruhusu sehemu ya pili ambayo inaipa nguvu Bunge hili Kifungu cha (4) na Kifungu cha (5) ambacho ndiyo mahsusi kabisa vinahitaji Bunge hili lipewe nguvu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba linajua kilichojadiliwa. Ukiniruhusu naomba nisome: Kifungu cha (4)(1) *For effective performance of oversight and advisory functions stipulated under Article 63(2) of the Constitution, the National Assembly may review any arrangements or agreement made by the Government relating to natural wealth and resources,* ambacho sasa ndiyo hiki kinaipa nguvu Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *procedure* za ku-*review* Kifungu cha *5(1) All arrangements or agreements on natural wealth and resources made by the Government shall, within*

*six sitting days of the National Assembly next following the making of such arrangement or agreements be reported to the National Assembly.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni siku ya saba ya kazi tangu tarehe 17 tulivyoingiamikataba mipya ya mwezi Aprili, lakini mpaka leo bado hatujaletewa hiyo kama ambavyo Kifungu hiki cha 5 kifungu kidogo cha sheria kinavyotaka tuletewe. Kwa hiyo, niombe kujua utayari wa Serikali na ufafanuzi wa Serikali ni lini sasa? Kwa sababu, bado tuko *within time,* ni lini wataleta sasa ili tujadili ili baada ya hapo ukiniruhusu, Kifungu cha 6 kinataka tukikubaliana hapa *within thirty days* Bunge hili lifanye maazimio ya kuletewa mikataba hii mipya ambayo ni ya juzi. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hebu msaidizi niletee ile sheria, sikonayo hapa mbele. Niletee hiyo sheria na vifungu alivyosoma Mheshimiwa hapa. Sasa hili la Mheshimiwa Hanje tutalirejea muda mfupi. Maana siwezi kusema ufafanuzi utoke kabla mimi mwenyewe sijaelewa vizuri hapa mbele. Nitampa nafasi Mheshimiwa Kwagilwa Reuben. Anataka na yeye ufafanuzi.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Uelekeo wa sera yetu kwenye madini ni jambo linalohusu *local content* ambayo hata hivyo imetungiwa sheria kwa maana ya kanuni, *"The Mining Local Content Regulations 2028."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi zinatutaka wachimbaji wetu wanapochimba madini yao, mathalani madini ya viwandani, wanapoyapeleka viwandani kuyauza kuwepo na bei elekezi na zisimamiwe na Serikali kuhakikisha kwamba, gharama ambayo mchimbaji ametumia kuchimba ndio gharama hizo na faida kidogo anayopata akiuza kiwandani, Serikali isimamie. Lakini vilevile inataka kuwepo na mkataba kati ya mchimbaji anaye-*supply* kiwandani na

kiwanda, jambo hili halifanyiki kama ambavyo lile la usimamizi wa bei halifanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si tu hivyo, sheria ile na sera hii inataka kwamba, kama kuna madini yanayohitajika kiwandani na yanapatikana ndani ya nchi, basi yatumike kwanza hayo kabla ya mtu ku-*opt* kuagiza nje ya nchi, na hiyo, ina sababu zake nyingi sana kwa nini tuliweka hivyo. Jambo hilo pia halifanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano mmoja; hivi sasa kumekuwa na uagizaji wa *copper* Silali ilihali tunazo *gypsum* kule Handeni na maeneo mengine ya nchi. Kwa hiyo, udhaifu wetu huu wa kuyasimamia haya ni kwa sababu mlezi wa wachimbaji wadogo ni *STAMICO* na pale *STAMICO* wachimbaji wadogo wanasimamiwa tu na meneja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka ufafanuzi, kwa nini tusiwe na kurugenzi kama ambavyo kuna kurugenzi nyingine, kwa nini pale *STAMICO* kusiwe na kurugenzi kwa ukubwa wake, ili iweze kushirikiana na Wizara nyingine ambazo zinashabihiana katika kuwalea hawa wachimbaji wadogo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni ushauri mzuri na tunaupokea. Tunaomba tupewe tu muda tuufanyie kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Tunarejea kwenye hoja ya Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Nusrat Hanje, sasa sijajua maana hapa ndio nikonayo hii, umefungua na wewe huko? Omba simu kwa jirani, fungua na wewe, ili tuwe tunaenda pamoja. Aah, wewe unayo kwenye karatasi, haya.

Hoja yako ulianzia kifungu cha 4, sio? Ili twende vizuri, ulianzia kifungu cha 4?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes*. Nimeanzia kifungu cha 4(1).

**MWENYEKITI:** Haya, kifungu cha 4(1), hebu tusomee.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *"For effective performance of oversight and advisory function stipulated under article 63(2) of Constitution the National Assembly may review any agreements or arrangements made by the Government related to natural wealth and resources."*

**MWENYEKITI:** Umeliona neno *may* kabla ya neno *review?*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio.

**MWENYEKITI:** Umeliona *may* kabla ya neno *review?*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio.

**MWENYEKITI:** Umeliona?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes.*

**MWENYEKITI:** Sawa. Sema sasa hoja yako.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote hapa tupo kwa ajili ya kusaidia hii nchi. Na kwa sababu kuna baadhi ya vitu ambavyo katika mchango wangu jana nilivieleza kuhusiana na gharama, kwa mfano mradi mmoja, *project* moja mpya ya Nguala, Songwe ambayo kuna maelezo kati ya upande mwingine na Serikali kwamba, wao

wanasema mradi una *cost* Dola, milioni 339, wanasema 320, lakini Serikali inasema 339 *difference* ni Dola 119.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa kwa vitu kama hivi ambavyo vingine pengine tungeletewa vingeondoa sintofahamu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye ku-*review* mikataba *aim* ilikuwa pia ni kujua *benefits* ambazo tunazipata nah ii mikataba ambayo Serikali inaingia, hususan ya *extractive industries* kwa sababu, ukisoma pia Sheria Namba 23 ya mwaka 2015 inayoeleza *permanent sovereignty* ambayo Watanzania wamepewa umiliki wa milele wa rasilimali, wana haki ya kujua kwa sababu, wao ndio wamiliki wa milele na sisi ni wawakilishi wao. Kwa hiyo, nilifikiri ni busara tungetumia ili tupate kwa sababu sheria imetupa *provision* hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Haya, hoja yako imeshaeleweka. Ni hivi Mheshimiwa, Kifungu ulichokisoma kiko vizuri kabisa na hoja yako pia, iko vizuri kabisa. Yaani Bunge linaweza, ukisema Bunge linaweza ni mpaka mtu kama wewe uwe umeona mahali kuna shida, maana shughuli ya kuingia mikataba sio shughuli ya Bunge. Serikali ikishaingia huko ndio Bunge linaweza, likiona kuna shida.

Sasa ukishamaliza hicho kifungu, kinachofuata kinakuelekeza utakapotaka sasa kufanya ufuate utaratibu gani. Maana yake ni nini, wewe kwa kuwa umeiona hiyo shida sasa ndio tumia hii sheria, sio kwa kusema hapa ndani, unafuata ule utaratibu halafu Bunge sasa likishafika mahali kwamba, sasa tunataka kujadili hapa kuna shida hii, kuna shida hii, lakini kwenye ngazi hii hapa aahhaa, sio sehemu ambayo tunaweza kutumia kifungu hicho. Sijui kama nimeeleweka?

Hakuna mazingira ambayo sheria hii imeweka kwamba, mkataba sasa tutaletewa hapa tutaanza kupitia kifungu, sio ambavyo Bunge linafanya kazi. Bunge letu linafanya kazi kupitia kamati zinazohusika kwa hivyo, lazima uwe umefuata ule utaratibu, lakini Bunge linaweza ndio hoja ya msingi. Kwa hiyo, sio kwamba, lazima lifanye, aahhaa, ni mpaka ikionekana kuna shida kwa sababu, la sivyo tutakuwa kila mkataba ukija tunasema lete hapa, aahhaa. Kwa hiyo, sheria imesema Bunge linaweza kwa hiyo, hoja yako ni ya msingi na ulitaka ufafanuzi wa Waziri, lakini kwa kifungu hiki acha nikusaidie mimi kufafanua kwa hiyo, nimeshafafanua.

Kwa hiyo, wewe fuata utaratibu, na hoja yako hiyohiyo nzuri fuata utaratibu, andika yale mapungufu uliyoyaona, sisi tutaitisha ule mkataba halafu tutausoma, halafu tutatumia sheria hii kufanya kazi yetu ya kibunge. *(Makofi)*

Nadhani hapo tumeelewana Waheshimiwa Wabunge? *(Makofi)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kwa muda wetu tulionao tutaenda kuyapitia haya mafungu.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..............................Sh. 5,200,471,167
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.......Sh.1,299,015,861
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*......Sh.1,972,172,391
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*.........................Sh. 645,000,594

Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*........................Sh. 998,560,585
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*..............................................Sh. 1,165,638,086
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*................................................Sh. 801,652,390
Kifungu 1009 – *Management Information Systems Unit*...................... .........................Sh. 766,186,000
Kifungu 2001 – *Minerals Division*........................Sh.53,336,243,926

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 2001 – *Minerals Division*.......................Sh. 23,172,550,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge Linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa Hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha

kazi zake. Naomba kutoa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge zima.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewahoji hapa na Wabunge ambao wamesema Ndiyo ni wengi kuliko waliosema Siyo. Kwa hivyo, bajeti hii imepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Madini na watendaji wote ambao wanawasaidia, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote na watumishi wote wa Wizara hii kwa kupitishiwa Makadirio ya Mapato na Matumizi na Bunge. Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa hayo itakapofika Julai. Pia nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao mmetoa michango yenu siku ya jana na leo na pia, Kamati yetu ya Nishati na Madini, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa kamati hii mmefanya kazi nzuri sana tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Pia kuna mambo machache hapa mbele; la kwanza ni Mwongozo ambao uliombwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane kuhusu Swali lake Namba 171 kutojibiwa kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge tarehe 25 Aprili, 2023 katika Kikao cha Kumi na Tatu cha Mkutano wa Kumia na Moja wa

Bunge, Mkutano wa Bajeti, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini aliomba Mwongozo chini ya Kanuni ya 76 na Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kuhusu swali lake Na. 171 kutojibiwa kikamilifu. Awali wakati wa kipindi cha maswali na majibu Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane aliuliza swali la Msingi Na. 171 kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; katika swali lake alitaka kujua ni lini Serikali itatangaza katika gazeti la Serikali kumbukizi ya Vita vya Majimaji, alivyoeleza kuwa vilianzia katika Kijiji cha Nandete.

Swali hilo lilijibiwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambapo pamoja na mambo mengine alieleza jinsi Serikali inavyoadhimisha kumbukumbu ya Vita vya Majimaji nchini. Katika maelezo yake alieleza jinsi maadhimisho hayo yanavyofanyika katika eneo la makumbusho ya Vita vya Majimaji katika Manispaa ya Songea kila tarehe 26 Februari ya kila mwaka. Vilevile alieleza kuwa kumbukumbu ya mashujaa kuadhimishwa na Jeshi la Tanzania tarehe 25 Julai, kila mwaka ili kuwaenzi mashujaa wetu.

Kuhusu kutangaza Kijiji cha Nandete, alieleza ifuatavyo, nanukuu, "Mamlaka ya kutangaza eneo lolote au lengo la kihistoria iko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Idara ya Mambo ya Kale, Sura Namba 333 ya Mwaka 2002, Kifungu cha 3(1) na (2). Sheria hiyo, inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya malikale kutangaza eneo lenye sifa ya urithi wa Taifa kwenye gazeti la Serikali kwa ajili ya kumbukizi ya Vita vya Majimaji, basi namshauri awasilishe ombi hilo Wizara husika ili liweze kufanyiwa kazi."

Mheshimiwa Ndulane alipopata nafasi ya kuuliza Swali la Nyongeza, alionesha masikitiko yake, ambapo alieleza kuwa swali lake halikujibiwa kwa ukamilifu kwa sababu, majibu ya Waziri ni kuwa swali lake lilitakiwa kujibiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na Utalii. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alijibu swali la nyongeza kwa

kumuondoa wasiwasi Mheshimiwa Ndulane kwa kueleza kuwa, Serikali ni moja hivyo, Wizara yake itashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, ili kumuongoza katika kufuatilia kama Kijiji cha Nandete kina sifa ya kuingia kwenye kumbukumbu za nchi yetu za maeneo ambayo yalitumika katika vita vya majimaji.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya siku hiyo, Mheshimiwa Ndulane aliomba Mwongozo wa Spika, kuhusu jambo hilo ambalo pamoja na mambo mengine alirejea maelezo ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kwamba, Wizara ya Maliasili na Utalii ndio inayohusika na suala lake hivyo, alitaka kujua iwapo Waziri wa Ulinzi alijibu swali lake kwa kadiri ambavyo swali hilo lilikuwa linaelekeza?

Baada ya maombi hayo Kiti (Mwenyekiti) kilieleza kuwa Mwongozo utatolewa badaye baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge, ili kujiridhisha kama majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri yalikuwa yanajitosheleza au hayajitoshelezi.

Waheshimiwa Wabunge, nimepitia *Hansard* ya tarehe 25 Aprili, 2023 inalo swali la Mheshimiwa Ndulane. Majibu ya Mheshimiwa Waziri pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Ndulane alipopewa nafasi ya kuuliza Swali la Nyongeza.

*Hansard* inaonesha kuwa swali la Mheshimiwa Ndulane lilitaka majibu kuhusu Lini Kumbukumbu ya Vita vya Majimaji Vilivyoanzia Kijiji cha Nandete Itatangazwa Katika Gazeti la Serikali?

Katika kujibu swali hilo Mheshimiwa Waziri alifafanua kuwa, masuala ya mambo ya kale yanasimamiwa na Wizara ya Maliasili kupitia Idara ya Mambo ya Kale, chini ya Sheria ya Mambo ya Kale, Sura Na. 333 ya Mwaka 2002. Mheshimiwa Waziri alieleza kwamba, Waziri mweye dhamana

ya Mali Kale ndiye mwenye mamlaka ya kutangaza eneo lenye sifa ya urithi wa Taifa kwenye Gazeti la Serikali.

Zaidi ya ufafanuzi huo Waziri alishauri Mheshimiwa Mbunge awasilishe maombi yake ya Kijiji cha Nandete kutangazwa katika Gazeti la Serikali katika Wizara husika, ili suala hilo liweze kufanyiwa kazi. Halikadhalika *Hansard* inaonesha kuwa alipopewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, Mheshimiwa Ndulane alionesha masikitiko kwamba, swali lake halikujibiwa kikamilifu. Kwa upande mwingine alimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuitaja Wizara inayosimamia masuala ya kale pamoja na sheria inayosimamia masuala hayo. Pamoja na shukrani hizo, Mheshimiwa Ndulane aliomba Kiti kipange upya swali lake, ili Wizara ya Maliasili na Utalii ijibu swali hilo kwa ufasaha siku ya tarehe 28 Aprili, 2023.

Waheshimiwa Wabunge, majibu ya Swali la Nyongeza yalisisitiza kwamba, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi kwa sababu, pamoja na swali lake kujibiwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara hiyo itashirikiana na Mbunge pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii na Utalii, ili kumpatia mwongozo na utaratibu unaotakiwa. Utaratibu huo utawezesha kujua kama Kijiji cha Nandete kina sifa za kuingia kwenye kumbukumbu za maeneo ambayo yalitumika katika Vita vya Majimaji.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitia *Hansard* pamoja na Masharti ya Kanuni ya 49 na 51 ya Kauni za Kudumu za Bunge, Kuhusu Maswali na Majibu, nimejiridhisha kuwa, majibu ya Mheshimiwa Waziri katika Swali la Msingi na Swali la Nyongeza yalikuwa ni kamilifu yanayoridhisha na yanayojitosheleza. *(Makofi)*

Kimsingi swali la Mheshimiwa Ndulane lilitaka kujua tarehe kwa maana ya lini kumbukizi ya Vita vya Majimaji katika Kijiji cha Nandete itatangazwa. Majibu ya Mheshimiwa

Waziri yalitoa ushauri kwa Mheshimiwa Mbunge kufuata taratibu za kuwasilisha maombi ya suala hilo, ili lifanyiwe kazi. Halikadhalika Mheshimiwa Waziri aliahidi kushirikiana na Mbunge pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii na Utalii katika kupata ufumbuzi. Majibu hayo yalikuwa sahihi na yenye kuridhisha kwa kuwa, yalilenga kupata ufumbuzi wa swali la Mheshimiwa Ndulane.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu maombo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, Kiti kilipange swali lake upya kwa tarehe na muda ambao alichagua; Mwongozo wangu ni kuwa, maombi hayo hayawezi kukubaliwa kwa sababu, swali hilo lilijibiwa kikamilifu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mwongozo huo ninayo matangazo mawili; la kwanza ni tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge: -

Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa kwamba, leo, Siku ya Ijumaa, tarehe 28 Aprili, 2023 kutakuwa na semina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji nchini na kwa hivyo, mnaalikwa wote katika Ukumbi wa msekwa. Semina hiyo, imeandaliwa na Wizara ya maji, Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa ili muweze kwenda kupata ufahamu zaidi juu ya mambo mengi yanayofanywa na Wizara hii, lakini pia na mipango yake.

Waheshimiwa Wabunge, hilo linafanyika, maana yake tukitoka hapa sote tuelekee Msekwa. Tangazo la pili linatoka pia kwa Katibu wa Bunge:-

Katibu wa Bunge anawatangazia Wabunge wote wanawake na wanaume kuwa, leo Tarehe 28 Aprili, 2023 kutakuwa na Sherehe ya Usiku wa Mwanamke wa Bunge itakayofanyika katika Viwanja vya Bunge mara baada ya Bunge kuahirishwa; sasa hii ilikuwa iwe jioni, sasa kwa sababu tutaahirisha saa hizi, maana yake Waheshimiwa Wabunge

tunatarajiwa turejee majira ya saa moja kamili katika Viwanja vya Bunge. Hapa tunasisitiza kwamba, ni Wabunge wote kwa maana ya Wabunge wanaume na Wabunge wanawake, na Wabunge wanaume watakuwa wanaongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge msikose kwa sababu, jambo hili ni jambo kubwa na ninyi mnafahamu tunaye kiongozi mahiri kabisa ambaye anatuongoza huko mbele, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, litakuwa ni jambo zuri, msiwe na wasiwasi juu ya hilo kwa hiyo, mnakaribishwa nyote. *(Makofi)*

Sasa, Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 2 Mei, 2023 siku ya Jumanne, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.41 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 2 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*